**10 APRILI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 10 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, leo hatuna maswali kwa Waziri Mkuu au leo naona pangechimbika.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Stella Manyanya.

Na. 31

**Ujenzi wa Wodi Kituo cha Afya Kihagara, Nyasa**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, lini ahadi ya Serikali ya kujenga wodi, Kituo cha Afya Kihagara itatekelezwa ili kuondoa changamoto kubwa iliyopo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu na uhitaji wa ujenzi wa wodi katika kituo cha Afya Kihagara kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa. Katika mipango ya mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali itatenga shilingi milioni 200, kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu (watoto, wanawake na wananume) katika Kituo cha Afya Kihagara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Stella Manyanya.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi na nina maswali mawili. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itajenga wodi na *mortuary* kwenye Kituo cha Afya Ndalambu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba kama *X-ray machine, ultra sound* pamoja na kujenga majengo yake kwenye Kituo cha Afya Kamsamba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge Conchester amefuatilia mara nyingi kuhusiana na ujenzi wa majengo yanayopungua katika Kituo cha Afya cha Ndalambo na ninaomba nimhakikishie tu katika bajeti ya Mwaka ujao wa Fedha 2025/2026 tumeweka mpango, kwa ajili ya kwenda kuongeza majengo katika Kituo cha Afya cha Ndalambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusiana na Kituo cha Afya cha Kamsamba, ni kweli, tunafahamu kuna baadhi ya vituo ambavyo vina upungufu wa miundombinu, lakini kuna upungufu wa vifaa tiba ikiwemo *X-Ray, Ultra-sound* na majengo ya kuhifadhia maiti. Ninaomba nimhakikishie Mbunge kwamba,

tunaendelea kuboresha upatikanaji wa vifaa tiba na majengo hayo kwa awamu na tutahakikisha tunakwenda kuboresha katika eneo hilo la Kituo cha Afya cha Kamsamba. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itapeleka *Digital X-ray* katika Kituo cha Afya Ushetu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka minne imepeleka fedha zaidi ya shilingi trilioni moja na bilioni 290 katika vituo vya huduma ya afya msingi kote nchini ili kununua vifaa tiba zikiwemo *Digital X-ray*. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Dkt. Mnzava kwamba, zoezi hili ni endelevu tutaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya vifaa tiba kwa mwaka ujao wa fedha na tutatoa kipaumbele, kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Ushetu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha za kujenga majengo ya *mortuary,* Vituka pamoja na Kirakala? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Ninafahamu kwamba, tulitoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri na hususan Manispaa, zenye mapato makubwa kama Temeke kuona uwezekano wa kutenga fedha angalau kwa awamu, kwa ajili ya kujenga miundombinu muhimu kama *mortuary*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumuelekeza na kumsisitiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke kuanza kutenga fedha kwenye mapato ya ndani, kwa ajili ya kuanza ujenzi huo. Pia, Serikali itaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya vifaa tiba, kwa maana ya jokofu na vifaa tiba vingine. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni. Jiandae Mheshimiwa Kaijage, Mheshimiwa Omar Massare.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Dalai ni moja ya kata ambazo zilitakiwa kujengewa vile vituo vya kimkakati. Nataka kujua ni lini sasa vituo hivyo vitajengwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeainisha kata za kimkakati kote nchini ambazo zinakidhi vigezo vya kuwa na vituo vya afya, ikiwemo kata ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja katika Halmashauri ya Chemba. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Monni kwamba, tutahakikisha tunatenga fedha kwenye bajeti zijazo, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo ya kimkakati.

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Kaijage.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Kituo cha Afya cha Kisorya kinahudumia wananchi wengi. Je, ni lini Serikali itaongeza wodi katika kituo hicho? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, tulijenga vituo vya afya kwa awamu ya kwanza majengo matano na tunafahamu kwamba, vituo vingi vya afya

vilivyojengwa kikiwemo Kituo cha Afya cha Kisorya vinahitaji ujenzi wa awamu ya pili, kwa maana ya wodi za wanaume, wanawake na watoto. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Kajege pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wote kwamba, vituo vile ambavyo vimejengwa kwa awamu ya kwanza tutaendelea kuvitengea fedha, kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili ili kukamilisha majengo hayo ya wodi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare, jiandae Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali iko tayari sasa kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Mwamagembe, ambayo Kituo jirani cha Rungo ni kilometa 70, na kilometa 70 tena, Kituo cha Mitundu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ikiwa kata hiyo, kwa maana ya umbali inakidhi vigezo na ikiwa kata hiyo inakidhi vigezo, kwa maana ya idadi ya wananchi katika eneo hilo, Serikali itahakikisha inaweka mipango, kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni wafanye tathmini, ili kujiridhisha juu ya vigezo na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, mpango kazi wa kuanza ujenzi kwa kutumia mapato ya ndani, lakini na sisi kwa maana ya Serikali Kuu tutaona namna ya kutenga fedha, kwa ajili ya kuanza ujenzi huo ikiwa itakidhi vigezo hivyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ahadi za viongozi wakubwa, kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Nanganga na sasa hivi tunakaribia kumaliza Mwaka wa

Fedha na wewe utakuwa ni shahidi, unakumbuka mwezi wa pili tuliahidiwa kwamba, pesa zote za kujenga vituo vya kimkakati kwenye maeneo mbalimbali zitatolewa. Je, pesa hiyo itatolewa lini kwa sababu mwaka wa fedha sasa unaelekea kwisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba, Serikali hii imefanywa kazi kubwa ya ujenzi wa vituo vya afya na Waheshimiwa Wabunge ni mashuhuda wazuri kwamba kazi iliyofanyika ni ya kihistoria katika ujenzi wa vituo vya afya na kazi hii ni endelevu. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha tunapeleka fedha, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata hiyo ya Mangaka na nimhakikishie tu kwamba, tunafahamu aliorodhesha kwenye zile kata za kimkakati. Kwa hiyo, ni suala la muda tu tutahakikisha tunapeleka fedha, kwa ajili ya ujenzi huo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Amandus.

**MJUMBE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hayupo. Kwa niaba.

**NAIBU SPIKA:** Hayupo, kwa niaba, yupo nani? Mwache Mheshimiwa Justin pale.

Na. 32

**Kupandisha Hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo Nachingwea**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA K.n.y. MHE. AMANDUS J. CHINGUILE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo Nachingwea kuwa Mamlaka ya Mji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287, (Mamlaka za Miji), Sura 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014. Mwongozo wa kuanzisha maeneo ya utawala unaanza kwa kusudio kujadiliwa kupitia vikao vya ngazi za msingi, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC)* na Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)*. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea inashauriwa kufuata utaratibu huo na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, mamlaka nyingi zilizoanzishwa bado zina upungufu wa miundombinu mbalimbali yakiwemo majengo ya utawala na huduma za kijamii, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kuboresha miundombinu iliyopo katika maeneo ya utawala yaliyopo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyamonga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri, lakini pamoja na hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Chinguile ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Mji wa Nachingwea ni mji wa kihistoria na ni mji mkongwe na maombi kwa kufuata taratibu zote yalishawasilishwa mara kadhaa. Je, kwa kuzingatia hadhi ya Mji wa Nachingwea, Serikali haioni ni wakati mwafaka sasa kwa kuipa hadhi ya kuwa na halmashauri kamili kama mji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni sambamba na hilo. Mji wa Ilula uliopo Kilolo na wenyewe una zaidi ya miaka 15 ukiwa ni mamlaka ya mji mdogo. Je, hii miji ambayo imekuwa na Mamlaka ya Mji Mdogo kama Ilula, ni lini sasa Serikali itaipa hadhi za kuwa halmashauri kamili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, Serikali ilianzisha mamlaka za miji midogo katika halmashauri mbalimbali kote nchini, lakini ili mamlaka zipande hadhi na kuwa halmashauri za miji kamili kuna vigezo ambavyo ni lazima vifikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo cha kwanza ni idadi ya wananchi; idadi ya wananchi katika halmashauri inayoanzishwa inatakiwa isipungue watu 150,000 na idadi ya wananchi wanaobaki katika halmashauri mama inatakiwa isipungue wananchi 250,000. Halmashauri ya Nachingwea ina wananchi 233,655, kwa hiyo, hata ikianzisha Halmashauri ya Mji kamili wa Nachingwea bado haitakidhi idadi ya wananchi wanaotakiwa kwa mujibu wa vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni uwezo wa mapato ya ndani; angalau 30% kwa mamlaka inayoanzishwa kuwa halmashauri. Bado Mamlaka ya Nachingwea haina uwezo wa kukidhi kigezo hicho. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea kuona kwa kadiri ya halmashauri zinavyoendelea kukua na baada ya kukidhi vigezo hivi tutazipandisha hadhi ya kuwa halmashauri za miji kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula. Kweli ni ya muda mrefu, lakini tumeshapokea maombi kutoka Mkoa wa Iringa na tunaendelea na tathmini ya kuona kama inakidhi vigezo hivyo, ili iweze kupanda hadhi hapo mamlaka itakaporidhia kuanza kupandisha hadhi mamlaka za miji midogo kuwa halmashauri. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya TAMISEMI iliagiza timu kwenda Wilaya ya Nkasi na wakasema Mamlaka ya Mji Mdogo Namanyere tumekidhi vigezo. Leo ni mwaka 2025 kutoka mwaka 2013, kama Wizara inaona haijakidhi

vigezo kwa nini wasiifute ili wananchi waendelee kuwa vijijini badala ya gharama wanazozipata kwa upande wa *TANESCO*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli zipo mamlaka za miji midogo zilizoanzishwa ambazo mpaka sasa zinakidhi vigezo, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anaongelea Mamlaka ya Mji Mdogo katika eneo la Halmashauri ya Nkasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mbunge kwamba, kupanga ni kuchagua na Serikali tumepanga kuanza na vipaumbele vya kukamilisha miundombinu kwenye halmashauri zilizopo. Tunafahamu zipo halmashauri hazina ofisini za wakurugenzi, zipo halmashauri za miji hazina majengo ya utawala na majengo ya huduma za kijamii. Tukaona ni busara kwanza kuanza na hayo majengo yakamilike na baadaye tutakuja kuanza kupandisha halmashauri zote ambazo zimekidhi vigezo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, zoezi hilo litaendelea muda utakapofika na watapa haki yao ya kuwa na halmashauri ya mji. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa *PAC*. Wewe siyo Makamu *PAC*? Hutaki jimboni wajue kuwa, wewe ni Makamu Mwenyekiti wa *PAC*? *(Kicheko)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itapandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Vwawa kuwa Halmashauri ya Mji kwa kuwa, umekidhi vigezo vyote? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba, tunafahamu zipo mamlaka ambazo zimekidhi vigezo,

lakini tumeweka kipaumbele kuboresha miundombinu ya utawala katika halmshauri zilizopo na baada ya hapo tutakwenda kuanza kupandisha hizo halmashauri nyingine. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Hasunga, wao wawe wavumilivu na kwamba, muda ukifika basi Serikali itaona uwezekano wa kuipandisha halmashauri hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa hii nafasi. Mwaka 2012, mwezi Januari, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, aliridhia kuigawa Wilaya ya Arumeru ziwe wilaya mbili kwa lengo la kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata huduma za utawala kirahisi. Je, Serikali haioni kwamba, sasa ni wakati mwafaka kutekeleza yale aliyoyasema Rais Mstaafu? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge Dkt. Pallangyo kwamba, tunatambua zipo halmashauri ambazo zinakidhi vigezo vya kugawa na pia zimeshawasilisha maombi hayo. Ninaomba nikuhakikishie mara tu baada ya kuanza mchakato wa kugawa halmashauri rasmi na baada ya kukamilisha maeneo ambayo tunakamilisha kwa sasa, tutaweka kipaumbele katika Halmashauri ya Arumeru. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Medard Matogolo.

Na. 33

**Ukarabati wa Shule Kongwe za Msingi, Chato**

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati shule kongwe za msingi katika Jimbo la Chato?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga shilingi 476,200,000, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 10 na matundu ya vyoo 77 katika Shule Kongwe za Bwanga, Bwina, Busalala, Ilemela, Itanga, Katale, Katende, Mwangaza, Nyantimba, Nyarutembo na Nyisanzi zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali imepanga kutumia shilingi 890,300,000, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 25 na matundu ya vyoo 75 katika Shule Kongwe za Bukiriguru, Busaka, Buzirayombo, Ihanga, Katete, Kibumba, Kinsabe, Katende, Kitela, Mwabasabi, Minkoto, Mwangaza, Nyakato, Nyamirembe na Nyangh'omango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha shule kongwe za msingi zikiwemo za Halmashauri ya Chato kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Matogolo.

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Pia ninatoa shukurani nyingi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia shilingi milioni 226 kwa ukarabati na kujenga madarasa manne kwenye Shule Kongwe ya Rudeba, Kata ya Iparamasa. Namshukuru Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri pia, kwa kututengea shilingi milioni 890, kwa ajili ya ukarabati wa madarasa mengine yaliyobaki. Kuna shule kongwe 169, nyingi zina uchakavu na kwa kweli fedha iliyotengwa nakubaliana nayo, lakini ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spuka, swali langu la kwanza; ninamwomba Mheshimiwa Waziri atembelee shule zote kongwe

na ninamwomba atembelee ndani ya miezi hii miwili kabla Bunge halijakwisha akatoe tamko ili ukarabati uanze.

Mhshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; fedha hizi shilingi milioni 890 zitatoka lini ili ujenzi na ukarabati wa madarasa ya shule zote kongwe ikiwemo Ilyamchele, Nyambogo, Ichwankima, Kasenga, Nyamirembe, Buzirayombo nao ufanyike kwa haraka? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani kwa kutaka kuhakikisha kwamba, katika jimbo lake Sekta ya Elimu inawekewa kipaumbele na hasa katika shule hizi chakavu, shule kongwe za msingi. Kuhusu swali lake la kwanza, ninaomba mimi na Mheshimiwa Mbunge tukae, tujadili na tupange ratiba inayotekelezeka, ili tuweze kuona tunafanyaje kuhusiana na kuzitembelea shule hizi kongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Serikali hii ya Awamu ya Sita, uwekezaji wa zaidi ya shilingi trilioni 5.1 umefanyika katika Sekta ya Elimu katika shule kongwe. Shule kongwe 832 zimeweza kufanyiwa ukarabati katika kipindi cha miaka minne na katika Jimbo lake la Chato jumla ya shilingi bilioni 1.53 zimeletwa, kwa ajili ya kuhakikisha zinakarabati shule kongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hata fedha hizi milioni 890 ambazo zimetengwa kwa mwaka huu wa fedha zimetengwa kwa ajili ya kuhakikisha zinakarabati shule hizo kongwe, lakini nitumie nafasi hii kuendelea kutoa msisitizo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha kwamba anaendelea kuzifanyia tathmini shule hizi Kongwe 169 katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge na kuziweka katika mpango na bajeti kwa ajili ya kuendelea kuzikarabati ili shule hizi ziweze kuwa katika hali nzuri na kuwanufaisha wanafunzi wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ninaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo imejenga shule nzuri sana, ambapo hata sasa hivi kule vijijini maharusi walio wengi wanakwenda kupigia picha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Mbeya wanapenda kujua, shule za *primary* (shule za msingi) kongwe ambazo hazijakarabatiwa ni nyingi sana. Ziko Halmashauri ya Busokelo, Rungwe, Kyela, Mbarali, Chunya, Mbeya DC na Mbeya Vijijini. Je, ni lini sasa Serikali itakwenda kukarabati shule hizo kongwe za msingi Mkoani Mbeya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Suma Fyandomo ambaye amekuwa akifanya ufuatiliaji mkubwa sana katika sekta ya elimu ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Mbeya wanapata elimu bora, kupelekewa fedha kwa ajili ya miundombinu, lakini kuboresha Sekta ya Elimu kwa ubora wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kutoa msisitizo kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita inafanya uwekezaji mkubwa sana kuhakikisha hata katika eneo la shule zetu hizi kongwe za msingi zinaweza kukarabatiwa na zinakuwa kaika hadhi nzuri kwa ajili ya wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema, shule kongwe 932 katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita tayari zimefikiwa na kukarabatiwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kuwa katika Mkoa wa Mbeya tutaendelea kuhakikisha kwamba tunafanya kazi ya kuzifikia shule hizo ambazo ni kongwe, kuzifanyia tathmini na kuziweka katika mpango na bajeti kwa ajili ya kuzifikia na kuzikarabati ziwe katika hali nzuri.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Stella, jiandae Mheshimiwa Minza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Changamoto iliyopo Chato ndiyo changamoto kubwa iliyopo ndani ya Wilaya ya Ileje kwenye Shule ya Msingi Iyuli, Nchala na Ilanga zilizopo Kata ya Mlale. Je, Serikali ina mpango wa kuhakikisha kwamba wanakarabati shule hizi kwa sababu ziko katika hali mbaya ambayo inahatarisha afya za watoto na walimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Stella Fiyao, kwa swali lake zuri kwa maslahi ya wananchi wake wa Mkoa wa Songwe. Ninaomba pia nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri katika Mkoa wa Songwe kuhakikisha wanafanya tathmini ya shule hizi za msingi ambazo ni kongwe na chakavu na waweze kuweka katika mipango na bajeti, tena bajeti zao wenye za halmashauri *(own source)* ili waweze kuzifikia shule hizi na waanze kuzikarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kuu nasi tutakuwa tunaendelea kuweka mkono na kuongeza nguvu ili mwisho wa siku miundombinu hii ya shule hizi iweze kuwa mizuri na ziweze kuwanufaisha watoto wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ninapenda kuishukuru sana Serikali yetu kwa ujenzi wa shule nyingi mpya katika Mkoa wa Simiyu. Swali langu ni hili, je, ni lini Serikali itakarabati Shule za Msingi Inalo, Itubilo na Mwagindu ambazo zimekuwa ni za muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Minza kwa swali lake zuri kabisa kwa ajili ya maslahi mapana ya wananchi wa Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nitumie nafasi hii kuendelea kutoa msisitizo kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri kuendelea kufanya wajibu wao wa msingi wa kuhakikisha wanawekeza katika kuendeleza miundombinu muhimu kabisa ya kutoa huduma ikiwemo katika Sekta ya Elimu. Kwa hiyo, watumie nafasi hiyo na wajibu wao wa msingi kufanya tathmini katika shule zote kongwe na kuweka katika mipango na bajeti za halmashauri zao (mapato ya ndani) ili waanze kuzifanyia ukarabati kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kuu itaendelea kufika maeneo mbalimbali kwa awamu ili kuongeza nguvu kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu ya shule hizi chakavu inaweza kuimarika na inawanufaisha vijana wetu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Minza kwamba Serikali itafika kwa ajili ya kuhakikisha shule ulizoziainisha katika Mkoa wa Simiyu ambazo ni chakavu zinaendelezwa, zinaboreshwa, zinafanyiwa ukarabati na zinakuwa katika hali nzuri.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Felista Njau.

Na 34

**Ujenzi wa Barabara ya Msinga hadi Masoka – Moshi Vijijini**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Msinga hadi Masoka ili kupunguza adha kwa wananchi wa Moshi Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Msinga hadi Masoka imekuwa ikitengewa fedha kwa kufanyiwa matengenezo ya kawaida mara kwa mara kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, barabara hii imefanyiwa matengenezo ya kawaida kwa kuchonga urefu wa kilometa 0.96 na kuchimba mifereji ya tupa maji *(mitre drain)* mita 100. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imeweka katika mipango yake ya bajeti shilingi milioni 13 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ili kuhakikisha inapitika wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya barabara katika Jimbo la Moshi Vijijini kwa kujenga, kukarabati na kufanya matengenezo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu kabla ya kuuliza maswali ya nyongeza nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini, Kata ya Uru Kusini, ambao wamepata maafa. Kuna zaidi ya kaya sita hawana makazi kwa sababu ya mafuriko na nyumba zao zimebebwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itajenga Barabara ya Kisawio mpaka Kaliwa, barabara ambayo imeleta maafa na kusababisha nyumba hizi kupelekwa na maji; ni lini Serikali itachukua mkakati wa ziada na wa makusudi kujenga hii barabara kwa sababu imekuwa inaleta adha kila mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, ni lini Serikali itajenga Barabara ya kuanzia Darajani mpaka kwa Seba, Kata ya

Kindi kwa sababu barabara hii pia imekuwa kero na uchumi wa Moshi Vijijini unategemea barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue fursa hii kuanza kwanza kumpongeza Mheshimiwa Felista Njau kwa maswali yake mazuri kabisa ambayo yanalenga kutaka kuona maendeleo katika sekta ya barabara katika Mkoa huu wa Kilimanjaro katika Wilaya ya Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inafanya uwekezaji mkubwa katika kuhakikisha inaboresha miundombinu ya barabara hizi zinazosimamiwa na *TARURA*. Ndiyo maana tutaona tangu Serikali hii ya Awamu ya Sita imeanza kazi na imeongeza bajeti ya *TARURA* kutoka bilioni 275 kwa mwaka hadi kufikia bilioni 710 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Kilimanjaro, bajeti imeongezeka maradufu. Mwaka 2020/2021, bajeti ya ya *TARURA* Mkoa wa Kilimanjaro ilikuwa ni bilioni 10.7, lakini tunapozungumza leo kwa mwaka huu wa fedha, bajeti ya *TARURA* ni bilioni 34.1. Kwa hiyo, utaona dhamira ya dhati ya Serikali kuhakikisha inafikia maeneo mbalimbali ya barabara zetu hizi za *TARURA* ili kuweza kuziboresha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali itafika katika Barabara hii ya Kisawio na Barabara ya Darajani mpaka Seba na kuhakikisha zinajengwa na kuwanufaisha wananchi kiuchumi na kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Jimbo la Newala Vijijini lina barabara nyingi ambazo zimeharibika na baadhi hazipitiki. Kwa mfano, Barabara ya Mkomatuchi – Memena haipitiki kabisa, Barabara ya Malatu Shuleni – Mchaulu – Mpalu, Mtopwa na

Chilondolo. Je, Serikali ina mpango upi wa kuhakikisha kwamba barabara hizi zinatengenezwa ili ziweze kupitika vizuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Maimuna Mtanda, kwa swali lake zuri kabisa lenye maslahi mapana kwa ajili ya wananchi wa Newala Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina nia thabiti ya kufikia mtandao mkubwa zaidi wa barabara hizi ambazo zinasimamiwa na *TARURA* (barabra zenye hadhi ya wilaya). Pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itafika kwenye barabara alizoziainisha kwa ajili ya kuzikarabati, kuzijenga ili ziwe kwenye hali nzuri na ziweze kuwanufaisha wananchi kiuchumi na kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Mhshimiwa Maganga**.**

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe….

**NAIBU SPIKA:** Ngoja kwanza, kwa nini umehama kwenye kiti chako? Ndiyo maana nimeshangaa, mimi najua siku zote wewe mwenye hela unakaa huku. Haya, endelea.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa nimekuelewa. Barabara za Mbogwe zinazomilikiwa na *TARURA* ziko choka mbaya, zimenyeshewa na mvua, zilizojengwa mwaka 2024 zimekatika kwa mvua. Je, Serikali ina mpango gani wa kwenda kukarabati barabara hizi ambazo zimekatikakatika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika,

ninaomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Maganga, kwa swali zuri ambalo linalenga kuwasaidia na kuwasemea wananchi wa Jimbo la Mbongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu Serikali ya Awamu ya Sita unaona kabisa imeongeza bajeti ya *TARURA* kutoka bilioni 275 mpaka bilioni 710 kila mwaka. Dhamira ya dhati ni kwamba, inataka kufikia mtandao mkubwa zaidi wa barabara zetu hizi za *TARURA* ili kuweza kuziboresha na ziweze kuwasaidia na kuwanufaisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata katika Jimbo lake la Mbogwe Serikali itaendelea kuleta fedha kwa ajili ya kuhakikisha barabara alizoziainisha zinaweza kukarabatiwa na kuwa katika hali nzuri na kuwanufaisha wananchi kiuchumi na kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Boma la Ng'ombe inayopita Ng'ingula – Masisiwe – Oidegenda mpaka Isanga wakati wa mvua haipitiki kabisa. Ni kwa nini Serikali isiikarabati? Kuna maeneo madogo tu kama mawili ambayo yanasababisha barabara hii isipitike muda wote. Je, Serikali iko tayari kuangalia sehemu ambazo ni korofi ili iweze kukarabati na kupitika muda wote? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Ritta Kabati, kwa swali lake zuri. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Barabara hii ya Boma la Ng'ombe itafikiwa na Serikali kwa ajili ya kukarabatiwa ili iwe katika hadhi nzuri na iweze kupitika katika kipindi cha mwaka mzima ili wananchi waweze kupata manufaa ya kiuchumi na waweze kufikia huduma za kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Reuben, kwa niaba yake Mheshimiwa Shangazi.

Na 35

**Kero ya Kukatika Umeme – Handeni Mjini**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO** aliuliza:-

Je, Serikali ina maelezo gani juu ya kero sugu ya kukatika umeme mara kwa mara Handeni Mjini na ni lini kero hiyo itatatuliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya kukatika umeme Wilayani Handeni inatokana na uchakavu wa miundombinu ya kusambaza umeme pamoja na urefu wa njia za kusambaza umeme. Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea na ukarabati wa miundombinu ya umeme, ikiwa ni pamoja na kubadilisha nguzo za miti na kuweka za zege. Aidha, Serikali kupitia Mradi wa Gridi Imara inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Mkata, Handeni ambapo kwa sasa mkandarasi yupo kwenye hatua za awali za ujenzi. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Kilindi umefikia 35% na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Mkata – Handeni hadi Kilindi umefikia 30%. Kukamilika kwa kazi hizi kutawezesha kuondoa kero sugu ya kukatika umeme Handeni Mjini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ujenzi huu wa Vituo vya Kupoza

Umeme katika eneo la Mkata, Handeni, Lushoto na Kilindi ni muhimu sana kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Tanga. Hata hivyo, miradi hii inakwenda kwa kusuasua sana. Je, Serikali iko tayari kuharakisha upatikanaji wa fedha ili miradi hii ikamilike kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; njia ya kusafirisha umeme kutoka kituo cha Mkata hadi Kilindi inasuasua kutokana na changamoto ya fidia. Ni kwamba, wale wananchi ambao wamepisha eneo la mradi bado hawajapata fidia. Je, Serikali iko tayari sasa kutoa fidia ili mradi huu ukamilike kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa maswali mawili mazuri ambayo ameuliza kuhusiana na kuharakisha ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme vya Mkata, Handeni, Lushoto pamoja na Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari wenzetu wa Wizara ya Fedha wametuhakikishia kuwa watawalipa wakandarasi hawa kwa wakati ili kufanya ujenzi wa vituo hivi vya kupoza umeme uweze kwenda kwa kasi ili wananchi wa Mkoa wa Tanga waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Lushoto ni Mradi wa Kasiga – Lushoto, ambapo patajengwa njia ya kusafirisha umeme na kituo cha kupoza umeme na tayari tumeshawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha na wametuhakikishia kwamba watatupatia fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa vituo hivyo vya kupoza umeme na njia ya kusafirisha umeme ya Kasiga – Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili la fidia; fidia ya wananchi ya kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka Mkata, Handeni mpaka Kilindi, ni takribani bilioni 2.63. Pia, tumeshawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha na wametuhakikishia watalipa fidia hii kwa sababu ile ya kituo cha kupoza umeme cha Mkata, Handeni tayari imelipwa. Kwa hiyo,

tuna uhakika na hii pia italipwa kwa ajili ya kuharakisha ujenzi huu wa njia hii ya kuharakisha umeme ambayo ni muhimu sana kwa maeneo ya Mkata, Handeni pamoja na Kilindi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Eng*. Samwel.

**MHE. SAMWEL X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniupa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Hanang ina changamoto kubwa ya umeme kukatika mara kwa mara hivyo kuathiri shughuli za uzalishaji ikiwepo uzalishaji kwenye viwanda. Je, Serikali ina mkakati gani kuondoa adha hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya hii ya Hanang upo Mradi wa Gridi imara wa kujenga kituo cha kupoza umeme kwenye awamu ya pili. Kwa sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza ya gridi imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mkakati wa kujenga Kituo cha Kupoza Umeme Hanang upo. Ni suala la muda tu kwa sababu mradi huo unatekelezeka kwa awamu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Iringa hasa Jimbo la Kalenga, kumekuwa na kukatika kwa umeme mara kwa mara na wananchi wanapata adha kwa sababu ya miundombinu chakavu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba miundombinu hiyo chakavu inarekebishwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Tunayo mikakati kwa ajili ya kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa

umeme katika Mkoa wa Iringa. Moja, kuendelea kuboresha miundombinu, kubadilisha nguzo, pamoja na kurekebisha waya chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika Mkoa wa Iringa kwenda Tunduma hadi Katavi tunao mradi mkubwa unaoitwa *TAZA* wa njia ya kusafirisha umeme ambao unajenga vituo mbalimbali vya kupoza umeme ikiwepo pale Iringa Mjini, Kisada mpaka kufika Mbeya na Tunduma. Vituo ambavyo vitaboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika maeneo yote ya wilaya ya ukanda huu kutoka Iringa, Mbeya, Tunduma mpaka Katavi; na ndio mradi ambao utakwenda kuunganisha gridi yetu pamoja na ya Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunafanyia kazi na hali ya upatikanaji wa umeme katika Jimbo la Kalenga na Mkoa wa Iringa itaendelea kuimarika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninaishukuru na kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwashia umeme katika vijiji vyote kwenye Jimbo la Tunduru Kaskazini, lakini pia na baadhi ya vitongoji vichache katika Jimbo lile. Je, sasa ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji vyote vilivyosalia ambavyo havina umeme katika Jimbo la Tunduru Kaskazini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mkakati. Kwa sasa hivi tunayo miradi ya vitongoji ambayo inaendelea katika Jimbo hili la Mheshimiwa Mbunge. Tunayo Miradi ya Ujazilizi *(IIC)*, lakini tuna Mradi wa Vitongoji 15 kwa kila Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mradi unaokuja wa Vitongoji 9,000 katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge vitapelekwa vitongoji

takribani 54. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inao mkakati wa kuendeleza miradi ya vitongoji katika Jimbo hilo, lakini tutaendelea kuwasimamia wakandarasi ili waweze kutekeleza miradi hii kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo, jiandae Mheshimiwa Butondo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika Jimbo la Mbagala, kunakosababishwa na ubadilishwaji wa nguzo kwa muda wa saa 18 kwa siku. Je, zoezi hili kwa nini lisiwe linaishia saa kumi na moja ili wananchi waweze kupata umeme kuanzia saa 12 mpaka alfajiri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli tunafanya marekebisho makubwa kwa ajili ya kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme Mbagala. Tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tutaufanyia ili kuhakikisha kwamba pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu basi tunasaidia vilevile wananchi shughuli zao za kiuchumi na kijamii ziweze kuendelea kwa kupunguza bughudha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua ulikuwa unang'aa nilifikiri Mheshimiwa Butondo kumbe ni wewe Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Mradi huu wa Gridi Imara ambao unaanzia Mkata hadi Kilindi wenye thamani ya shilingi 98,500,000,000 ni mradi muhimu sana kwa sababu dhamira yake ukiacha katikakatika ya umeme, lakini pia ni kwenda katika maeneo ambayo yana migodi na hususan katika Wilaya ya Kilindi ambayo ina migodi mingi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kuhakikisha kwamba unalisukuma jambo hili ili wawekezaji na wachimbaji wadogo waweze kunufaika na mradi huu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mradi huu wa kujenga Kituo cha Kupooza Umeme Kilindi na njia ya kusafirisha umeme kutoka Mkata - Handeni mpaka Kilindi ni mradi muhimu sana kwa ajili ya wananchi wa Kilindi na tulifika pale na Mheshimiwa Rais na aliahidi kwamba mradi huu utaendelea kutekelezeka kwa wakati. Kwa sasa mradi umefikia 30%, mkandarasi yupo *site* nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kumsimamia mkandarasi ili muda wa kukamilisha mradi ambao ni Aprili, 2026, utakapofika basi mradi huu na wenyewe uwe umekamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia, Mheshimiwa Nyamoga.

Na. 36

**Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano Lukani na Ng'uluhe Kilolo**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano Vijiji vya Lukani na Ng'uluhe - Kilolo ili kuboresha mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *UCSAF* ilifanya tathmini ya hali ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali Wilayani Kilolo mwaka 2021/2022 kwa lengo la kubaini maeneo yenye changamoto ya mawasiliano ya simu. Katika tathmini hii ilibaini uwepo wa changamoto katika Kata za Ibumu, Irole, Uhambingeto, Kimala, Mahenge na Masisiwe. Wizara ilijumuisha Kata hizo kwenye Mradi wa Ujenzi wa Minara 758 katika kata 753 unaotekelezwa kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi katika Kata mbili za Irole na Masisiwe umekamilika na utekelezaji katika kata nyingine nne unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wizara kupitia *UCSAF* ipo katika maandalizi ya kutekeleza mradi wa awamu ya kumi, hivyo Kata ya Ng'uluhe hususan maeneo ya Vijiji vya Lukani na Ng'uluhe alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vitaingizwa katika zabuni hii ya awamu ya kumi ambapo utekelezaji wake unatarajiwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2025/2026. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri na pia ninaishukuru Serikali kwa kukamilisha minara katika Kata zilizotajwa za Ilole na Masisiwe na mawasiliano yanaendelea vizuri, lakini nina maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; mnara unaojengwa katika Kata ya Kimala ulisimamishwa kutokana na mgogoro kati ya *TFS* na wajenga mnara kwamba wamejenga kwenye eneo la msitu. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kutatua mgogoro huo ili mnara ule uweze kukamilika na wananchi wa Kata ya Kimala waweze kupata huduma?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; minara mitatu ya maeneo ya Kata ya Mahenge, Ibumu na Uhambingeto imekuwa ikijengwa, lakini kwa kasi ndogo sana. Je, Serikali kwa kuzingatia kwamba uchaguzi unakaribia na baadhi ya kura zinategemea minara hiyo haioni sasa ni wakati muafaka wa kukamilisha minara hiyo ili kufanya mawasiliano mazuri na wajumbe wakati tukiomba kura?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze sana Mheshimiwa Justin

Nyamoga kwa kazi nzuri ambayo unaifanya na tunashukuru kwa *appreciation* kwa maeneo ambayo tayari tumeweza kukufikia. Nikutoe hofu migogoro yote ambayo inatokea katika utekelezaji wa ujenzi wa minara tunaishughulikia na huu pia ninaomba niseme nimeupokea na nitausimamia kwa karibu kuhakikisha kwamba unakamilika ili ujenzi wa mnara uweze kufanyika na wananchi wapate huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika minara hii mitatu, kwamba kasi yake ni ndogo; Mheshimiwa Mbunge, Kaka yangu Mheshimiwa Nyamoga nikutoe hofu kuwa Mheshimiwa Waziri, Jerry Silaa ameshatoa maagizo minara hii yote inatakiwa ikamilike ndani ya muda ambao mkataba umesainiwa hivyo *SPID* wameshaagizwa na sasa hivi utaona mabadiliko makubwa katika ujenzi wa minara hii na hata namna ya kuelekeza wananchi wakati wa uchaguzi itakuwa nyepesi kwako, lakini vilevile kwa Chama Cha Mapinduzi kwa sababu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano katika vijiji vya Mkoa wa Simiyu ambavyo havina mawasiliano? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo aliyoyataja tuna minara ambayo tayari ipo kwenye Mradi wa Tanzania ya Kidigitali, minara 758 lakini tuna minara 632. Kwa hiyo, tunatarajia kuyafikia maeneo yote ya Tanzania na bado tuna *batch* nyingine ya minara ambayo *TTCL* pia watakuja kuijenga. Hivyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Esther Midimu maeneo hayo ya vijiji vyote alivyovitaja tutakuja kutekeleza ujenzi wa minara. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zodo.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itajenga mnara katika Kata ya Mabalanga, Jimbo la Kilindi ambapo kuna mradi mkubwa wa Serikali wa shule kubwa ya kisasa ya wasichana? Ninashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zodo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Kilindi tena kwenye ujenzi wa sekondari maeneo yote yanayotoa huduma za umma ni kipaumbele chetu kuhakikisha mawasiliano yanaimarika tena si tu *2G* tunasisitiza *3G, 4G* kwa sababu vijana wetu sasa wanasoma pia kidigiti. Kwa hiyo, eneo hili pia Mheshimiwa Mbunge nimelichukua kuhakikisha kwamba wataalam wetu wanafika na kazi ya ujenzi wa mnara iweze kupangiwa muda wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi, ajiandae Mheshimiwa Mhata.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri mwaka jana alitembelea Jimbo la Ukerewe, Kata ya Bukiko na kupitia mnara wa *Halotel*. Eneo lote lile la Kata ya Bukiko lina shida kubwa ya mawasiliano na kuna maelekezo alitoa. Kuna shida gani watendaji kutekeleza maelekezo aliyoyatoa tukawaondolea tabu wananchi wa Kata ya Bukiko wenye shida kubwa ya mawasiliano? Kwa sababu mpaka sasa hakuna mawasiliano kwenye Kata nzima ile ya Bukiko. Mheshimiwa Naibu Waziri ninaomba msaada wako na ninaomba maelezo kwenye hili. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mimi na yeye tulitembelea eneo la mradi na ule mnara kwa taarifa nilizonazo *Halotel* wameweza ku-*upgrade*. Kwa hiyo, ninafikiri tu ni kazi ya kiufundi kidogo labda ku-*twist* kidogo hivi ili kuona kwamba uelekeo wake sasa usababishe mawasiliano ya uhakika katika Kata ya Bukiko. Ninaomba nipokee na nitasimamia maelekezo niliyoyaacha Kata ya Bukiko. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kata ya Napacho iliyopo ndani ya jimbo langu Mkandarasi Minara Tanzania alipewa kazi ya kusimika minara katika jimbo langu, sasa ni mwaka mmoja umepita tangu mkandarasi huyo aripoti ndani ya eneo na kutoweka. Nini kauli ya Serikali juu ya Mkandarasi huyu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mhata kwa ufuatiliaji wa ujenzi wa minara ya mawasiliano katika Kata hii ya Napacho, ninaomba nipokee na nimwagize Meneja anayehusika na kanda ile ya kusini kuhakikisha anafahamu kwa nini Mnara Tanzania hajaja kutekeleza mradi huu na ikibidi sheria iweze kufuata mkondo wake kwa sababu ameshasaini mkataba; basi tuweze kuona namna ya kumpatia mtoa huduma mwingine ambaye atatuletea mnara maeneo haya ya Napacho na mawasiliano kuimarika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Mwanyika.

Na. 37

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Mkoa wa Njombe**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa uwanja wa ndege wa kisasa utaanza Mkoani Njombe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu, Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Njombe ni muhimu kimkakati hususan kwenye kukuza uchukuzi katika usafiri wa anga kijamii, kiuchumi na kibiashara ikiwemo biashara ya mazao ya misitu, mbogamboga, matunda (maparachichi) ambayo yote hayo huzalishwa na kusafirishwa nje ya nchi. Aidha, kufuatia uboreshwaji wa Shirika la Ndege la *ATCL* uliopelekea manunuzi ya ndege kubwa ya mizigo aina ya *Boeing* 767-300 F, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* kwa kushirikiana na Mkoa wa Njombe imekamilisha uchambuzi wa eneo jipya la *TANWAT* kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege na sasa Serikali inaendelea na taratibu za utwaaji wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali imeidhinisha taarifa za awali za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambapo kiasi cha shilingi milioni 804 zimetengwa kwa mwaka 2024/2025 huku Mtaalamu Elekezi akiendelea na utayarishaji wa rasimu ya mwisho ya nyaraka zitakazotumika kwa ajili ya ununuzi ya mkandarasi atakayetekeleza mkataba wa ujenzi. Mara baada ya kazi hii kukamilika, ujenzi utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa mwaka 2025/2026 Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Kiwanja hicho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninashukuru sana kwa hatua iliyofikiwa na maelezo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa. Kwa namna ya pekee tunashukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu hii ilikuwa ni ahadi aliyoitoa kwa Wana-Njombe alipotutembelea mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza. Kwa vile Mji wa Njombe unakua kwa haraka na sasa mapendekezo ya kuwa manispaa yana ngoja maamuzi ya Serikali na kwa vile *pressure* ya ardhi katika Mji wa Njombe ni kubwa sana, eneo hilo lipo katikati kabisa ya mji. Je, Serikali inaweza kufikiria kulirudisha eneo hilo kwa halmashauri yetu ya mji ili tuweze sasa kufanya matumizi mengine ambayo ni ya muhimu sana kwa shughuli za kijamii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Deo Mwanyika kwa ufuatiliaji wake wa karibu wa Uwanja wa Ndege wa Njombe ambao kama nilivyoeleza ni muhimu sana kwa maslahi ya mkoa huo na maeneo ya nyanda za juu kusini kwa ujumla. Pili, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa nipokee shukrani alizozitoa kwa Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inaahidi na kutekeleza. Hoja yake ya mwisho amezungumzia kuhusiana na kuomba eneo hilo ambapo tutakapohamisha uwanja kama lingeweza kutumika kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria Namba 108 ya mwaka 2024 ambayo pamoja na mambo mengine imetoa mwongozo wa namna ya kufanya uendelezaji wa rasilimali za viwanja vya ndege nchini. Hivyo, mara baada utakapokamilisha uhamishaji wa kiwanja hicho Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaweka mfumo mzuri wa kukaribisha wawekezaji wa ndani na wa nje ikiwemo mwananchi mmoja mmoja pamoja na halmashauri hivyo, nitamwomba na yeye Mheshimiwa Mwanyika pamoja na halmashauri muda

ukifika basi waweze kuchangamkia fursa hiyo ili kuendeleza eneo hilo kwa maslahi ya wananchi na nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Uwanja wa Ndege wa Bukoba unaweza uka-*accommodate* ndege ndogo, lakini tuna abiria wengi sana. Ni lini sasa Serikali itajenga uwanja mkubwa na wa kisasa wa kimataifa wa Bukoba? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa Mkoa wa Kagera kuwa na uwanja mkubwa ambao utaweza kuendana na mahitaji ya sasa. Awali tulipanga kufanya maboresho katika uwanja ule uliopo ikiwa ni pamoja na kujenga jengo la kuongozea ndege pamoja na kuweka taa, lakini baada ya kubaini umuhimu mkubwa Serikali imeanza mchakato wa kutafuta eneo lingine. Tayari eneo limeshapatikana tumeanza taratibu za awali ili kujenga uwanja mkubwa ambao utakuwa ni wa kisasa na utaweza kusaidia shughuli mbalimbali za Mkoa wa Kagera na wilaya zake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza. Uwanja wa Ndege wa Musoma umekuwa ukipewa ahadi kwa muda mrefu kukamilika kwa kiwango cha lami na kama mnavyojua Mkoa wa Mara ni mkoa ambao umeshiriki katika harakati za nchi hii, anakotokea Baba wa Taifa, ili kumuenzi ni lini watakamilisha Uwanja wa Ndege wa Musoma kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa Uwanja wa Ndege wa Musoma siyo tu kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge kwa maana kama kumuenzi Baba wa Taifa, lakini pia huko ndiko kuna utalii kwa wingi lakini shughuli za madini pamoja na shughuli za uvuvi. Hivyo basi, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na mchakato wa kukamilisha taratibu za ndani kwa maana ya kuwalipa wakandarasi ili ujenzi huo sasa uweze kuendelea na ninakuhakikishia kwamba utakamilika na utakwenda kuwanufaisha wananchi wa mkoa huo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Antipas kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

Na. 38

**Barabara ya Rupiro – Malinyi – Kilosa Kwa Mpepo – Namtumbo**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA K.n.y. MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha za ujenzi wa kilometa chache za Barabara ya Lupiro, Malinyi, Kilosa kwa Mpepo na Namtumbo ambayo ni ya Ilani ya CCM?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imesaini mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa Sanifu na Jenga kwa sehemu ya Ifakara – Lupiro – Mtimbira yenye urefu wa kilometa 112 ikiwa ni sehemu ya barabara kutoka Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo hadi Lumecha Mkoa wa Ruvuma ambapo hiyo barabara yote kwa ujumla wake ina kilometa 435.8 kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya kuanza kutenga fedha ya kutengeneza hii barabara kwa sababu imekuwa ya muda mrefu. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; je, lini Barabara ya Mahenge – Liwale – Nachingwea mpaka Masasi ambayo ina umuhimu kwa sababu inaunganisha mikoa mitatu ambayo ni Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Mtwara itaanza kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; swali hili la pili huwa ninaliuliza mara kwa mara humu Bungeni, lakini bado sijapata majibu sawasawa ni kipande cha Kilosa – Mikumi na kipande cha Turiani - Mziha ni lini vitaanza kujengwa ili kusudi kuunganisha Barabara ya kutoka Tanga kwenda mpaka Morogoro na kwenda kwenye Mikoa ya Kusini? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mahenge – Liwale - Masasi ni barabara ambayo kwa sasa kimsingi haipo, lakini tulitenga katika mwaka huu wa bajeti na nimelijibu kama siyo jana ni juzi hili swali kwamba sisi kama Wizara tumeshatenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa hiyo Barabara. Nilisema pia ninaendelea kusema kwamba, kwa kuwa ni barabara yote inapita kwenye Mbuga ya *Selous* kwa maana ya Mwalimu Nyerere tuna wadau wengi ambao tunashirikiana nao ili kufanya usanifu wa barabara hiyo kabla hatujaanza kuijenga. Kwa hiyo, sisi kama Wizara tumeshatenga fedha na taratibu zimeshaanza ya kufanya upembuzi yakinifu na kuona uwezekano wa kuijenga barabara ambayo itaunganisha Mikoa ya Kusini na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili kuhusu Barabara ya Kilosa - Mikumi. Barabara ya Kilosa - Mikumi itakuwa ndiyo mwendelezo wa barabara ambayo ndiyo iliulizwa kwenye swali la msingi kutokea Songea – Ifakara kuja Mikumi, lakini watu hawa wanapokuja huku wangependa wapitie kuja Kilosa kwa ajili ya kuja Dodoma. Tayari Barabara hii imeshafanyiwa usanifu na tumeshaanza kujenga kwa awamu. Kwa mfano, kutoka Dumila mpaka Kilosa tayari na sasa hivi tunatafuta fedha ya kujenga Kilosa kuja Mikumi ili sasa tuweze kuunganisha Mikumi na Kilosa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya Serikali ya kujenga kipande cha Barabara ya lami kilometa 10 kutoka Waso kwenda Loliondo Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha lakini mpaka sasa ahadi hii haijatekelezwa. Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi hii kwa wananchi wa Ngorongoro? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli usanifu ulishakamilika na maelekezo yalishatoka kutoka kwa Makamu wa Rais kwamba barabara hiyo ijengwe na tumeshakamilisha taratibu zote. Kwa hiyo, sasa hivi tunatafuta fedha kumlipa mkandarasi malipo ya awali ili kipande hicho cha kilometa kumi kiweze kujengwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami kilometa 22 za Barabara ya Isyonje Kikondo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya kutoka Isyonje kwenda Kikondo aliyoitaja ni barabara ambayo

inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Njombe na haiishii Kikondo; kimsingi inakwenda Makete. Katika barabara hii barabara yote yenye kilometa karibu 96.4 imeshafanyiwa usanifu, na tumeshaanza kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mhesimiwa Naibu Spika, Serikali tuliamua tujenge eneo ambalo ni korofi (eneo la katikati) ni eneo la Kitulo kwenda Iniho katika ile Mbuga ya Kitulo. Kwa hiyo, tumeshaanza na mkandarasi yuko *site*. Wakati tunatafuta fedha ya kukamilisha vipande vingine kwa Mkoa wa Mbeya na upande wa kutokea Makete. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kolandoto kwenda Mhunze ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu ni barabara ambayo ipo katika mpango wa bajeti ya mwaka huu ambao tunakwenda kuumaliza na katika Bunge liliopita nilipata majibu ya Serikali kwamba barabara hiyo inaenda kutangazwa na kimsingi imo kwenye bajeti hii. Sasa nataka nipate majibu ya Serikali ni lini sasa barabara hii inaenda kutangazwa na kuanza kutekelezwa? Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumepanga iko kwenye utaratibu wa kuanza kujengwa hiyo barabara ambayo ni sehemu ya barabara zetu kuu katika nchi yetu. Tunachosubiri sasa hivi ni kuitangaza hiyo barabara kama tulivyokuwa tumeipanga kwenye mpango wa bajeti ya mwaka huu wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa, jiandae Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii barabara inayotoka Namtumbo kupita Malinyi mpaka Ifakara Serikali imetwambia itajengwa kwa awamu. Je, kwa wakati huu inaweza ikatufungulia kusafirishia wakati inajengwa kwa kiwango

cha lami basi angalau tuwe tunapita kuitumia njia hiyo kwa kiwango hicho cha changarawe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara ilikuwa imetangazwa yote. Kwa hiyo, tulitegemea mkandarasi ambaye angekuwepo angeweza kuwa anaifanyia matengenezo. Baada ya kufanya utaratibu tumeshawaagiza Mameneja wa Mikoa ya Ruvuma na Morogoro kuhakikisha kwamba kile kipande ambacho kitajengwa ataendelea na mkandarasi, lakini vipande vilivyobaki ma-*regional managers* wa-*TANROAD* wahakikishe kwamba wanazikarabati kupita kipindi chote cha mwaka. Kwa hiyo, kwa kiwango hicho cha changarawe kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Namtumbo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke, jiandae Mheshimiwa Halima.

**MHE. JOSEPHINEN J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itajenga Barabara ya kutoka Kitanga – Kigadye – Helushingo - Nyarugusu mpaka Makere kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa barabara hii ya mpakani kati ya Tanzania na Burundi inafanyiwa usanifu, lakini kilichofanyika kwa sasa ni kuunganisha kwanza Wilaya ya Kasulu na Wilaya ya kibondo ambapo Daraja lililokuwa la Malagarasi ndilo linahamishiwa pale na mkandarasi yuko *site*. Sasa wakati tunajiandaa kutafuta fedha baada ya kukamilisha usanifu kuweza kuijenga kwa kiwango cha lami na hasa tukizingatia hilo eneo ndiko kuna shamba kubwa na kiwanda kikubwa cha miwa, pia ni barabara ya mpakani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inadaiwa na wakandarasi shilingi trilioni 1.3. vilevile, kutokana na kutokulipa mnadaiwa riba ya shilingi bilioni 136; ndiyo maana barabara zimekwama. Kwa nini Mheshimiwa Naibu Waziri unawapa Wabunge majibu ya matumaini ambayo unajua hayatekelezeki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima swali hili lilikuwa la ujenzi wa barabara umeingia kwenye masuala. Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Neema William Mgaya.

Na. 39

**Barabara ya Njombe – Kibena – Madeke – Lupembe – Morogoro**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Njombe – Kibena – Madeke - Lupembe kuelekea Mkoa wa Morogoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza ujenzi wa Barabara ya Njombe – Kibena – Madeke – Lupembe hadi Mikumi Mkoa wa Morogoro kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Sehemu ya Mikumi hadi Ifakara yenye urefu wa kilometa 109 ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami umekamilika. Sehemu za Ifakara – Mbingu kilometa 62.5 na Mbingu – Chita kilometa 37.5 kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea. Kwa sehemu iliyobaki ya Chita hadi Kibena, Mkoa wa Njombe kilometa 246.44, Serikali inaendelea kutafuata fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini kwa sisi Wananjombe hususan watu wa Lupembe hii ilikuwa ni moja kati ya ndoto zao kuona Barabara inayotoka Morogoro inapita Mlimba inakuja hadi Lupembe, Njombe inajengwa na Serikali niiweke wazi kwamba wamefika kwenye hilo eneo na tayari mkandarasi anaendelea na taratibu nyingine. Kwa hiyo, kwa niaba ya Mheshimiwa Neema na Mbunge wa Jimbo pia tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo maswali yangu ni mawili. Swali la kwanza; je, ni lini hivyo vipande viwili vilivyobakia yaani upande wa Morogoro na upande wa kuja hadi Njombe Mjini vitaanza pia kutangazwa ili ianze kujengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; wakati Waziri anajibu swali namba 38 alizungumza kuhusu kipande cha Makete, Kitulo kuelekea Mbeya Barabara ya Isyonje ni kweli mkandarasi amefika na ni kweli mkandarasi ameanza kazi, lakini hivi ninavyozungumza muda huu magari mengi yamekwama barabarani kwa sababu ya hali mbaya ya barabara. Ni yapi maelekezo ya Serikali muda huu kwa mkandarasi aweze kuyanasua na barabara iweze kupitika ili wananchi waendelee na shughuli za kiuchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kujibu swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge. Katika kipindi hiki cha Masika na hasa pale ambapo tunakuwa na ujenzi tunakuwa na hizi barabara za mchepuko kwa maana ya *diversions* na maeneo mengi kwa sababu barabara inakuwa si imara sana kama barabara yenyewe mvua ikinyesha kubwa ama inaondoa tuta ama inafanya lile eneo lisipitike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa Mkoa wa Njombe kuhakikisha kwamba anamsimamia mkandarasi ambaye yuko *site* kukwamua magari yote ambayo yamekwama ili wananchi wasipate hiyo adha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili la vipande vilivyobaki kutangazwa, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Njombe na hasa Mbunge wa Lupembe, sasa hivi tunavyoongea jana zabuni ilifunguliwa ishatangazwa kilometa 42 kutoka Kibena hadi Kijiji kinaitwa Kidegembe kilometa 42 ambayo yalikuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tayari Zabuni imefunguliwa. Kwa hiyo, tunategemea kazi itaanza haraka iwezekanavyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara hii ya Morogoro Njombe *border* kupitia Mlimba kipande cha kutoka Ifakara – Chita, Ifakara – Mbingu – Igima tayari mkandarasi yuko *site*. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba anijibu kwa nini mkandarasi hajaanza kazi na yuko *site* huu ni mwaka wa pili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaposema barabara imeanza kujengwa ni kwamba taratibu zile za manunuzi na mkandarasi ameshaenda *site* tunajua kwamba tayari tumeshaanza mchakato wa kuanza kuijenga na ambacho kinafanyika sasa hivi ni kumlipa *advance* huyo mkandarasi. Kwa hiyo, kipande cha kwanza tayari ameshalipwa na tunategemea muda si mrefu kipande cha pili mkandarasi atalipwa. Hivi vipande vyote vinavyokamilisha kilometa 100 vianze kujengwa kwa kasi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tecla, jiandae Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Barabara ya kutoka Kiranjeranje – Nanjilinji – kwenda Ruangwa itajengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii Barabara ya Kiranjeranje kwenda Ruangwa tumeshaifanyia usanifu yote. Hata hivyo, hii barabara pia nataka nimjulishe Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba ina mito mingi mikubwa ambayo ilikuwa ni mtihani mkubwa kupita hapa. Tunachoongea sasa hivi madaraja matatu ambayo yako katika barabara hii Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatafuta fedha ambazo kwanza tutahakikisha tunayajenga hayo mdaraja ya kudumu likiwemo Daraja la Mto Mbwemkuru ambalo lilikuwa ni mtihani mvua ikishanyesha hapapitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukishakamilisha hayo madaraja sasa ndiyo tutaanza kujenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami, lakini kwanza wananchi wawe na uwezo wa kupita kwa mwaka mzima. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkandarasi wa Kichina anayejenga Barabara ya Mbulu – Garbabi ametelekeza mradi huu kwa zaidi ya mwaka sasa na kwa kuwa barabara hiyo imekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wa Mbulu. Je, ni lini Serikali itamrudisha huyu mkandarasi ili akamilishe kazi iliyoko kwenye mkataba wake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tayari Mheshimiwa Mbunge alishafika ofisini na kutoa hiyo changamoto. Tumeshatoa maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa manyara kuhakikisha kwamba mkandarasi anarudi. Hata kama hajaanza, lakini ana wajibu wa kuhakikisha kwamba barabara hiyo inapitika kipindi chote na hasa katika kipindi hiki. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati tunatafuta fedha ya kumlipa, lakini ile kazi ya kuhakikisha watu wanapita aifanye kwa sababu ni wajibu kimkataba. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaishukuru Serikali kwa kukubali kujenga Barabara ya Haydom kwenda Labay na kwa kuwa mkandarasi yuko *site* na hawajamlipa fedha. Je, ni lini watamlipa fedha ili barabara hiyo ianze kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu mengine. Wakandarasi wote ambao wameshakwenda *site* sisi kama Wizara tumeshapeleka hati za madai yao Wizara ya Fedha na wametuhakikishia kwamba muda si mrefu wakandarasi hao watalipwa malipo yao ili waweze kuendelea na kazi ikiwepo na hiyo barabara ya Mheshimiwa Flatei kama alivyouliza. Kwa hiyo, tuna uhakika wakandarasi watalipwa, lakini cha muhimu mkandarasi aendelee kufanyia matengenezo hiyo barabara katika kipindi hiki cha mvua.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kwa Sadala – Kwale – Lemira kilometa15 Serikali iliahidi mwaka wa fedha huu kufanya upembuzi yakinifu. Ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara hii ya Kwa Sadala – Kwale – Lemira kilometa 15? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tuliahidi na tunachofanya sasa hivi kwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Hai, ni kwamba tunavyoongea sasa hivi kazi tunayofanya mwaka huu barabara ilikuwa haijasanifiwa, ni kuifanyia usanifu barabara yote ikiwa ni pamoja na kulijenga lile Daraja la Kikafu Juu ambalo tayari mkandarasi yuko *site* kulijenga hilo Daraja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo, jiandae Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami na hasa ukizingatia kwamba Arusha tutanufaika na barabara ya njia nne kutoka Kona ya Mbauda mpaka Kwa Mrombo ambapo tunakwenda kujenga stendi ya kisasa lakini pia na Kona ya Kiserian hadi *by pass* kule kwenda *Fun Retreat*. Ujenzi wake utaanza lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge wa Arusha Mjini ilikuwa ni sehemu ya zile barabara za *EPC+F*. Baada ya kufanya mabadiliko ya ujenzi barabara hii itajengwa kilometa70 kuanzia Arusha na barabara zote hizo alizozitaja ni sehemu ya ujenzi wa hiyo Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoongea tarehe 11 Februari tulisaini mikataba kwa sababu wakandarasi wa awali ndiyo haohao ambao watajenga. Kwa hiyo, tunategemea na hasa tukijua barabara hizo pia zitahudumia sana mashindano ya *AFCON*. Tuko makini tutakapokuwa tumekamilisha taratibu zote barabara hiyo itaanza kujengwa kipindi hiki cha mwaka wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Gulamani kabla hujauliza swali kuna tukio la Kitaifa jana hebu kidogo lipongeze halafu uendelee. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niwapongeze Simba kwa kufuata nyayo za Yanga; hongereni bado hamjafikia fainali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa niweze kumuuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa sasa ni miezi mtano toka tupate mkandarasi wa kujenga Barabara ya Choma – Ziba – Mkinga mpaka Puge. Je, ni lini tutasaini mkataba kwa ajili ya kuanza kwa kazi hiyo ya ujenzi? Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaposaini mikataba tunakuwa tumefanya mawasiliano ya karibu na tumeshawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha kwa barabara zote ambazo ziko tayari kuzisaini basi tunavyosaini tuwe na uhakika kwamba zinaenda kuanza kujengwa ikiwa ni pamoja na hii barabara ya Mheshimiwa Gulamali ya Choma kwenda Ziba.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Felix.

Na. 40

**Viwanda vya Kuchakata Zao la Migomba**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanda vya kuchakata zao la migomba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Zao la Migomba ama ndizi ni miongoni mwa mazao makubwa katika Wilaya ya Buhigwe na maeneo mengine nchini. Kutokana na tafiti zilizofanywa duniani zao la migomba linaweza kutumika kutengeneza bidhaa kama vile vikapu, mikeka, kofia, chakula cha mifugo, mbolea, nguo, karatasi, nyuzi, dawa za asili na malighafi za kujengea lakini pia matunda yake hutumika kama chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo *(SIDO)* na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini *(CAMARTEC)* ina teknolojia ya kuchakata migomba kwa ajili ya chakula cha mifugo na viwanda

vya kutengeneza mvinyo, unga wa lishe, keki na *crispy* zinazotokana na ndizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa uongezaji thamani zao la migomba pamoja na ndizi, Serikali kupitia *SIDO* imepanga kuanzisha kongani ya zao la migomba na ndizi katika halmashauri, ikiwemo Halmashauri ya Buhigwe ili kuongeza mnyororo wa thamani kwa zao hilo. Aidha, zao hili ni miongoni mwa mazao yatakayoongeza thamani nchini kupitia mpango maalum wa kuendeleza viwanda wa miaka mitano unaotarajiwa kuanza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2025/2026 hadi 2029/20230. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imesema itaanzisha kongani ifakapo Julai, 2025, je, programu hii imewekwa kwenye bajeti au Serikali itatumia chanzo gani mahususi kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mpaka sasa kuna hatua gani zilizochukuliwa kuandaa wakulima wa migomba kwa ajili ya kongani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Felix Kavejuru kwa kuendelea kufuatilia kuhusiana na uongezaji wathamani mazao ya kilimo katika Mkoa wa Kigoma na hasa Jimbo la Buhigwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kongani tunazozianzisha hapa nchini maeneo yote zinawekwa kwenye bajeti na hili liko kwenye mpango wa bajeti ambayo itasomwa hapa kwa ajili ya mwakani 2025/2026 ambayo Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Selemani Jafo atawasilisha katika Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo,

nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, Serikali tumejipanga na ndiyo maana tumesema tutaanza kutekeleza kwa mwaka huo 2025/2026 kwenda 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hatua ambazo tumechukua kuwaanza wakulima na wadau wote katika hatua za awali. Kwanza kama nilivyosema ndizi au migomba ni zao ambazo linalimwa Tanzania nzima na maeneo mengine. Kupitia Wizara ya Kilimo wamewezeshwa pembejeo na utaalam kupitia Maafisa Ugani ili kuhakikisha wanazalisha kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tayari utaratibu huu tunao kwenye mazao mengine kwa mfano katika Mkoa wa Kigoma kwenye zao la chikichi tayari kuna kongani hizo na zimeonesha kufanya vizuri sana pale Kigoma na yeye ni shahidi. Kwa hiyo, tutatumia *module* hiyo hiyo kuhakikisha na kwenye zao la ndizi na migomba tunafanya hivyo. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Mgeta ina wakulima wa mbogamboga na wakulima wa matunda, lakini wamekuwa wakipata hasara kila mwaka kwa sababu ya kukosa soko la uhakika. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kujenga kiwanda kidogo cha kusindika matunda katika Tarafa ya Mgeta? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri, lakini hasa kwenye sekta hii ya matunda na mbogamboga ambayo maeneo mengi hapa Tanzania tunazalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha tunaongeza thamani ya mazao yote ya kilimo ikiwemo haya ya matunda na mbogamboga. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Tarafa ya Mgeta nao watanufaika na mpango

huu na kama nilivyosema tunaanza kongani katika mikoa yote na halmashauri zote ili kuhakikisha kila kwenye mazao haya tunapunguza upotevu baada ya mavuno *(post-harvest loses)*. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge hata kule Mgeta nako tutafika na tutawasiliana ili tuone namna gani ya kuvutia wawekezaji waje katika jimbo lako. Ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Viongozi wa Wanafunzi kutoka Chuo cha Teknolojia cha Jijini Dar es Salaam *(DIT)*, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge: Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Kikundi cha Zabron *Singers* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wengine wawili wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, kutoka Kampuni ya *Power of Africa*, wakiongozwa na Ndugu Mussa Ally Mbwego, Mkurugenzi wa *Power of Africa* (ameandaa Filamu ya MUFASA: The King Lion), karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni Wachungaji kutoka Mikoa ya Arusha na Tabora. *(Makofi)*

Wageni 34 wa Mheshimiwa Samweli Hhayuma ambao ni Wanakwaya kutoka Hanang Mkoani Manyara. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Madaktari wa Vituo vya Afya Mkoani Kigoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Suma Fyandomo, Ndugu Christina Malasusa, Dada yake kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambao ni wapigakura wake kutoka Sikonge Mkoani Tabora. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe ambao ni Katibu wa Mbunge na Msaidizi wa Ofisi ya Mbunge, kutoka Ndanda Mkoani Mtwara. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Viongozi watatu wa Shirika lisilo la Kiserikali *(Acceleration of Life Skills Foundation)* kutoka Jijini Dar es Salaam.

Pia, tunao wanafunzi 90 na Walimu 10 wa shule ya Sekondari ya Wasichana Mtakatifu Monica ya Jijini Arusha. Shule hii ni miongoni mwa shule zinazofanya vizuri sana kielimu hapa nchini Tanzania, ikiwa ni pamoja na malezi mazuri ya watoto wetu wa kike. Hongereni sana karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kuna Mbunge hapa ana hoja ya dharura. Hoja yake ni kwamba anaomba tuahirishe Bunge kwa mjadala uliopo mezani tujadili penati za Simba. *(Makofi)*

Sasa kabla sijafanya maamuzi yoyote ni jambo la msingi na jambo la kitaifa. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu karibu, najua ulitumwa na Mheshimiwa Rais kwenye majukumu ya kiserikali. Hongera kwa kufanya kazi nzuri na hongera kwa kurudi. Sasa hili nitalitolea maamuzi baadaye. *(Kicheko/ Makofi)*

Namwita Mwenyekiti aje sasa aendelee na majukumu yaliyobakia.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge ni wakati sasa wa kupokea michango yenu kuhusiana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi. Nina majina hapa na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha Sekta ya Elimu, bado mfumo wetu wa elimu hautengenezi wahitimu wenye weledi na umahiri mkubwa kwa sababu hauzingatii shauku ya kujifunza kwa wanafunzi na vilevile hauzingatii vipaji vya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Howard Gardner wa Chuo Kikuu cha Harvard ameandika kitabu kinaitwa *Frames of Mind*. Katika kitabu chake anasema wanadamu wana vipaji vya aina tisa, mimi nitavitaja sita ambavyo ni:-

(i) Uwezo wa kuzungumza na kuandika;

(ii) Kutunza mazingira;

(iii) Kucheza michezo ya aina mbalimbali;

(iv) Sanaa ya ubunifu;

(v) Ushirikiano na mahusiano katika jamii; na

(vi) Kazi za mikono na ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya mifumo yetu ya elimu na malezi inadumaza vipaji, uwezo na karama za wanafunzi kwa sababu inawalazimisha wasome masomo yasiyoendana na shauku zao pamoja na vipaji. Uzoefu unaonesha watu waliofanya mambo makubwa duniani wamefanya mambo wanayoyapenda moyoni na yanayozingatia vipawa vya asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni nini? Tukiwalazimisha kwa mfano, kama mzee ni daktari anataka na mwanaye awe daktari, kama ni mhasibu anataka mwanaye awe mhasibu; hatari yake ni nini? Inaathiri ari ya kujifunza na ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali imezindua sera mpya ya elimu. Hata hivyo kwa maoni yangu, utekelezaji wake unahitaji kiwango kikubwa sana cha fedha ili kuwaandaa walimu wenye ujuzi, ujenzi wa maabara za kisasa na karakana za ufundi. Ili tuweze kukabiliana na tatizo hilo napendekeza tufanye mambo mawili ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza; Serikali itumie ipasavyo Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kuandaa walimu kwa mafunzo hasa katika mbinu za kisasa za kufundishia na hapa ninasisitiza matumizi makubwa ya teknolojia ya kisasa na ubunifu katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wanaweza kutumia *projector,* wanaweza kutumia kompyuta na wanaweza kutumia mitandao kuwaonesha watoto majaribio mbalimbali ya kisayansi na kiufundi bila ya gharama kubwa. Unaweza kuwaonesha watoto jinsi damu inavyotembea kwenye mwili, unaweza kuonesha jinsi mimea inavyotengeneza chakula kwa kutumia nishati ya jua na unaweza kuonesha jinsi miti inavyosaidia kutengeneza mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninaiomba Serikali ihimize matumizi ya mazingira ya shule na sayansi ya nyumbani

katika ufundishaji. Kwa mfano, tunaweza kufundisha masomo ya sayansi kwa kuonesha watoto jinsi nishati ya jua inavyotumika katika shughuli mbalimbali za binadamu kama vile usafi wa mwili na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kujenga Taifa linalojitegemea elimu yetu inapaswa kujengwa kwa misingi ya kujitegemea kama alivyosema baba wa Taifa hili. Misingi ambayo inazingatia si mafunzo ya ufundi peke yake bali mafunzo ya sayansi na teknolojia, ubunifu, ugunduzi, na ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalisema hili suala la elimu la kujitegemea kwa sababu ninasikitika sana kwamba tuna vitivo vya kila aina vya uhandisi lakini bado haviwezi kutoa majibu ya masuala ya msingi ya matatizo ya Taifa letu. Nitatoa mifano mitatu. Mfano wa kwanza, tuna mwanga wa jua kila mahali wahandisi hawatusaidii kubuni teknolojia inayoweza kuvuna mwanga ili nishati ya mwanga itumike katika kilimo cha umwagiliaji maji na kuendesha pampu za kusukumia maji na matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili, tunaagiza mitungi ya gesi kutoka nje, tunaagiza majiko sanifu wakati tuna wahandisi wa kila aina. Mfano wa tatu, tuna wahandisi wengi lakini bado madaraja na mejengo mbalimbali katika nchi yetu yanajengwa na watu kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natafakari nikasema, kwa nini katika anga kuna hewa ya *Hydrogen* ya kutosha lakini wahandisi hawaivuni tukaweza kuitumia kama nishati? Ninalisema hili kwa sababu hivi karibuni kuna kijana mmoja Zimbabwe amebuni teknolojia ya kuvuna mawimbi ya redio yanayotumika kuendesha gari badala ya mafuta. Kwa nini lisiwezekane hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa maoni yangu kuna haja ya kuangalia muundo wa vyuo vikuu vyetu vya Tanzania ili visisitize mafunzo ya vitendo zaidi kuliko nadharia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza tuwe na vyuo vya aina tatu. Kwanza tuwe na vyuo vikuu vya utafiti *(research universities),* pili tuwe na vyuo vikuu vya mafunzo ya kazi mbalimbali *(professional studies),* na mwisho tuwe na vyuo vikuu vya sayansi na teknolojia *(universities of applied sciences and technology)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha. Nimwite sasa Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa pili katika hotuba hii ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kipekee niungane na Watanzania wenzangu kuipongeza Klabu ya Simba, benchi la ufundi, uongozi na mashabiki wote waliokuwa nyuma ya timu na hatimaye jana timu ya Simba imetuheshimisha kwa kiwango kikubwa maana ilikuwa ni timu pekee inayotoka ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati iliyokuwa imebaki kwenye mashindano haya, kwa hiyo imevuka imetupa heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai na kuiomba Serikali. Jana baada ya mechi nadhani ndani ya saa moja tuliona tangazo linazunguka wakisema kwamba Uwanja wa Benjamini Mkapa umefungiwa na hautatumika katika mechi tena. Sasa kama Ulega ameishi njiani kule Mikoa ya Kusini ikafunguka, tunachoomba Serikali ifanye jitihada zinazowezekana ili uwanja ule urejee kwenye hali yake na mechi za tarehe 20 zichezwe pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuwa *champion* mkubwa na motisha hiyo wanayoipata wachezaji wakafanya vizuri katika klabu zetu ni kwa sababu yuko nyuma yao. Itakuwa ni jambo la ajabu na aibu nusu fainali hii ikachezwe

kwenye nchi nyingine wakati nchi nyingine zimekuwa zinakimbia kucheza mechi zao. Kwa hiyo, tuombe hilo Serikali ilifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba nirejee katika mchango wangu. Mtunga Zaburi anasema, "Wako wapi wazee na watu wenye busara waliyoyaona matendo makuu haya ya bwana na hatimaye wawakumbushe vijana na watu wengine ambao hawakuyaona wayafanyie kazi na hatimaye wapate kuyajua." Kwa nini ninayasema haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 Mheshimiwa Rais Samia alipoingia madarakani mpaka sasa ametimiza miaka minne. Yapo mambo ambayo yamefanyika mwaka 2021, wazee na watu wenye hekima wasipowakumbusha ambao hawakuyaona wakati ule au waliosahau tutakuwa hatumtendei haki Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu yamesemwa mengi, yamefanyika mengi na tunaenda kwenye uchaguzi; haikosi kuna watu wamesahau. Kwa hiyo, ninataka nichukue wito huu nikumbushe baadhi ya mambo makubwa ambayo yamefanyika katika wakati huu. Hata hivyo, licha ya haya mambo kufanyika na yametajwa katika Hotuba ya Waziri Mkuu bado mambo mengine makubwa yamefanyika kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na miradi mikubwa ya kitaifa kama Bwawa la Mwalimu Nyerere, reli ya kisasa ya *SGR*, tukawa na Daraja la Kigongo Busisi, tumekuwa na Daraja la *Tanzanite*, tumekuwa na Daraja la Mto Wami na *flyover* nyingi zimejengwa. Pia tuna *key issues* ambazo zimefanyika katika kipindi hichi cha miaka minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, 2022 tulikuwa na sensa ya watu na makazi. Sensa haijitokezi kila wakati lakini pesa nyingi ambazo zimeenda huko, ambazo zingeweza kufanya miradi mingine, lakini zimetumika kwenye hili zoezi. 2024 tumekuwa na uchaguzi, vyote hivi vinafanyika kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023/2024 tulipata janga la *El-Nino* na hatimaye nchi wakaweza ku-*stabilize* ikarudi kwenye mahali pake. Sasa mambo yote haya makubwa ambayo yamefanyika huenda watu wameyasahau na leo tunapoelekea kwenye uchaguzi mwingine anaweza akaangalia kiti kimoja akasema hiki, hiki na hiki. Ni lazima tuelewe nchi imekuwa *engaged* kwenye vitu vikubwa. Pia, tuko tunajenga viwanja kwa ajili ya *AFCON* na mambo mengine makubwa yanayoendelea katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo yote haya, Wabunge katika kipindi cha miaka minne tumesimama ndani ya Bunge tukifanya uwakilishi wetu kwa wananchi waliotutuma. Yaliyo mengi yamefanyika kwa sababu Serikali pamoja na kuwa na miradi mikubwa haikutuacha Wabunge, ilitusikiliza. Sasa kwa sababu naongea kwa niaba ya wananchi wa Biharamulo ninataka nitaje baadhi ya vitu ambavyo ninaamini hata Wabunge wengine kwenye maeneo yao vimetajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwakumbushe ile habari ya mtunga Zaburi akihusia watu wazee na wenye busara waliyoyaona yale yanafanyika wakumbushwe. Haikosi kuna mtu mwingine aliona barabara haikuwepo, lakini sasa hivi akipita hajui kama kulikuwa na shida ya barabara. Mara nyingi nimekuwa nawakumbusha watu hata ule Uwanja wa Ndege wa Kimataifa *Terminal Three* ulipojengwa pale zamani kilikuwa ni kijiji cha kipawa kile. Watu waliondoka pale, mtu mpya akiingia pale anaona uwanja ha-*imagine* kwamba kuna watu waliwahi kuishi pale miaka ya 2000 mpaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mfano kwangu tu miradi ya maji ambayo imefanyika kwangu kwenye habari ya vijijini. Katika muda wa miaka hii minne tumepokea shilingi bilioni 8.8 katika miradi ambayo imeshatekelezeka na nina miradi mingine ya takribani shilingi bilioni 5.19 inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biharamulo Mamlaka ya Maji nina 3.3 *billion*. Ukipiga tu hesabu hapo ni karibu shilingi bilioni 17 ambazo Biharamulo peke yake tumepokea kwenye miradi ya

maji. Tumeongeza idadi ya *distribution* ya watu ambao walikuwa hawapati maji na hatimaye wamepata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea habari ya shule. Mwaka 2020 shule za msingi nilikuwa nazo 98, lakini leo nina shule za msingi 117, ongezeko la shule mpya 19 za msingi; sio kazi ndogo. Nakumbuka nilipoingia nilikuwa nina Shule moja ya Msingi Nemba - Biharamulo ilikuwa na wanafunzi 5,259 shule moja ina madarasa tisa. Leo ninapoongea tumetoa shule nne mpya pale. Kwa hiyo, yote hayo ni mambo makubwa ambayo yamefanywa na Serikali na ni lazima tujivunie nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika habari ya afya. Nilikuwa na zahanati 18 sasa hivi nina zahanati 26, ongezeko la zahanati nane mpya katika miaka hii minne. Vituo vya afya nilikuwa navyo sita sasa hivi ninavyo saba. Sikuwa na Hospitali ya Wilaya lakini tayari ninayo moja. Unaweza ukaona *commitment* ya Serikali, pamoja na kufanya mambo makubwa, lakini bado kwenye majimbo tumeendelea kuhudumiwa na miradi ile ya kiwilaya na kimajimbo imeendelea kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee habari ya barabara katika jimbo langu la Biharamulo, wakati Mheshimiwa Rais anaingia pesa niliyokuwa napokea Biharamulo ilikuwa ni milioni 670 tu kwa ajili ya barabara, leo hii naposimama hapa na *2.467 billion* ninayoipokea kutoka milioni 670.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuona *commitment* barabara za lami tulizokuwa nazo Biharamulo ilikuwa ni kilometa 4.59, leo nina kilometa 10.18 ongezeko la zaidi ya kilometa tano kwa miaka hii minne. Barabara za changarawe nilikuwa na kilometa 111, sasa hivi nina kilometa 275. Tumepunguza barabara za udongo kutoka kilometa 391 ni kilometa 222 zilizobaki na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *box culvert* hatukuwa nayo hata moja, sasa hivi nina *box culvert* tano zimejengwa Biharamulo. Pia *line culvert* nilikuwa nazo 415 sasa hivi nina 618 na tumefungua barabara mpya kilometa 191 zilizojengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu habari ya umeme 2020 ni vijiji 46 pekee ndiyo vilikuwa na umeme lakini sasa hivi nina vijiji 74 ndiyo vyenye umeme na vitongoji 15, sasa hivi muda siyo mrefu mkandarasi anaingia *site*. Kwa hiyo kwangu vijiji vyote vimefikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeamua niyaseme haya? Ninayasema haya kwa sababu ni lazima tuwapongeze mawaziri wametushika mkono. Wabunge tumeongea humu lakini Mawaziri waliyasikia kutokea ndani ya Bunge wakapeleka hatimaye wakatuletea hizi fedha. Kwa hiyo, kama hatuwezi kuyaona hata haya tukashukuru hatutakuwa tunawatendea haki na kuitendea haki Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa mwenye hii hotuba ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunapoyaona haya yanafanyika Waziri Mkuu amekuwa anafikika, Waziri Mkuu amekuwa ni mtu mwenye ushirikiano kwa Wabunge kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Wabunge tume-*address* kwa Serikali na kuongea nayo kupitia ndani ya Bunge hili, Kiongozi Mkuu wa shughuli hizi akiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo ni lazima tumpongeze na kuona kwamba *commitment* yake katika kusikiliza hoja za Wabunge imekuwa kubwa hatimaye mambo haya waliyoyasikia katika Bunge wakaenda kuyajadili katika Baraza na kuyapeleka kwa Mheshimiwa Rais hatimaye pesa zikamwagika, zikaja, zikafanya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipee pia nimpongeze Waziri Mkuu, kwa sababu siyo rahisi nadhani ni Waziri Mkuu wa kwanza ambaye ametumika katika Serikali mbili na Marais wawili *full time,* akitumika katika Serikali ya Awamu ya Tano kama Waziri Mkuu na ametumika katika Serikali ya Awamu ya Sita kama Waziri Mkuu mpaka sisi tunamalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii, uaminifu wake na *commitment* yake katika kuwasaidia Marais hawa wawili ni kubwa. Kwa hivyo, kipekee kwa niaba ya wananchi wa Biharamulo nichukue nafasi hii kumpongeza na kumuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumhifadhi na kumlinda ili hatimaye

*commitment* hii ambayo umeionyesha Mungu wa Mbinguni akamlipe mara dufu hatimaye tumuone tena wananchi wa Ruangwa wakimuamini na kumpa nafasi nyingine tena ya kuja kushiriki hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nikushukuru kwa nafasi na niseme kwamba naunga mkono hoja, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** *Engineer* John Chiwelesa ahsante sana kwa mchango wako. Nimuite sasa Mheshimiwa Simon Lusengekile atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hotuba hii ya Bajeti. Ninaungana na mchangiaji aliyemaliza Mheshimiwa Chiwelesa kuwapongeza sana timu ya Simba kwa ushindi wa jana chini ya mgeni rasmi, Mheshimiwa Jumaa Aweso, hakika Jumaa Aweso ameona namna gani timu ya Simba inafanyakazi nzuri na kama methali yake ambavyo amekuwa akisema 'anayejua hali ya mgonjwa ni yule aliyelala nae kwa sababu anajua mihemo yake' kwa hiyo Mheshimiwa Aweso amesikia mihemo ya Simba na tunaiombea Simba kwa ajili ya nusu fainali ambayo iko mbele yao.*(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anazozifanya na kwa namna anavyopambana kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata maendeleo, katika kazi nzima ya kutafuta fedha katika majimbo yetu na katika nchi yetu kama ambavyo Mheshimiwa Ezra, amesema hapa, miradi mikubwa ambayo sasa imekamilika na mingine imeanza kazi ikiwemo *SGR,* Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo tunaenda kupata *megawatts* 2,115 itakayosababisha kuwa na *megawatts* 4,031 katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maendeleo makubwa na ni pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. Angalia daraja la Busisi na lenyewe ni kama limekamilika muda siyo mrefu litaanza kutumika. Hii miradi ilikuwa ni mikubwa na mingine ilikuwa inatumia fedha zetu za ndani, ninampongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii na mimi nataka niwaambie watanzania Mama Samia tunae na tunatamba nae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais lakini pia nimpongeze sana mwenye hotuba, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi nikupongeze sana kwa kazi unayomsaidia Mheshimiwa Rais, Wabunge hatuna mashaka na wewe tunajua utendaji wako wa kazi mkubwa na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kukuamini wewe na kuendelea kuchapa kazi kwa ajili ya watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona anavyotembelea Halmashauri zetu, pale unapokuja wewe tunaona mabadiliko makubwa sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulikuja pale kwangu sikumbuki nafikiri 2022 au 2023, tukaanza kujisifia heeeee! Kumbe unatusubiri tu, dakika mbili mbele Mheshimiwa Waziri Mkuu unauliza kwa nini milioni kadhaa hazikupelekwa kwenye akaunti? Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli umeendelea kuzisaidia sana Halmashauri zetu, umeendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa majukumu ambayo umeendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba tu wananchi wa Ruangwa kwamba waendelee kukuamini, ni mchapakazi na mimi niwaambie bado tuna wewe na tunatamba na wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pamoja na hayo Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na pongezi hizo tunatambua mambo makubwa uliyoyaeleza kwenye hotuba yako, tunatambua sekta mbalimbali ulizoeleza kwenye hotuba yako, tunaona maendeleo makubwa sana kwenye nchini yetu, tunaona namna gani nchi yetu imeendelea kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kadri tunavyoendelea tutakuwa pazuri zaidi, tukiona sasa hata uchumi wetu wa nchi

unazidi kuimarika, ninamkupongeze wewe kwa namna unavyoendelea kumshauri Rais, niwapongeze Mawaziri kwa namna mnavyoendelea kumshauri Waziri Mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake hakika nchi yetu sasa iko vizuri na maendeleo ni kemkem, 'ma-ti' na 'ma-bi' yameendelea kuwepo kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Busega kama Busega tumenufaika na fedha nyingi. Tukisema tuanze kutaja hapa Mheshimiwa nitahitaji nusu saa katika mchango wangu ili niyataje yale ambayo yamefanyika kwenye Jimbo letu la Busega. Tumeona tulikuwa na Hospitali ya Wilaya na sasa tulipokea zaidi ya bilioni nne na Hospitali ya Wilaya sasa inafanyakazi, haya ni mapinduzi makubwa na wanabusega wanasema Mheshimiwa Rais wanae na wanatamba nae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo pia barabara zimefunguka kwa kiwango kikubwa sana, bajeti yetu ya 2020 ilikuwa milioni 714 na sasa tunavyozungumza kila mwaka kuanzia 2021 mpaka sasa tumekuwa tukipata bilioni mbili na milioni mia saba hii ni hatua kubwa na Busega sasa imefunguka na haya yote ni mapenzi makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan, tunae na tunatamba nae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tumepata shule za msingi mpya za kisasa shule mbili na shule za sekondari mpya mbili. Haya ni mafanikio makubwa kwa wananchi wa Busega, nina imani kwamba kazi kubwa iliyofanywa na Serikali wananchi wa Busega watazidi kuiunga Serikali yao ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tumepata Vituo vya Afya vya kutosha ambavyo Jimbo letu la Busega wameendelea kunufaika, tunaishukuru Serikali imeendelea kutuletea wahudumu wa afya wakiwemo madaktari lakini pia tuendelee kuiomba, kuendelea kuimarisha eneo la watumishi ili sasa vituo vya afya ambavyo tayari vimejengwa na Serikali yetu

pendwa sana ya Awamu ya Sita viendelee kutoa huduma iliyo na tija kwa wananchi wa Jimbo la Busega na wananchi wa Tanzania nzima. Hii ni kufatana na upatikanaji wa wahudumu katika vituo vyetu ambavyo vimejengwa, wakiwemo madaktari, wakiwemo manesi na watu wengine ambao wanahitajika kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Kata moja ya kimkakati, Kata yetu ya Kabita pale Nyamikoma. Tulishaleta pendekezo letu kama wananchi wa Busega kwa ajili ya kituo cha afya, ni imani yangu sasa bajeti itakapokuja ya TAMISEMI, eneo hili sasa ni eneo muhimu ili Wananchi wa Kata ya Kabata wapatao zaidi ya 36,000 wapate huduma ya kituo cha afya ili wao sasa na kata zingine za jirani kama Kalemela waweze kufikiwa na huduma ya karibu ya kituo cha afya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulipata mafuriko pale Lamadi na mafuriko haya yalisababishwa na magugu maji ambayo yamevamia Ziwa pamoja na Mto Lamadi ambao ulisababisha Ziwa Victoria kujaa kwa maeneo yale na maji sasa kurudi kwa wananchi ambao wananchi wetu walipata hadha kidogo. Sasa tulishaandika andiko letu kwa ajili ya milioni 118 ya kutoa magugu maji kwenye mto pale, Mto Lamadi. Tunaomba sasa Wizara husika itakapokuja ije ione namna gani inawasadia wanabusega kwa sababu maafa haya hayabishi hodi siku nyingine tuondokane na hadha hii tupate hizo fedha kwa ajili ya kujenga mitaro lakini kwa ajili pia kutoa magugu maji kwenye eneo hili la Lamadi na wananchi wa Lamadi waweze kuishi salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja hayo Mheshimiwa Waziri Mkuu pale Busega tumeanza ujenzi wa *VETA*, tunaishukuru sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa ajili ya Ujenzi wa *VETA* lakini kwa kweli sasa una muda mrefu umesimama takribani miezi sita. Tunaomba sasa wizara yetu, Wizara ya Elimu iangalie namna gani *VETA* hii inakamilika kwa wakati ili wananchi waweze kuitumia na *value for money* iendelee kuonekana kwa wananchi wetu kwa sababu *VETA* hizi zilijengwa kwa ajili ya vijana na zilijengwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yetu sasa zitakapokamilika zitaleta tija kwa vijana ambao watakuwa wamesoma katika maeneo yale na katika wigo mzima wa kupata ajira, wananchi wetu watapata ajira na itaweza kuwasaidia kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana kwa kuendelea kutupa nafasi hii ili tuweze kuchangia na kuona mustakabali mzima wa bajeti ilivyo salama ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi sasa niungane na Waziri Mkuu kuunga mkono hoja hii na tumpitishie fedha alizoomba ili waweze kutekeleza majukumu yao, niwapongeze sana Mawaziri mnaomsaidia Mheshimiwa Lukuvi, Ridhiwani na Manaibu Waziri mnaosaidia hii Wizara ya Waziri Mkuu, tunaimani kubwa pamoja nanyi na mimi niungane nanyi kupitisha bajeti yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nirudie tena Mheshimiwa Rais tunae na tunatamba nae wananchi wa Ruangwa Mheshimiwa Waziri Mkuu tunae na tunatamba nae na tunampongeza kwa kazi, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda atafuatiwa na Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hii bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani zaidi ya miaka tisa sasa nimekuwa nikilalamika sana kwa zao la chai, zao la parachichi na mara nyingi sana hata Waziri Mkuu alipotembelea katika Mkoa wetu wa Mbeya mimi nilikuwa sikosi na nikilalamika na nikitoa malalamiko mbalimbali juu ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema namshukuru Mungu baada ya malalamiko haya ya muda mrefu mwezi huu Mheshimiwa Bashe kama Waziri mwenye dhamana ya Kilimo

ameweza kutoa nafasi na kutoa elimu na kutoa tamko kwa ajili ya kuwasiliza wakulima hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa mara ya kwanza ninaipongeza na ninampongeza waziri kwa maana yeye anafanya kwa niaba ya Waziri Mkuu kwamba ameweza kujibu kilio cha wakulima wa parachichi. Mwaka huu ulikuwa mwaka mbaya sana kwenye mazao, parachichi ziliuzwa vibaya lakini Mheshimiwa Waziri ameamua kuja na suruhisho na ninapenda niwaambie Wabunge waelewe ni nini alisema kwenye siku ya wadau wa parachichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe pia kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo ulikuwepo. Baada ya kuona kilio kikubwa sana na uharibifu wa zao hili likiendelea Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo mahsusi na ninaamini Waziri Mkuu atakapopitishiwa bajeti hii ataenda kutekeleza yale ambayo waziri wa dhamana ameyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ameweka kitu kinaitwa *(COPRA)* amewekea nguvu kwa watu wa *(COPRA)* waweze kusimamia tasnia hii ya parachichi kwa kumuweka dada Hellen kuwa ndiyo msimamizi pale na tunaamini tunamwamini dada huyu wa sababu wanawake wakiwa na jambo lao huwa wanafanya vizuri kwa hiyo tunaamini Ndugu Hellen atasimamia *(COPRA)* na atafanya maagizo ambayo Mheshimiwa Waziri amempa na sisi tutamsaidia kuhakikisha anatimiza wajibu huo kwa wakulima wa parachichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ameona kuna umuhimu Mheshimiwa Waziri Bashe kununua magari zaidi ya 18 ya kuchimba visima kupeleka kwenye mashamba ya parachichi hii, ni kwa mikoa 6 inayolima parachichi. Hili ni jambo kubwa sana na la muhimu kwa wakulima kwa sababu tumesema parachichi ni zao la kijani ni dhahabu ya kijani inaleta uchumi na inaongeza Pato la Taifa, basi wazo hili la Mheshimiwa Bashe kutoa fedha na anasema ifikapo Aprili 30 magari haya yatakuwa tayari mimi nipongeze kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna fahamu kabisa kwamba mbolea na viatilifu kwa ajili ya parachichi sasa hivi Mheshimiwa amesema vitatoka kama ruzuku na fedha yake ipo tunaamini inakwenda kutekelezeka na wakulima sasa wataenda kufanya. Wajibu wa mkulima sasa uliobaki ni kusimamia mazao hayo kwa uangalifu kwa sababu suala siyo kupanda tu mche na kuacha ni lazima usimamiwe na kufika kwenye viwango vya kimataifa ili tunapodai soko basi soko letu lipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa Mheshimiwa Bashe amezungumzia suala la kuongeza Maafisa Ugani. Ni ukweli usiyopingika kwamba Maafisa Ugani hawatoshi lakini mwisho wa siku kwa sababu zao hili limekuwa la kimkakati basi amefikiria kuna namna ya kuongeza na kuhakikisha vijana hawa wanakuwepo kuwasaidia wakulima wetu, mimi kwa hilo ninapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo suala la soko tumekuwa na soko la Ulaya kwa muda mrefu lakini tumepata taarifa kutoka wizarani kwamba sasa India na China wanakwenda kununua parachichi za wakulima. Kwa hiyo, suala la kuwa na mazao yanaozea mashambani pale kwetu sisi kama wakulima na tunaowasimamia wakulima imetupa furaha ya kujua msimu unaokuja hatutatupa maparachichi yetu na kuuza kwenye viroba, sasa basi soko liko tayari na ndugu zetu watasimamia ambao wamepewa dhamana kuhakikisha mwaka ujao basi hatutakuwa na kilio tena cha kuozesha parachichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza pia Wizara, Mheshimiwa Waziri Mkuu nimesoma katika bajeti yako umeelezea kwamba kuna magari zaidi ya 40 yananunuliwa, pikipiki 555. Basi tuombe, mimi ninaamini nchi nzima inaenda kupata keki hii lakini mwisho wa siku tusisahau baadhi ya Majimbo ambayo kwa kweli tumepata, lakini tunafikiri yaongezewe kwa sababu tunafahamu Mkoa wa Mbeya ni katika zile *big five* ambayo inalisha Taifa hili, basi katika mgawanyo tuhakikishe watu wa Mbeya hususan Jimbo la Rungwe wanapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmesema mnajenga nyumba, tujengewe basi hata sisi kajumba kamoja msitusahau kwa Maafisa Ugani. Tunafahamu kabisa zao la parachichi lilianzia Rungwe japokuwa ndugu zetu wa Njombe wamefanya kwa uzuri zaidi basi msitusahau sisi mkahakikisha katika mgawanyo huu ikiwemo visima tunapata katika Jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu akisimamia mazao kwenye korosho amefanya vizuri, kwenye ufuta amefanya vizuri, kwenye chai nimelalamika wakati ule mwaka 2016 chai ya Rungwe ilikuwa shilingi 132 kwa kilo, leo imefika kwenye mia tatu na basi Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba bei ya chai uhalali wake unafahamu angalau iwe 700 kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu mkulima anatumia gharama kubwa sana na dola imepanda, kwa hiyo ni lazima tuweke bei iwe juu ili wakulima wetu wafanikiwe. Ninafahamu mmeanzisha soko la chai, hiyo ni juhudi kubwa ambayo mmefanya lakini bado tunahitaji jitihada za zaidi kwa wale wawekezaji ambao wamewekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu tuweze kuhakikisha wanawasaidia watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunae mwekezaji ambaye ameacha kuvuna chai "Mo". Tunatambua kabisa kwamba wawekezaji wanahitaji kupewa mazingira mazuri, lakini wawekezaji hawa hawawezi kuacha kununua chai bila kuwa na taarifa kwa wakulima. Tunafahamu zaidi ya wafanyakazi 300 hawana ajira sasa, nakumbuka tarehe 30 mwezi wa tano mwaka jana Mheshimiwa Bashe alimwambia mwekezaji tunaomba uvute muda ili tuweze kujipanga kama wananchi, kama Taifa tuone tunawasaidiaje watu hawa, lakini mwekezaji alifunga pamoja na kwamba anaweza akawa na haki, tunaomba Sheria za Wawekezaji ziangaliwe upya tuwe tuna *win win situations,* mwekezaji hawezi kuacha ghafla, chai imekuwa mashamba makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipita kiongozi wa CCM katika Wilaya yetu wananchi walilalamika, leo hii mashamba ya chai

yametupwa hayana nafasi, basi yale mashamba kama ni hivyo mtupatie tuwagawie vijana waweze kulima, vijana waweze kujenga, maana maeneo yale sasa yamekuwa mapori hayasaidii lolote. Pamoja na hayo hawa wananchi ambao wameachishwa kazi, wapate haki yao ikiwa ni pamoja na *NSSF* ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uaichukue hili na kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Tunafahamu kabisa kwamba, mazao mengine ya ndizi ni ya msingi kabisa. Kuna nchi kama Jamaica wananunua silaha kwa ndizi. Sisi tunaamini ndizi ni zao zuri, kama likisimamiwa vizuri. Viwanda vidogovidogo vijengwe kwenye maeneo yetu, wawekezaji waje waangalie, kuwekeza na kuongeza thamani ya mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndizi ni zao ambalo linatoka kwa wingi sana katika Jimbo la Rungwe na katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Tunaomba Serikali, kwa Bajeti inayokuja, basi muhakikishe viwanda vingi vinaletwa na kuweza kuongeza thamani katika mazao ambayo tunayasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi; ninatambua kabisa ardhi ina migogoro ya muda mrefu na jitihada mbalimbali zimefanyika. Kuna wawekezaji ambao wanachukua maeneo makubwa, hawayafanyii kazi na wanaondoa wananchi bila utaratibu. Tunaomba muweze kuyasimamia ili wananchi hawa wapate haki katika nchi yao ambayo wamezaliwa, maana hawana sehemu nyingine ya kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kwa mara ya kwanza ninaunga mkono bajeti hii kwa sababu, ninajua kuna mbolea ya parachichi inakuja, ninafahamu kuna visima vya parachichi vitachimbwa. Basi, kwa maana hiyo sina sababu ya kuipinga, ninaiunga mkono hoja ya bajeti hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na Mheshimiwa Bonnah Kamoli, ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama humu kwenye Bunge lako Tukufu na kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoitoa. Kwa kweli, ni nzuri sana, ambayo inaonesha utendaji na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia hili pamoja na Mawaziri ambao wapo chini ya sekta yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa muda wa miaka minne hii, kwa kweli ameonesha kazi ya umahiri. Ni mwanamke shupavu, ni Rais wetu ambaye tunampenda sana, anatuonesha mambo mengi aliyoyafanya kwenye Awamu ya Sita. Kweli tunamshukuru na tunampogeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mkazi wa Morogoro, siachi kuongelea reli ya kati ambayo imejengwa kwa kiwango kikubwa cha kimataifa. Wananchi wa Morogoro na Tanzania tunamshukuru sana kwa sababu, reli hii ya mwendokasi tayari imejengwa kuanzia Dare es Salaam kuja mpaka Morogoro, tunakwenda bila ya matatizo kuja mpaka Dodoma, tunafurahia sana usafiri. Wabunge na wananchi wengi tunatumia usafiri huu wa reli ya kati ambayo ni mwendokasi, ni nzuri sana. Ukikaa humo unatulia na unaweza hata kusinzia, kwa kweli unafika kwa wakati, kwa muda mfupi, ukilinganisha na usafiri wa basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii imeleta ajira kwa vija wetu tunawaona wasichana kwa wavulana, tunashukuru sana. Reli hii ni ya kimataifa ambayo kwa kweli ni ya kiutalii, ni nzuri sana. Jambo muhimu sana kwa reli hii ninaomba sana wananchi, wasafiri pamoja na wafanyakazi waendelee kuitunza. Sehemu hizi ambazo zimebaki za Makutopora – Tabora – Mwanza –

Kigoma ziweze kwenda kwa wakati, ili tuweze kuserereka bila ya kuchelewa. Rais kweli tunaye na tunasema kuwa tunatamba naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninaweza kuongelea ni Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere. Tunamshukuru sana Rais wetu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Biteko na Naibu wake. Kwa kweli, tunafurahi sana kuona umeme tayari umewaka, bwawa limekamilika. Hili bwawa halipo popote, tunasema kuwa, sana sana lipo Mkoa wa Morogoro kwa hiyo, tunashukuru sana pamoja na Mikoa ya Lindi, Pwani na Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme megawati 2,115 ambazo zimeongezwa kwenye gridi na kufikia megawati 4,000 sio chache. Kwa hiyo, tunashukuru, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kusimamia, kumalizia na kulikamilisha hili Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo wazo la kulijenga lilianza enzi za Baba wa Taifa. Kwa hiyo, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la muhimu ni tuweze kusambaza huu umeme uweze kwenda kwenye vitongoji na vijiji kadiri Serikali ilivyopanga, ili kusudi wananchi wote wafurahie umeme huu. Kwa kweli, tunashukuru kwa umeme huu ambao tumepewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kuongelea ni maji. Ninamshukuru sana Mheshimiwa ametenga fedha tumepata maji na miradi ya maji inaendelea. Tunashukuru sana wananchi wengi wanapata maji. Wananchi 76.6% ni ambao wanapata maji vijijini na mijini ni 90%. Kwa kweli, tunashukuru kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao bado hawajapata maji, ninaamini Mheshimiwa Waziri, Aweso, pamoja na Naibu wake hawalali, wanafanya kazi kweli. Kwa hiyo, tunaomba maji yaweze kuwafikia watu wote kwa wakati, lakini tunashukuru kwa hiki tulichopata, unaendelea vizuri, maji tunayo.

Kwa mkoa wangu wa Morogoro tuna maji, lakini kwa ile miradi ambayo bado haijakamilika tunaomba ikamilike kwa wakati, ili watu wote waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaloongelea ni kuhusu barabara, kwa kweli tunajivunia mtandao wa barabara wa lami. Sasa hivi ninaweza nikatoka Dar es Salaam nikaenda mwisho wa nchi yetu. Mwisho wa nchi siyo kwingine ni Mkoa wa Kagera, Ruvuma na hata Tanga, kwa gari bila ya kuwa na tatizo. Hata *saloon* inakwenda kwa sababu mtandao wa lami umeenea. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali kwa ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa barabara hizi za *TARURA* ambazo bado ninaamini fedha zitategwa kwenye bajeti hii tunashukuru sana kuwa, tumepata mtandao mzuri na zenyewe zitajengwa. Ninaamini hata barabara nyingine ambazo bado hazijakamilika, kama asubuhi tuliuliza swali la Barabara ya Ifakara kwenda mpaka Namtumbo, tumejibiwa majibu mazuri; fedha zinatengwa kwa hiyo, hii barabara itajengwa. Mheshimiwa Rais tunamshukuru kwa mambo mengi anayofanya, kwa kweli Watanzania tunajivunia kuwa na yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Kidunda limekuwa la muda mrefu, lakini ninashukuru limewekewa jiwe la msingi. Mheshimiwa Waziri Mkuu tulikuwa pamoja kule Morogoro, aliweka jiwe la msingi. Kwa hiyo, tunamshukuru na tunajivunia sana kuwa na yeye. Tunajivunia sana Rais wetu, mambo mazuri yanakwenda na Bwawa la Kidunda litakamilika watu wa Dar es Salaam na Pwani watapata maji ya kutosha hata Morogoro, vijiji vinavyozunguka Bwawa la Kidunda vitaweza kupata maji ya kutosha na umeme. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa hili kwa sababu, katupatia Mama Samia kuwa Rais wetu. Ahsante Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni vituo vya afya. Ukweli, nani ambaye haoni kuwa Mheshimiwa Rais amejenga vituo vya afya vingi, kila jimbo na mkoa tuna vituo vya afya. Tunajivunia sana kuwa na vituo vya afya, sasa hivi madaktari wataletwa na pale ambapo hawatoshi watawekwa, ikiwa ni

pamoja na dawa zitakuwepo. Kwa kweli, tunashukuru, mambo ni mazuri, ila maboma ambayo bado hayajakamilika tunaomba yakamilike kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninashukuru, nina furaha sana pale ninapoongea kuwa, Mama Samia amefanya mambo mazuri. Kweli tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia Rais wetu. Ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu ambariki. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ishengoma. Ninamwita sasa Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Bonna Kamoli na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo kwa kweli, ameionesha kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na mwenzangu kusema kwamba, wakati anaachiwa nchi miradi mikubwa iliyokuwa imeanzishwa kama asingekuwa shupavu, miradi hii, isingeendelea na isingekamilika. Kwa kweli, sisi tunajivunia uwepo wake na utendaji kazi mzuri ambao kwa kweli, Watanzania tulikuwa tunahitaji Rais wa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo wenzangu wamezungumza, uchumi unakuzwa na miundombinu. Miundombinu ya reli, kwa sasa watu ambao tunasafiri kutoka Dodoma – Dare es Salaam kwa kweli, wameturahisishia sana kwa gharama ndogo na pia, muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara pia zimeendelea kufunguka na madaraja yameendelea kujengwa. Ama kweli, lile ambalo limesemwa kwenye Biblia kwamba, watu walivuka baharini kwa Fimbo ya Mussa, ndilo ambalo tunakwenda kuliona Usagara – Busisi kwenda Sengerema ambavyo daraja linaendelea kukamilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri Mkuu, ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Amekuwa nasi hapa akitusikiliza, lakini amekuwa kioo kwa Mawaziri wengine. Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa mtendaji mzuri sana wa Serikali kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuyazungumza haya kwa sababu, tarehe 21 ukiondoa mengine, mwezi Desemba alikuwa kwangu Magu. Alipoingia tukaanzia pale Kisesa, Bujora, ambapo kulikuwa na tenki kubwa la maji, likikamilika litasaidia Miji ya Bujora na Kisesa. Mvua ilianza kunyesha, Waziri Mkuu hakusita akaanza kuongea na wananchi mvua inanyesha. Huyu ni Waziri Mkuu wa aina tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni Waziri Mkuu wa aina tofauti, tumeona Mawaziri Wakuu, lakini huyu ni wa tofauti. Tunaomba Mwenyezi Mungu aendelee kutusimamia na kumpatia moyo huo huo wa kuwajali wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotoka pale tulikwenda Shule ya Wasichana ya Kimkoa na tulipotoka pale tulienda Nghaya. Tulipofika Nghaya kwenye daraja ambalo Rais ametupatia shilingi bilioni 9.3, maana yake ni kwamba wale tunaobeba fedha kwenye mabegi ni mabegi 93 yamewekwa pale Nghaya. Mvua ilimwagika, Waziri Mkuu hakusita, akatoka mbele ya turubai akasimama kwa wananchi akaanza kuwahutubia wananchi mvua inanyesha mpaka mwisho wa hotuba yake. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri kwa kweli, yeye anamsaidia Mheshimiwa Rais kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakusita, tukaondoka hapo tukaenda kwenye Daraja la Simiyu ambalo Mheshimiwa Rais ametupatia shilingi bilioni 148 na linaendelea kujengwa. Sisi tunaobeba mabegi shilingi milioni 100 ni sawa na mabegi 480; haijawahi kutokea fedha hizo kuletwa Magu, kwa kweli tunakupongeza Mheshimiwa Rais kwa kutupatia fedha nyingi kiasi hicho. Pia, tunampongeza Waziri Mkuu alitembea mvua ikiwa inanyesha, akiwa unawahutubia wananchi maelfu kwa maelfu. Aendelee kuwa na moyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapompongeza Mheshimiwa Rais na pia, tunaendelea kusema mapungufu ambayo kwa kweli, sasa hivi tunahitaji fedha, kwa ajili ya kumalizia. Mradi wa Maji wa Lugeye ambao upo 65%, Mradi wa Iseni, Nyanghanga, Mradi wa Mwamabanza, Mwarina-Salonghwe ambao upo 85% ni fedha kidogo tu za kumalizia hii miradi wananchi waweze kupata huduma. Tunaamini mipango ya Serikali muda si mrefu itatoa fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapompongeza Mheshimiwa Rais kwa kuleta fedha nyingi za elimu, madarasa mengi yamejengwa. Tunaendelea kukupongeza Waziri Mkuu kwa usimamizi wako madhubuti ambao kwa kweli, umeendelea kujionesha kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niendelee kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita. Tulikuwa na jengo ambalo limeanza mwaka 2012, limekaa kwa muda mrefu, lakini sasa hivi ninafurahi kusema kwamba, Halmashauri yangu ya Magu imehamia mwaka huu kwenye jengo jipya ambalo Mheshimiwa Rais ameendelea kutupatia fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapompongeza Mheshimiwa Rais tunaendelea pia, kupongeza jitihada, hasa kwenye vituo vya afya ambavyo tumepewa na vifaatiba vinavyojitosheleza. Wananchi sasa hivi wanapata matibabtu ya kutosha huko kwenye vituo vya afya kuliko hata kwenda kwenye Hospitali zetu za Wilaya. Tunaomba tuendelee na Serikali iendelee kuweka fedha, hasa kwenye vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina Kituo cha Afya pale Nghaya, kimebakiza shilingi milioni 250 kukamilika; ni pale ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimama, mvua inanyesha. Pale Busaranga kituo kile kinapelea shilingi milioni 250 tu kiweze kukamilika kwa hiyo, tunahitaji Serikali inapopata fedha iweze kutupatia. Pia, hata kwenye kituo cha afya ambacho tulikuwa tumekipatia kipaumbele, kama ambavyo Serikali walielekeza kwamba, angalau kila jimbo liweze kuleta orodha ya kituo kimoja kimoja. Kituo cha Lutale nacho tunahitaji fedha, kwa ajili ya kukamilishwa ili kiweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya mambo mengi na tunaamini kwamba, mahitaji ya Watanzania yapo mengi. Tunapokwenda kwenye umeme, sasa tumekwenda vitongoji 15 ambavyo Serikali imetupatia, ninafurahi kusema kwamba, vitongoji 15 kwenye Jimbo la Magu mkandarasi yupo kazini na anaendelea vizuri. Sasa tunahitaji vitongoji vingine na hapa, tunaomba watuangalie sisi wenye majimbo makubwa. Serikai haiwezi kutufananisha na majimbo mengine madogo na ikatugawia labda vitongoji 50 kila mmoja, wengine tupo *double*, naomba waangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo ambapo ninataka nisisitizie kwamba, sisi tulio na majimbo makubwa watupatie angalau vitongoji vingi kwa sababu, mimi nina vitongoji 508, huwezi kufanisha na mtu mwenye vitongoji 206, kwa kweli waangalie hilo. Wizara ya Nishati iweze kupima ukubwa wa majimbo yetu, halafu iweze kutupatia vitongoji ambavyo vinafanana na majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapompongeza Mheshimiwa Rais, ninataka tu niseme kwamba, tumepiga hatua kubwa. Kama ambavyo wenzangu wamezungumza, Bajeti ya Barabara, *TARURA* ilikuwa ni shilingi milioni 830, leo nina shilingi bilioni 2.8. Maana yake ni kwamba, nimeongeza fedha ambazo tulikuwa hatuna kuanzia mwaka 2020. Hata hivyo, bado uhitaji wetu wa barabara ni mkubwa mno kwa sababu ya maeneo yenyewe husika, hasa kwenye Mji wa Kisesa na Bujora. Niombe hili kwamba, katika fedha za wafadhili zinazokuja kuboresha miji, Mji wa Kisesa na Bujora unatakiwa uwekwe sasa kwenye mpango wa kuboreshwa na fedha hizi za wadafhili, hasa *World Bank*, kwa ajili ya kuhudumia barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapompongeza Waziri Mkuu na Mawaziri wanaomsaidia. Kazi hii ya kumsaidia Mheshimiwa Rais ni kubwa. Alipoanza Waziri Mkuu kwamba, mazao matano ya kimkakati pamba, chai na mengine, ninataka nimhakikishie kwamba, ninampongeza sana Waziri wa Kilimo, ameanzisha utaratibu mzuri wa *BBT* hata wafanyabiashara wa uchambuaji wa pamba wakakubaliana kuwalipa vijana waliotoka vyuo vikuu,

kwa ajili ya kusimamia kilimo. Mwaka huu tunayo matumaini makubwa kwamba zao la pamba litakwenda kuongezeka. Ni kazi ya Serikali sasa kuona mwenendo wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya kazi kubwa sana ya kuhamasisha. Kwa hiyo, hapa Mawaziri wanamsaidia kikamilifu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kengele ya pili.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umeisha?

**MWENYEKITI:** Umeisha. Kengele ya pili.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaunga mkono hoja, lakini namhakikishia kwamba, Wabunge tutaendelea kumwombea Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais aendelee kumwamini kwa sababu, anamsaidia kikamilifu. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangira na Mheshimiwa Michael Joseph Mkundi, ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya. Pia, ninampongeza kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa kuweza kukutana na wananchi wangu wa Kata ya Kipawa, kufanya nao vikao na hatimaye hao wananchi wakalipwa. Kwa hiyo, ninachukua nafasi hii kumpongeza kwa niaba ya wananchi wa Kata ya Kipawa. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kutuona na kuweza kuanza kutulipa kwa kilio ambacho tulikuwa nacho kwa takribani miaka tisa; kwa kuweza kuwaona sasa wananchi wa Kipunguni. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwaona wananchi wa Kipunguni ambao wamekaa kwa muda wa miaka 27 wakidai madai yao ya fidia ili waweze kupewa fidia kutokana na viwanja vyao ambavyo vilichukuliwa na *Airport*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza vile vile Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa. Kwa namna ya pekee ninampongeza sana sana Naibu Waziri Mheshimiwa David Kihenzile kwa kazi kubwa aliyoifanya, kwa kuja Kipunguni na kuongea na wale wananchi. Pia, ninampongeza Mkurugenzi wa Viwanja vya *Airport*, ambaye ni Ndugu Mambokaleo kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa wananchi wangu wa Kipunguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sasa ninaomba nitoe hotuba yangu. Kwanza nianzie kwa watu wa Kipunguni, kwamba wamelipwa, lakini waliolipwa si wote; wamelipwa nusu. Nimepata habari sasa hivi kwamba wale waliobaki wataanza kulipwa mwezi huu. Kwa hiyo, ninaendelea kushukuru na ninaendelea kuwaasa wananchi wa Kata ya Kipawa waendelee kuwa na uvumilivu, kwamba tulielewana malipo yatakuwa ni ya awamu. Wamelipwa awamu ya kwanza, lakini pia awamu ya pili inaenda kulipwa mwezi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ninaomba niipongeze sana Serikali kwa Mradi wa *DMDP*. Kama mnavyojua, kwa kweli Mkoa wetu wa Dar es Salaam kila siku tumekuwa tunauongelea kutokana na mvua ambazo zinanyesha, lakini pia miundombinu ambayo haiko vizuri katika Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa sasa Mradi wa *DMDP* umesainiwa. Tunachokiomba tu Serikali ni kwamba, hao watu ambao wamesaini au hawa wakandarasi ambao

wameshasaini Miradi ya *DMDP*, sasa waanze kwa haraka. Kwa sababu huu mradi tumeusubiri kwa muda mrefu, lakini hatimaye umesainiwa. Ninampongeza sana Waziri wa TAMISEMI kwa kuweza kulikamilisha jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na *issue* ya Bonde la Mto Msimbazi. Pamoja na miundombinu ambayo tunaisema Mkoa wa Dar es Salaam, lakini pia katika majimbo yetu, takribani majimbo yote tuna Bonde la Mto Msimbazi, bonde ambalo limepita katika Jimbo la Segerea, limepita katika Jimbo la Ukonga, liko Ilala, liko Kinondoni na pia liko Kawe. Bonde hili la Mto Msimbazi ni muda mrefu sana tumekuwa tukiambiwa kwamba litaanza kujengwa. Kama unavyojua, juzi juzi hapa mvua imenyesha Dar es Salaam na watu bado wameendelea kupata mafuriko. Wananchi wengine wanajua kabisa kwamba bonde hili lilikuwa kwenye mkakati wa kuendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka katika majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu atakavyokuja kuhitimisha, atuambie sasa Bonde hili la Mto Msimbazi limefikia wapi? Kwa sababu ndilo bonde ambalo linaendelea kutupa shida katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kama nilivyosema, shida si katika jimbo moja, ni shida katika majimbo yote. Unaweza labda ukasema kwa sababu majimbo mengine yako mbali hayajaweza kufikiwa, lakini pia kuna mikondo ile ambayo imefika kwenye majimbo hayo. Kwa hiyo, ni mkoa mzima ambao unaathiriwa na Mto Msimbazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililotaka kuongea ni kuhusiana na *issue* ya miundombinu ya elimu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Katika Mkoa wa Dar es Salaam hususan jimbo langu kwa kweli madarasa mengi yameongezwa, shule nyingi za sekondari zimejengwa. Katika shule tisa ambazo zimejengwa katika hii miaka minne ya Mheshimiwa Rais, kwenye jimbo langu peke yake zimejengwa shule nne za ghorofa na shule moja ina madarasa 40. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba, katika jimbo langu kuna shule ambazo zitachukua watoto ambao walikuwa wanakwenda kusoma sehemu tofauti; kwa hiyo, watabaki pale pale katika Jimbo langu la Segerea, Wilaya ya Ilala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kupongeza sana, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, pia ninampongeza Waziri wa TAMISEMI kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Ninapenda kuwaambia Wabunge wenzangu hapa kwamba, shule ambazo tumejenga katika Jimbo langu la Segerea ni shule ambazo ni za mfano kwa sababu kuna shule za ghorofa nne, lakini pia kuna shule tano ambazo ni shule za msambao. Kutokana na Jimbo langu la Segerea kuwa na sehemu ndogo ya ya kujenga tumeamua sasa tujenge madarasa au shule za ghorofa ili tusitumie nafasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ninapenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa TAMISEMI kutokana na kazi kubwa ambayo ameifanya kwenye Sekta ya Afya. Katika Jimbo langu la Segerea kabla ya Mama Samia kuingia hatukuwa na kituo cha afya. Kwa sasa hivi tuna Kituo cha Afya Kata ya Kinyerezi, tuna Kituo cha Afya Kata ya Kiwalani na tuna Kituo cha Afya Kata ya Segerea. Bado tunaendelea kutafuta maeneo mengine ili kuweza kujenga vituo vya afya. Kwa hiyo, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana sana sana Mheshimiwa kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ili kuwaletea huduma za karibu wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ninataka niongelee suala la 10% kwa vijana, akinamama, pamoja na walemavu. Tunashukuru kwamba kipindi kilichopita watu waliweza kufaidika sana kutokana na hii 10% mpaka iliposimamishwa. Sasa hivi imeanza kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kuwaomba wananchi, kwa sababu kuna wananchi wengine bado hawajajua na hawajui kwamba hii 10% inatoka. Kwa hiyo, waende watengeneze vikundi ambavyo vinaweza kuwasaidia kwenda halmashauri na kufuata masharti. Pia, ni muhimu sana kuweza kurudisha hizi pesa ili na watu wengine waweze kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Mkundi na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninapenda kuanza kuchangia mchango wangu katika eneo la Taasisi ya Chakula na Lishe *(TFNC)*. *TFNC* ilianzishwa kama shirika la umma la kutoa huduma, kwa Sheria ya Bunge Na. 28 mwaka 1973.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uundwaji wa taasisi hii ilikuwa ni utekelezaji wa maono ya Baba wa Taifa, kwa maana ya kuhakikisha kwamba tunalinda Taifa letu vizazi kwa vizazi katika eneo la lishe pamoja na chakula. Eneo la lishe pia, ninapenda kumpongeza na kumtambua Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Kinara wa Lishe tangu akiwa Makamu wa Rais. Hivyo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anaendeleza utekelezaji wa maono ya Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusikitika, Disemba, 2023, Waziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Utekelezaji aliitangaza *TFNC* kama moja ya mashirika ambayo yanafutwa kwa sababu hayazalishi ilihali Shirika hili la *TFNC* lilianzishwa kwa sheria na kutambuliwa kwamba ni shirika la kutoa huduma. Hivyo, suala la uzalishaji wa mapato na fedha halimo kabisa katika msingi wa uanzishwaji wa Shirika hili la *TFNC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki cha hivi sasa tangu tangazo hili litoke, kumekuwa na sintofahamu kubwa kuhusiana na namna ambavyo masuala ya lishe yatakavyoratibiwa katika Taifa letu. Hatueleweki kama Tanzania. Wakati bado tuna uhitaji mkubwa na tuna changamoto nyingi za masuala ya lishe (utapiamlo) na aina zote nyingine, sisi tunaamua kwenda kufuta shirika kama la *TFNC*. Wakati umefika sasa tufikirie upya uamuzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, ninaomba nishauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, hivi karibuni Serikali iliamua kutokuendelea na uamuzi wake wa kufuta Shirika la Elimu Kibaha. Kwa msingi huo huo, kama Serikali iliweza kutambua kwamba kutaka kulifuta Shirika la Elimu Kibaha ilikuwa ni makosa na itakuwa na madhara makubwa, basi kwa msingi huo huo ninaiomba sana Serikali ipitie upya na ifute ule uamuzi wa kufuta shirika hili la Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania, kwa sababu bado lina umuhimu mkubwa na tuna uhitaji nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili katika eneo hili, Serikali ifanye marekebisho kwenye Sheria ya Chakula na Lishe Sura ya 199, ili Taasisi ya Chakula na Lishe iwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambaye sasa hivi ndiye anayeratibu masuala ya lishe, kwa sababu masuala ya lishe ni masuala mtambuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zimeshaonyesha kuchangia kudhibiti na kupambana na masuala ya utapiamlo kwa upande wa Wizara ya Afya, inachangia 20% tu, 80% inachangiwa na sekta nyingine. Hivyo, ni muhimu sana Taasisi ya Chakula na Lishe kuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye pia ndiye anayeratibu Mpango Jumuishi wa Lishe *(NMNAP)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia hapa kwa unyenyekevu mkubwa nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu ahadi aliyotoa tarehe 3 Oktoba, 2024, kwenye mkutano Mwanza kuhusiana na suala hili la kurejesha *TFNC* na ahadi hii Mheshimiwa Waziri Mkuu aliitoa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu, Mzee wetu Mheshimiwa Mizengo Pinda. Kwa hiyo, ninaamini kupitia hotuba hii ya bajeti tutapata kusikia kauli ya Serikali kuhusiana na nini Serikali inakwenda kufanya katika kuiokoa na kuirejesha Taasisi ya Chakula na Lishe *(TFNC)*, kwa sababu bado tuna uhitaji nayo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la pili ni usalama wa chakula *(food safety)*. Hali ya sasa ya vyakula vinavyouzwa sokoni, na hivi ni vyakula vinavyotoka ndani na nje ya nchi, hairidhishi, kwa maana ya upande wa usalama wa chakula, eneo la *food safety*. Mwaka 2019, kwa maono na mapenzi mema

kabisa Serikali iliamua kufua *TFDA* na kuhamishia jukumu la udhibiti wa usalama wa chakula *(food safety)* kwenda *TBS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme kwa uwazi kabisa, *TBS* imeshindwa kuratibu na kudhibiti masuala ya usalama wa chakula. Hatuwezi kuendelea kuendesha suala la usalama wa chakula kibiashara. Suala la usalama wa chakula ni suala ambalo linahusu uhai na afya za Watanzania. Hatuwezi kuendelea kuweka maisha ya Watanzania rehani kwa sababu tu ya kuangalia maslahi ya kibiashara. Kwa hiyo, wakati umefika sasa, kwa unyenyekevu mkubwa chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tupate kauli ya Serikali. Maana katika Bunge hili tangu mwaka 2021 tumekuwa tukiomba Serikali irejeshe masuala ya udhibiti na usimamizi wa usalama wa chakula *(food safety)* Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata ahadi mbalimbali hapa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imeshajadili, Serikali imeona lina tija, suala hili liko kwenye uamuzi wa mwisho. Ninaomba sana tupate kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je, ni lini sasa suala la udhibiti wa usalama wa chakula *(food safety)* litarejea Wizara ya Afya ili tuache kuendelea kuweka maisha ya Watanzania rehani kwa sababu tu ya maslahi ya kibiashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni pana kwa sababu, katika makubaliano ya Kikanda na Kimataifa ili uweze kuuza vyakula vyako nje ya nchi, suala la usalama wa chakula ni muhimu. Sasa hivi Tanzania kuna maeneo ambayo tunapata changamoto kuuza mazao yetu nje ya nchi kutokana na kwamba tunashindwa kukidhi vigezo vya usalama wa chakula, kwa maana ya *chemical residue* pamoja na masuala mengine yanayoendana na hayo. Kwa hiyo, suala hili la usalama wa chakula si suala la kuendelea kulichukulia kwa wepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niiambie Serikali jambo moja, kama haifahamu. Sasa hivi ukienda pale *TBS* wale wataalam wetu wa *food safety* sasa hivi hata vyeo vyao vya *food safety* havipo tena. Sasa hivi wote wanatambuliwa kama *Quality*

*Assurance Officers*. Wataalamu wetu wa *food safety* sasa hivi wanafanya kazi ya kupima ubora wa nondo. Haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikubaliki katika Taifa ambalo tumeona ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukiza. Tumeona ongezeko kubwa la magonjwa ya *cancer*; tumeona namna gani ambavyo Mfuko wetu wa Bima ya Taifa ambavyo umeelemewa, ambapo zaidi ya 70% ya magonjwa yanayotibiwa pale ni magonjwa yasiyoambukiza. Magonjwa haya ni magonjwa ambayo yanaepukika. Yanaepukika kwa kuhakikisha tuna mfumo ulio thabiti wa kulinda suala la usalama wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, suala la usalama wa chakula haliwezi kuendelea kuwa chini ya *TBS*. Tumesema sana ndani ya Bunge hili, nalo tumepata ahadi nyingi sana ndani ya Bunge hili. Sasa, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa unyenyekevu na kwa uchungu mkubwa wa maisha ya Watanzania, tufike mwisho kwenye jambo hili. Tusiendelee kurudisha nyuma jitihada za Serikali. Serikali inafanya uwekezaji mkubwa sana kwenye maeneo mengi, halafu tunatumia fedha nyingi sana kutubu magonjwa ambayo yanaepukika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya jitihada kubwa sana kuweka wawekezaji kwenye maeneo mengi yenye tija, halafu tunarudisha na kufifisha jitihada hizo kwa kupunguza ubora wa nguvu kazi yetu. Jambo hili halikubaliki na sasa wakati umefika lifike tamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa kuzingatia masuala ya chakula, lishe na usalama wa chakula ni masuala ambayo yanashabihiana. Ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa sana niishauri Serikali ifikirie namna ya kuunda chombo kipya chenye hadhi na mamlaka zaidi ya kuratibu, ya kuongoza, ya kusimamia, ya kudhibiti na kushauri katika eneo hili la chakula, lishe na usalama wa chakula *(food safety)*, kupitia Sheria ya *Executive Agencies Act, CAP*. 245. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana. Ninaamini chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu

wetu Kassim Majaliwa na namna ambavyo yeye mwenyewe ni Kinara wa Lishe, ni Kinara wa Usalama wa Chakula, tutapata ufumbuzi na kauli thabiti ya Serikali ni lini *TFNC* inarejeshwa na ni lini masuala ya usalama wa chakula *(food safety)* yataondolewa *TBS* na kurejeshwa Wizara ya Afya. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Michael Mkundi, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Massare na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma Kikoyo ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kunijaalia uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya na kuwatendea wananchi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ukerewe kama sehemu ya Taifa hili, tangu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia ameingia madarakani limefaidika kwa miradi mingi sana ya maendeleo. Karibu kila sekta wananchi wa Ukerewe wamenufaika na uongozi wake; Sekta za Afya, Elimu, Nishati, Miundombinu na nyinginezo. Kwa hiyo, ninampongeza sana na kumshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake; hotuba nzuri ambayo pia inaakisi utendaji wake mzuri. Sina mashaka na yale yaliyoko kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, mambo mengi sana yamefanyika kwenye maeneo yetu. Ukerewe ikiwa sehemu ya Taifa hili kama nilivyosema, imenufaika kwenye maeneo mengi. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninampongeza kwa namna ambavyo Serikali imetekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani yetu ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 – 2025, Ibara ya 9(f) inaelezea dhamira ya Serikali kutengeneza ajira 8,000,000. Kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mpaka sasa ajira milioni 8.08 zimetengenezwa. Kwa hiyo, ninapongeza sana kwa utekelezaji wa Ilani yetu ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango wa Maendeleo wa Mwaka wa Fedha 2025/2026, moja ya misingi ambayo itatupelekea kwenye mafanikio ya kuongeza ya ajira hizi ni ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Ni kwamba sekta binafsi ina mchango mkubwa sana kwenye utengenezaji wa ajira hizi, ndiyo maana utaona katika ajira milioni 8.08 zilizotengenezwa mpaka sasa ni milioni 1.04 tu ambazo ni sekta iliyo rasmi na karibu milioni 7.04 ni sekta isiyo rasmi. Hii inaonesha namna mchango wa sekta binafsi ulivyo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi inaweza ikaingia kwenye uchumi, kutengeneza hizi ajira kama miundombinu na mazingira wezeshi yatakuwepo, lakini kama kutakuwa na kikwazo itakuwa ni changamoto kubwa. Kwa maana hiyo, ule uchumi jumuishi au kwa Kikerewe tunavyoita *inclusive economy* itakuwa ngumu kidogo. Sasa kwenye eneo hili niombe ili wananchi wa Ukerewe waweze kuwepo na wajumuike kwenye huu uchumi jumuishi kuna baadhi ya maendeleo ninaomba Serikali iyafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, miradi iliyokuwa imeanzishwa na haijakamilika basi iweze kukamilishwa; baadhi ya miradi ya maji, Serikali ifanye kila linalowezekana ili iweze kukamilika. Vilevile, miradi ya barabara ni muhimu sana, kwa mfano, Barabara ya kutoka Bunda kuja Nansio ambayo mkandarasi aliingia *site* pale akavuruga barabara ile ili aanze kuitengeneza lakini kwa sababu ya kutolipwa pesa yake ameondoka *site* inaathiri sana uchumi wa wananchi wa Ukerewe. Kwa hiyo, niombe kwa msisitizo mkubwa, Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tusaidie barabara hii

iweze kukamilishwa ili wananchi waweze kushiriki kwenye uchumi jumuishi, lakini na kutengeneza ajira kupitia sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani kushauri kwenye maeneo mengine mawili, kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kupandisha utalii wetu kupitia *The Royal Tour Film* pamoja na *Amazing Tanzania* ambayo imepelekea idadi ya watalii kuongezeka kutoka milioni 1.048 mpaka kufikia idadi ya watalii milioni 1.1 karibu tisa, ni jambo jema sana. Bahati njema sana tuna fursa kubwa ya kuongeza idadi ya watalii. Kwa mfano sasa tunaelekea kwenye michezo ya *AFCON* ambapo Tanzania itakuwa mwenyeji mwaka 2027, lakini kinachonitia mashaka na ambacho ningependa kushauri, sioni kama tunaweka nguvu kubwa sana kwenye matangazo ili kuweka *awareness* ya kidunia, watu wajue kwamba mwaka mmoja au miaka miwili ijayo kuna tukio kubwa litakuwepo Tanzania na watu wajiandae kuja kushiriki, kuhudhuria kwenye michezo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala yake kwa sababu tunaandaa na nchi nyingine tukishirikiana, wenzetu wataanza kuwa bora kwenye matangazo na kwa hiyo watalii wataingia kwenye nchi zile sisi tutakuwa wanufaika watatu au wa pili kupitia fursa ya michezo hii ya *AFCON*. Kwa hiyo, ninashauri kuanzia sasa Serikali ione umuhimu wa kuweka nguvu kubwa kwenye kutangaza michezo hii ili dunia ijue kwamba mwaka mmoja ujao au miaka miwili ijayo katika nchi ya Tanzania kuna tukio fulani litakuwepo itangaze vivutio vyetu vya utalii iweze kuwa sehemu ambayo fursa hii ya utalii tukaitumia vizuri kupitia michezo hii ya *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la tatu ambalo ningependa kushauri kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, niipongeze Serikali imeonesha kukua kwa diplomasia ya uchumi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kama mwanadiplomasia namba moja. Changamoto iliyopo na ambayo ninaiona ni kweli kwamba kama Taifa tumefanya kazi kubwa sana kupandisha diplomasia ya kiuchumi, tumeshiriki mikutano mingi sana ya nje, viongozi wetu wakuu wameshiriki sana mikutano mingi ya nje na

shughuli mbalimbali za kiuchumi za kimataifa tumeshiriki; na sisi kama Taifa hapa nchini tumeandaa mikutano na shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo watu wengi wamekuja wakahudhuria lakini kuna shida moja ambayo tunaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la elimu kwa wananchi wetu. Wananchi wetu hawana elimu ya kutosha kuweza kujua hii diplomasia ya uchumi ni nini na fursa zinazojitokeza ni namna gani wananchi wa Taifa hili waweze kutumia zile fursa ili waweze kufaidika na fursa zilizopo kupitia diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya mambo ya nje inafanya kazi kubwa sana kuunganisha na kutafuta fursa mbalimbali kwenye mataifa mbalimbali nje ya nchi, lakini namna gani sasa sisi kama jamii tuna *grab* zile fursa ili tuweze kuzitumia. Kwa hiyo, ningeshauri moja ili kuongeza *awareness* lazima tuwe na *programs* maalum kwa ajili ya kuelimisha kupitia idara, Wizara na maeneo mbalimbali. Kwenye ofisi zetu wanakuja watu wa nje kwa mfano wanakuja kuleta fursa, lakini wanapoingia kwenye ofisi kwa mfano za halmashauri zetu au kwenye idara mbalimbali inachukua muda mrefu kuhudumiwa jambo ambalo linachelewesha matumizi ya fursa zile ambazo Wizara ya Mambo ya Nje au taasisi nyingine yoyote imezifanyia kazi kuzileta nchini. Kwa hiyo, ni muhimu sana tukawekeza kwenye ku-*create awareness* kwa wananchi wetu ili wajue hii diplomasia ya uchumi ni nini na namna gani sasa tunaweza tukaitumia kwa ajili ya kutengeneza ajira, lakini na kuimarisha uchumi wetu kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye eneo hilo hilo, kwenye diplomasia ya uchumi ninahisi kunakosekana chombo maalum kwa ajili ya kuratibu ili fursa hizi zinapotengenezwa na Wizara ya Mambo ya Nje basi namna gani Wizara nyingine au idara nyingine zinashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje ili kufanya fursa hizi ziweze kuonekana na kuweza kutumika. Kwa hiyo, Serikali ifanyie kazi mambo haya ili tuweze kutengeneza uchumi kupitia diplomasia hii ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Yahaya Massare, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma Kikoyo na Mheshimiwa Salome Makamba ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii na nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa chama changu (Chama Cha Mapinduzi), kwa jinsi anavyoipeperusha bendera yetu vizuri na kufanya takwa la kikatiba ambalo mwaka huu linategemewa kufanyika. Ninaamini chama changu kitaenda kushinda kwa kura nyingi sana kutokana na kazi nyingi zinazofanywa na watu wanaomsaidia Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake yenye kurasa nyingi zaidi ya kurasa 110 ambazo kwa hakika zimesheheni mambo ya msingi na yenye tija kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi ya Waziri Mkuu inazo taasisi nyingi na za muhimu ikiwemo Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo mwaka huu inaenda kusimamia Uchaguzi Mkuu, ambalo ni takwa la kikatiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, Tume hii Huru ambayo imebadilika kutoka Tume ya Uchaguzi sasa na kuwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye Msajili pia wa Vyama vya Siasa, lakini na taasisi nyingi ambazo zipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambazo kwa hakika ufanisi wake unaifanya Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kufanya kazi ambazo zimetukuka sana katika kipindi hiki cha miaka minne. Ninaomba nichukue nafasi hii kupongeza kazi ambazo zimefanyika katika sekta zote hususan Sekta ya Elimu, Sekta ya Afya, Sekta ya Maji, Sekta ya Nishati na Sekta ya Mawasiliano katika Jimbo langu la Manyoni Magharibi

ambalo siyo muda mrefu sasa litaenda kuitwa Jimbo la Itigi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha miaka minne Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na mimi Mbunge wake na Madiwani wetu katika Halmashauri yetu ya Itigi tumeletewa pesa nyingi sana na Serikali na kujenga shule nyingi ya msingi na sekondari. Sasa, mfano mdogo, kuna kijiji kilikuwa na shule moja sasa kina shule nne, kingine kina shule tano, kingine hadi shule saba, kutoka shule moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni namna ambayo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia inavyofanya kazi kwa weledi mkubwa sana hasa katika kuhakikisha watoto wa wakulima na wafugaji ambao walikuwa *scattered* wamekaa kufuata mazingira bora ya kilimo katika eneo langu sasa wamepelekewa shule. Kwa hiyo, watoto wale ambao kaka zao na dada zao walikosa fursa ya elimu leo wanaenda kusoma pasipo na shida japo kutakuwa na changamoto kadha wa kadha pengine walimu hawatatosha lakini tumeanza na majengo, maana yake kitakachofuata ni hayo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ukurasa wa 58 imezungumzia sana juu ya suala zima la elimu katika nchi hii lakini suala la afya katika ukurasa wa 62; lakini suala la maji katika ukurasa wa 61, kwa hakika ninataka niseme pia Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu huyu anaitendea haki nafasi yake na anatutendea haki sisi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa naye humu katika Bunge hili na yeye kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika nyumba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri haya ninatamani kuishauri Serikali yangu baadhi ya maeneo ambayo yanapaswa kwenda kufanyiwa kazi. Mkoa wa Singida hadi tunavyozungumza hivi haujaunganishwa na Mikoa ya Mbeya na Simiyu kwa njia ya Barabara. Mkandarasi yupo *site* lakini bado anasuasua, kama zipo changamoto ambazo wanaziona hawajaenda naye sawa ninaomba Serikali ikae naye mezani

amalizie kipande hiki ambacho anaendelea nacho ili wananchi wa jimbo hili na wananchi wa Mkoa wa Mbeya na wa Mkoa wa Singida, lakini kuunganishwa na Mkoa wa Simiyu kupitia Daraja la Sibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mtu akitoka nchi Jirani ya Kenya akipita Mkoa wa Mara akaja Simiyu kama anakwenda Mbeya hatakiwi kupita Morogoro, hatakiwi kupita Dodoma, anatakiwa apitie Itigi kama barabara ni ya lami anakutana na Mkoa wa Mbeya, anaingia *boarder* nyingine ya Zambia. Kwa hiyo, Mkoa wetu wa Singida umepakana na mikoa miwili, Mkoa wa Mbeya ambao ni mkoa wa mpakani, Mkoa wa Simiyu unaenda kupakana na Mkoa wa Mara ambao nao ni mpakani. Kwa hiyo, maana yake fursa ya kufungua Mkoa wa Singida kwa barabara unatengeneza uchumi wa nchi hii, unamsaidia mwananchi wa Tanzania na wa nchi jirani ambaye anakusudia kufanya biashara na nchi nyingine jirani kutoka ukanda mmoja kwenda ukanda mwingine. Vilevile ni *corridor* muhimu sana ya katikati kiuchumi tukiacha hii ya kupita Babati, Dodoma, Iringa lakini *corridor* nyingine ni ile pale mtu anatoka Moshi anakuja Arusha, Manyara, Singida tayari ameshafika Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu wa zaidi ya kilometa 150 mtu anayepita anayetoka Moshi kwenda Mbeya kupitia Babati, kupitia Dodoma na Iringa na yule atakayepitia Babati, Singida na kwenda Mbeya atapunguza zaidi ya kilometa 150 kama barabara hii itakuwa ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mengine hayo lakini kwenye Sekta ya Nishati, pia ninaomba niipongeze sana Serikali yangu, kwa kazi nzuri na kubwa zilizofanyika katika sekta hii. Vijiji vyangu vyote vimewashiwa umeme na sasa tunakwenda vitongojini. Ninaomba sasa nihimize Serikali mkandarasi wa Mkoa wa Singida hajapatikana, basi katika kipindi hiki kifupi tukiwa humu ndani tumwone mkandarasi wa Mkoa wa Singida naye amepatikana ili na sisi tu-*enjoy* fursa hii ambayo wenzetu wa mikoa mingine hapa wamekuwa wakitamba kwamba vitongoji vyao vinapelekewa umeme, sisi Mkoa wa Singida bado jambo hilo halijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawasiliano ya mitandao ya simu, mawasiliano ya redio, niipongeze sana Serikali kwa jitihada za kuweka na kutenga pesa nyingi, leo baadhi ya maeneo ya jimbo langu ambayo yalikuwa na changamoto kubwa ya mawasiliano yanaenda kupatiwa huduma hii adhimu na mahsusi. Kama nilivyosema jimbo langu lipo sehemu kubwa linaelekea Mbeya maeneo ya Kintanula leo mkandarasi yupo *site* anajenga mnara kwa hakika ni jambo ambalo limesubiriwa kwa muda mrefu sana na nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hilo, lakini bado usikivu wa Redio ya *TBC* haupo vizuri katika eneo zima la Halmashauri ya Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walizindua mnara pale Manyoni tukitegemea kwamba Itigi napo utasikia, leo hausikiki kabisa. Ninaomba jitihada za makusudi za Serikali tunapoelekea katika uchaguzi, wananchi wetu wanapenda kusikiliza redio zao zaidi kuliko *TV*, maana yake kule vijijini nguvu ya wananchi kununua *TV* ni ndogo wanaweza kununua karedio kale kadogo na wakasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Ishengoma Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba na Mheshimiwa Tecla Ungele na Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae baada ya hao.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kunipa fursa ya kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nianze na shukurani kwa kazi kubwa ambayo imefanyika ndani ya kipindi cha miaka mitano hususan katika Sekta za Mawasiliano, Ujenzi na Uchukuzi; nimechukua hizo sekta. Ninaishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanyika hasa Ziwa Victoria, ujenzi wa bandari na kuimarisha uchukuzi katika Ziwa Victoria lakini na Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali imekarabati Bandari ya Bukoba na imekarabati Bandari ndogo ya Kemondo ili

kurahisisha uchukuzi katika ziwa na hii ni ku-*complement* kazi kubwa ambayo imefanya na Serikali ya kutujengea meli kubwa. Kama unavyojua meli kwa Kanda ya Ziwa, meli ni siasa na meli ni uchumi. Itasaidia akinamama ambao wanauza ndizi kutoka Bukoba kuzipeleka Mwanza na tutapata masoko na kufanya hivyo tutajenga uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ambayo imefanyika ya kujenga hizo bandari tunaishukuru Serikali, tunajua meli kubwa sasa itatia nanga Kemondo na Bukoba kama ilivyokuwa miaka ya nyuma tulikuwa tumeikosa hii. Ninaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inaongozwa na Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukamilisha hili jambo, ni jambo kubwa amejenga historia na ametuheshimisha kusema kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Bandari ndogo za Kyaukwikwi na Bandari ndogo ya Katebe Magarini, ninashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuja Magarini alipotembelea Wilaya ya Muleba na alitoa maelekezo. Ninaomba sasa maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Wilaya ya Muleba alielekeza *TPA* kwenda kujenga gati mpya ya Katebe Magarini. Maelekezo hayo hayajatendewa kazi, lakini ninajua watakuja na ninaomba kuanzia sasa tunapoongea hapa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoyatoa yakatekelezwe Magarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu na Bandari yetu ya Kyamkwikwi ambayo imechukuliwa na *TPA* ijengwe ili meli ndogo ambazo zilikuwa zinatoa huduma kabla ya kujenga meli kubwa sasa zikarahisishe usafiri na usafirishaji kupitia hizi Bandari ndogo za Kyamkwikwi na Katebe Magarini kwenda katika Visiwa vyetu vya Ikuza na Mazinga, Bumbile, Kerebe na Goziba ili ziwa lote sasa likapate usafiri wa haraka na usafiri wa bei nafuu; na tuweze kusafirisha mazao ya Ziwa letu la Victoria kutoka eneo moja kwenda eneo lingine kwa ajili ya kupata masoko ya dagaa na samaki wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali yetu, kwani kwa kipindi kirefu Wilaya ya Muleba hatukuwahi kuwa na hospitali ya

wilaya. Ni Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetutengea fedha kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Wilaya ya Muleba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesaini mkataba, na mkandarasi yupo *site*. Naiomba Wizara ya Fedha ikamlipe *advance payment* ili mkandarasi yule asitoke *site* na tupate Hospitali ya Wilaya ya Muleba, watu wetu wa Muleba wakatumie na wenyewe wakafurahie hospitali ya wilaya ambayo tumeikosa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye zao la kahawa. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, alikuja pale Kagera akatoa maelekezo na mwongozo ambao kusema kweli umewanufaisha na kuwafaidisha wakulima wa zao la kahawa Mkoa wa Kagera. Bei imepanda na wakulima wanafurahi na wanaishukuru Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto ndogo tunapoelekea msimu wa kahawa Kagera. Naiomba Serikali yangu sikivu, tunapokuja kwenye msimu wa kuvuna kahawa, tunapata changamoto ya watu wetu wanaovuna kahawa kutoka kwenye mashamba yao, wanakamatwa barabarani kwa kisingizio kwamba ni magendo. Hili jambo lilishatolewa kauli na Serikali. Hivyo basi, naomba katika bajeti hii Waziri wa Kilimo atoe maelekezo mahususi kuhusu masuala ya kahawa, wananchi wetu wanapotoka kuvuna kahawa kwenye mashamba yao wasibughudhiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya ndani kwa ndani nadhani siyo magendo. Biashara ya magendo ni pale ambapo tunavusha kahawa kutoka katika mipaka ya nchi yetu, huko tukashughulike nao; lakini ndani ya wilaya, ndani ya kata zetu, ndani ya tarafa zetu, naomba Bunge lako Tukufu likatoe kauli kabla wananchi hawajaanza kubughudhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani tena kwa upande wa miundombinu Mkoa wa Kagera. Tunaishukuru sana Serikali, kwani imetupa fedha nyingi za kujenga miundombinu katika

mkoa wetu na hususan Jimbo langu la Muleba Kusini. Barabara nyingi zimejengwa na zinapitika. Hata hivyo, bado nina kilio cha barabara yangu ya kutoka Muhutwe - Kamachumu - Buganguzi - Kishanda - Nshamba – Muleba ambayo ina urefu wa kilomita 56. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, imejenga kilomita zaidi ya 49, zimebaki kilomita saba. Naiomba Serikali, kwa kuwa ilishatoa *commitment* ya kumaliza hiyo Barabara, tukamalizie hicho kipande cha kilomita saba ili wananchi wa Muleba wakafurahie kutumia barabara ya lami ambayo ni ya Muhutwe - Kishanda, Muhutwe – Kamachumu - Buganguzi - Kishanda - Nshamba – Muleba, kilomita saba tu zimebaki. Najua kwetu wanasema, ukishakula mbuzi usishindwe kula mkia wake. Naomba tukamalizie na mkia uliobaki ili barabara hii ikapitike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali yangu, tumepata kwani fedha nyingi na ya heshima, tunajenga daraja la Kamishango katika Mto Ngono. Hili daraja ambalo lilikuwa limeshindikana kwa miaka mingi, ni kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita tumepewa fedha za kutosha na mkandarasi yupo *site*. Wananchi wa Muleba wanaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inaongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuonea hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanasema kura za Mama tunapokwenda kwenye Uchaguzi Mkuu zipo salama na hazina shaka yoyote. Pale, kazi iliyofanyika kila mmoja anaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwenye kilimo na uvuvi. Mkoa wa Kagera hususan Wilaya ya Muleba, tunapakana na Ziwa Victoria. Uchumi wetu umefungamanishwa na Ziwa Victoria, lakini tunayo matatizo makubwa sana ya uvuvi haramu ambao unatishia ustawi wa mazalia ya samaki kwenye Ziwa Victoria. Nashukuru wakati Serikali inaongelea kupumzisha ziwa, na ninashukuru nimeongea na Waziri wa Mifugo na Uvuvi leo, Ziwa Victoria halimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunaomba Serikali yetu sikivu tulishakuja na pendekezo hapa kuunda mamlaka ya uvuvi ambayo itasaidia kulinda mazingira ya Ziwa letu Victoria, kulinda mazalia ya Samaki, lakini kikubwa zaidi kupambana na uvuvi haramu. Hali ilivyo kwa sasa, hatuwezi tukalinda mazingira ya Ziwa Victoria tukapamba na uvuvi haramu kama hatuna chombo mahususi cha kupambana na hayo madhara ya uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara husika tunapokwenda kumalizia hii bajeti, ituambie hiyo mamlaka tunaiunda lini? Kwa sababu tumeliongelea hili jambo miaka zaidi ya mitatu. Hili jambo lina faida kubwa sana kwa uchumi wa nchi yetu hasa kwa mazao ya samaki na dagaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Victoria pale tunayo changamoto kubwa, na nimemwelezea Mheshimiwa Waziri, kwenye Ziwa Victoria tulikuja na taa za *solar* ambazo wavuvi wengi wanalalamikia kwa sababu zina athari kwa mazalia ya Samaki, lakini zina athari hata kwa wananchi ambao wapo nje ya ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali hii ikafanye utafiti, iangalie ni madhara gani yanasababisha hizi taa za *solar* na ikachukue hatua haraka sana iwezekanavyo ili kunusuru mazalia ya samaki na kunusuru afya za watu wetu hasa wanaoishi ukingoni mwa Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hiyo hiyo ukiangalia umiliki wetu wa Ziwa Victoria, tunamiliki zaidi ya 51%, wenzetu Uganda 43%, nadhani, wenzetu Kenya asilimia sita; lakini ukiangalia faida tunayoipata, na hii nilishawahi kuichangia hapa Bungeni. Wenye asilimia ndogo wana viwanda vingi vya samaki kuliko sisi wenye asilimia kubwa. Hili jambo halikutokea tu kwa sababu ya miujiza au ya nini, inatokana na mfumo wetu wa tozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliomba Bunge letu Tukufu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wakaangalie tozo tunazotoza. Tunang'ang'ania vitu vidogo vya tozo tozo, lakini watu

wanakimbia eneo letu kuwekeza viwanda, wanakwenda kuwekeza nchi jirani na tunapoteza ajira, tunapoteza kodi, tunapoteza mali kabisa, kwa sababu ya vitozo vidogo vidogo. Unang'ang'ania shilingi 20,000 unapoteza shilingi 1,000,000. Hii haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara, Serikali ikafanye tathmini *(due diligence)* wakaangalie kwa nini, viwanda vinakimbilia nchi za jirani? Ukiwa ziwani mle hakuna *traffic,* wala hakuna nini. Biashara zinafanyika humo ziwani kwa sababu sisi tozo zetu zipo juu, na nchi jirani zipo chini, wanakimbilia kule wanauza hata samaki kule. Badala ya kujenga viwanda hapa, sisi tutabaki tu na maji tunayaangalia, wenzetu wanatengeneza fedha huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi, na kwa kuwa hili jambo kwa kiwango fulani lipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tukaliangalie, tukarekebishe tozo ili tuvutie viwanda wakawekeze kwetu, tukaajiri vijana wetu, na pia tukapate kodi kutokana na viwanda vitakavyojengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naishukuru Serikali yangu kwa minara mingi ya mawasiliano kwenye jimbo langu, sasa kuna usikivu wa simu. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Salome Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Tecla Ungele, na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, ajiandae.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye hotuba hii muhimu kwenye bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kusema, nilikuwa nimejipanga kuchangia siku ya jana na Mheshimiwa Naibu Spika aliposema twende tukatafakari bajeti hii, akawa amenivuruga kidogo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyofika nyumbani baada ya kusoma kwa kina hotuba hii yenye kurasa 103 ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametumia saa mbili kuisoma nilielewa kwa nini Mheshimiwa Naibu Spika alisema turudi nyumbani tukatafakari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwa makini hotuba hii, na kwa uzoefu mdogo nilionao wa kukaa ndani ya Bunge hili kwa miaka 10, nimejifunza jambo moja kubwa sana. Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na kwamba tunamsifia ndani ya Bunge hili, kuna kazi kubwa sana ambayo ni mtihani mkubwa, labda pengine wengi wetu tusingeweza kufaulu kama tungepewa ambao mama huyu alifaulu kuufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mataifa mengi yanapokuwa yamemaliza uchaguzi, au yanapobadilisha utawala, moja kati ya changamoto kubwa ambayo yanapata Mataifa hayo ni namna ya kuendeleza miradi au mipango ya mtangulizi aliyetoka madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ukarejea hotuba mbalimbali kwa miaka mitano, sita, kumi iliyopita, unaona namna ambavyo Mheshimiwa Rais ameonesha siyo tu dhamira ya dhati, lakini ameonesha *commitment* ya hali ya juu kuhakikisha kwamba mipango ya watangulizi wake inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuonesha *commitment* hiyo kabla, sijaanza kutaja mipango hiyo. Mama huyu ametupa dira kwa kusema kwamba na isitokee tena ndani ya nchi utawala ukibadilika mipango inabadilika. Akaamua kutengeneza Wizara maalumu, Wizara ya Mipango, akatengeneza Tume Maalumu ya Mipango akamweka Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na mjomba wangu pale Mheshimiwa Nyongo, wasimamie Wizara ile kuhakikisha mipango ya nchi hii inayopangwa kwa miaka 25, miaka 50 itatekelezwa pamoja na kubadilika nyakati mbalimbali za mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu na upande wa nishati, lile Bwawa la *Stiegler's,* mipango yake ilianza kufanyika tangu miaka ya 1960. Watangulizi wake walihangaika kutekeleza wakahangaika na kuhangaika, lakini hivi tunavyozungumza leo mitambo yote imeshawashwa chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, *turbine* zote zimewaka, vijiji vyote 10,000 na kitu vimewashiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya hayatokei hivi hivi, ni lazima uwe na kiongozi ambaye anasimamia shughuli hizi zitekelezwe, sio mwingine, ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, mambo haya hayatokei kama muujiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Wizara ya Kilimo, kama, ulikuwa humu Bungeni tunaongelea bajeti ya shilingi bilioni 200, leo tunaongelea *1.3 trillion*. Kaka yangu Mheshimiwa Bashe, anasimamia, Mheshimiwa Waziri Mkuu anakimbizana nao kila siku, anaangalia namna ambavyo miradi inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya uongozi wa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, leo sisi Tanzania tunajivunia tumeagiza ndege kwa maana ya *(Aeroplane)* ya kuua ndege wale waharibifu, ya kupulizia dawa. Haya mambo hayatokei hivi hivi, ni lazima uwe na viongozi makini kusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa ukurasa wa sitini na ngapi? Anasema kwenye Wizara ya Maji, ndani ya mwaka mmoja visima vya maji 925 wastani kila jimbo moja la uchaguzi limepata visima vitano. Hivi mimi ni nani leo nishindwe kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ni nani kama nitakuwa sina uchungu na nchi hii? Akina mama wametuliwa ndoo kichwani. Nami Salome nilikuwa pale Shinyanga, tunatembea kilomita 13 kufuata maji ya kunywa na ya kutumia. Leo angalau kila Jimbo limechimbiwa kisima ndani ya mwaka mmoja, tena siyo kimoja.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, anafanya kazi kubwa, anasimamia Serikali, anatusimamia na kazi inaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwetu Shinyanga Ibadakuli, ule uwanja wa ndege ilikuwa ni *nightmare,* ilikuwa ni ndoto. Kamati ya Bunge imeenda kukagua juzi uwanja, unakaribia kukamilika, ndege zitatua pale. Serikali inafanya kazi. Leo unatenganishaje demokrasia tuliyonayo na maendeleo makubwa na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali iliyopo madarakani? Nitakuwa ni mtu ambaye sina shukurani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaibuka mtu mmoja tu leo, unajua, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu; hii nchi tumeanza uchaguzi wa vyama vingi mwaka 1992 na mwaka 1995 tulikuwa na Wabunge wa Upinzani 51, mwaka 2000 tulikuwa na Wabunge wa Upinzani 26, wakati huo Mheshimiwa Mbowe ndio aligombea Urais; mwaka 2005, tulikuwa na Wabunge wa Upinzani 41, mwaka 2010 tulikuwa na Wabunge wa Upinzani 89, mwaka 2015 tulikuwa na Wabunge wa Upinzani 116 na 2020 tupo Wabunge 28 wa Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu aliyesema hashiriki uchaguzi mpaka tufanye mabadiliko ya sheria. Kwenye chaguzi zote, hakuna mtu aliyethubutu kusema hivyo, hakuna mtu aliyesema tuingie barabarani tufanye uasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna mtu mmoja aliyekuwa na tamaa ya Urais, ameukosa kwa sababu anajua Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya kazi, anataka kumwaga mboga, anataka kumwaga ugali, na maji ya kunawa. Hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukubali. Ukweli ni kwamba, kwa namna ambavyo mazingira ya uchaguzi yamewekwa, kwa namna ambavyo wameruhusiwa kufanya mikutano ya hadhara, kwa namna ambavyo wametumia vibaya nafasi yao ya kufanya haki ya demokrasia, wamegundua kwamba wakishiriki uchaguzi huu, hawapenyi, ndiyo maana wameweka mpira kwapani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka yote awamu zote sita ambazo tumeshiriki uchaguzi kwenye hii nchi, CCM ni ile ile, Katiba ya nchi ni ile ile. Tume ya Uchaguzi imeboreshwa mwaka jana 2024, wanaweka mpira kwapani, hii haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, unaweza kusema yote kwenye hii nchi, lakini mimi Salome Makamba ni Msukuma wa Shinyanga, sina pa kwenda. *Passport* ya kusafiria kwenda nje nchi, nimepewa na Bunge. Sina pa kwenda, mama yangu, na familia yangu haina pa kwenda. Hatuwezi kuhamasisha uasi kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kung'ang'ania kitu kisichowezekana, kung'ang'ania kwamba hatuwezi kufanya uchaguzi, imebaki miezi mitatu twende kwenye uchaguzi; unang'ang'ania hatuwezi, na mtu ni Mwanasheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua humu ndani kwamba utaratibu wa utungaji wa sheria, na utaratibu wa kurejea sheria una namna yake ambayo unahitaji muda. Ni lazima tu-*table* mara ya kwanza, ni lazima tu-*table* mara ya pili, ni lazima watu watoe maoni, na ni lazima wananchi watoe maoni. Huo mchakato unahitajika. Mtu, ametia mpira kwapani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wale wanaojiita sijui *G55,* sijui nani? Mimi naenda kugombea, na nitarudi humu Bungeni. Nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimeona wameongeza bajeti. Baba ongeza mpunga, leta *ballot paper,* leta maboksi, sisi tupo tayari kwa uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mtu mmoja awe ndio anaamua kwamba hii nchi leo iwe Jumapili, kesho iwe Jumatatu, anaongea yeye, mwanaume yeye, kibaunsa yeye. Hatuwezi kukubali. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie kitu kimoja, mimi Mheshimiwa Salome na wananchi wa Shinyanga hasa akina mama tunasema hivi, yote yametekelezwa. Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia mitano tena, Mama Samia mitano tena, tumeyasubiri

maboksi ya kura kwa muda mrefu, kwa ajili ya kuhakikisha tunapiga kura. Tunamvika huyu Mama nguo, tunamfuta machozi kwa kazi kubwa aliyoifanya, na kutukanwa kwa ajili yetu sisi wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walisema yote, mara ameuza bandari, mara sijui mama amefanya hivi. Sasa hivi wameishia kusema Mama akifungua pochi mambo yanatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo Kamati ya TAMISEMI, kwa mara ya kwanza kwenye nchi hii, nimeshuhudia kwa macho yangu jengo la mama na mtoto. Mimi nina Watoto. Jengo la mama na mtoto, yaani ukishindwa kujifungua kawaida, chumba kinachofuata unaweza ukafanyiwa *operation;* chumba kinachofuata kama mtoto wako ni njiti, unaweza kumweka kwenye chumba cha watoto njiti; chumba kinachofuata kama umefanyiwa *operation,* unaweza kupumzishwa pale. Haya mambo tuliyaona lini haya? Hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Ulinzi na Usalama lipo. Kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa, Waziri wa Mambo ya Ndani upo, tekelezeni wajibu wenu. Hii nchi ni ya demokrasia. Kuzuia uchaguzi ni uhaini na hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie tu ukweli, huyu jamaa anataka kutupiga changa la macho. Chama chochote cha siasa lengo lake namba moja, ni kushika dola. Hilo ni lengo lake namba moja. Sisi hatufanyi kazi ya uharakati hapa. Najua siasa ni kushika dola. Haiwezekani hata siku moja, wamekaa nje huko, leo watu waendelee kukaa nje huko, hatuna kambi rasmi ya upinzani, hatuwezi kurudi Bungeni kama Waheshimiwa Wabunge, halafu unasema sisi ni wanasiasa. Hapana, ni lazima tushike dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliopo nje ninaungana nao. Ni lazima turudi humu ndani kama tulivyokuwa zamani. Lazima tukae humu ndani kama tulivyokuwa zamani. Serikali ishauriwe, ipokee ushauri; nasi tushauriwe, tupokee

ushauri, tulijenge Taifa moja kwa umoja. Hiyo ndiyo kazi ya chama cha siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, uwakilishi wa wananchi, huwezi kuwakilisha huko kwenye majukwaa, na ndiyo maana unaona huko wanapofanya haina tija. Ni lazima tukae kwenye mabaraza ya vijiji, ni lazima tukae kwenye Baraza la Madiwani, ni lazima tukae Bungeni ili tuweze kuishauri Serikali kwa mfumo unaoeleweka. Huwezi kuishauri Serikali nje ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, rai yangu, tunataka uchaguzi, na tupo tayari kushiriki uchaguzi. Hatupo tayari kuungana na mtu ambaye anataka kupindua nchi hii na kuleta uhaini. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, wapi? Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri sana wa Mheshimiwa Mbunge, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema, uhuru bila demokrasia ni udikteta; lakini demokrasia bila ya nidhamu ni fujo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoendelea hivi sasa ni sheria kuzingatiwa kwenye kuweka mipango ya kuwapa Watanzania fursa ya kutumia haki yao ya kuchagua. Ni dhahiri kabisa kwamba Mheshimiwa Mbunge alichokizungumza hapa, ameonyesha kabisa kama Yesu Kristo alivyosema, atakayenionea haya mbele za watu, nami nitamwonea haya mbele za baba yangu. Hakujali itikadi, hakujali jambo lolote, amemsifia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na rekodi iliyotukuka, aliyoionyesha. Dunia inajua, Tanzania inajua na wapinzani wanajua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Salome Makamba unapokea taarifa?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hiyo taarifa naipokea. Kazi namba moja ya chama cha siasa ni kushika dola. Huwezi kushika dola kwa kwenda kwenye vyombo vya Habari, wala huwezi kushika dola kwa kwenda kwenye mikutano kuwaambia watu wafanye uasi na uhaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unashika dola kwa kushiriki chaguzi huru na za haki. Unashika dola kwa kuhamasisha watu waende kupiga kura. Unashika dola kwa kuwa na ushawishi kwa vyombo vinavyotoa maamuzi ndani ya nchi hii, na kwa kufanya hivyo ndiyo njia sahihi ya kueleza yale ambayo unatamani yafanyike ndani ya nchi yako. Tofauti na hapo ni kinyume na Katiba, ni uasi na ni uhaini kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome Makamba kwa mchango wako wa kizalendo kabisa. Nimwite sasa Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani, na Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunipatia uzima na afya njema. Nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ya maendeleo iliyofanyika ndani ya nchi hii. Kila mtu anaendelea kushuhudia sehemu zote pande nne za nchi hii na dunia pia inashuhudia.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaomba utulivu kidogo. Mheshimiwa Ungele endelea.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia miradi hiyo mingi kama vile *SGR* na mingine. Sasa hivi usafiri kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam ni rahisi tu. Hata wenye changamoto ya miili, ni shida kwenye mabasi, lakini

tunakwenda na *SGR*. Hiyo ndiyo kazi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Lindi, tuna miradi mingi ya maendeleo, amefanya miradi mingi sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na inaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Sekta ya Afya. Katika wakati wote nilivyoendelea kutoa huduma za afya, sijapata kushuhudia kuona huduma za *ICU* zikiwepo kwenye ngazi ya Wilaya pamoja na wagonjwa wa dharura ndani ya wilaya, lakini kwa mikoa ya Lindi na kwingineko, hospitali za wilaya kumejengwa huduma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye elimu kuna madarasa na kila kitu. Sasa hivi inajengwa shule kubwa ya wavulana ya sekondari pale Kiwalala kwenye Wilaya ya Lindi Vijijini kwa ajili ya mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi inayoenda kugharimu shilingi bilioni 4.1. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha hizo. Jambo hili hatujapata kulishuhudia, ndiyo sasa tunayaona mambo haya katika kipindi chake cha Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, sisi Wanalindi na Mtwara tumeshuhudia bei nzuri ya mazao ya biashara kama vile korosho, ufuta na mbaazi, na kila mmoja anashuhudia. Hapa ninapozungumza, kila mmoja anayesikiliza huko Lindi na Mtwara wanashuhudia na wanakubali jinsi alivyofanya mambo makubwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hakuna leo atakayekuja akatudanganya danganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapita huko, lakini hakuna lolote. Wengine wanakwenda kushangaa tu kwamba kumbe huyu ndiyo bwana huyu! Lakini siyo kwamba wanasikiliza yale wanayoyasema. Hakika mambo mazuri yanaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa kwa jinsi alivyowasilisha

hotuba yake jana kwa umahiri na umakini mkubwa sana. Masaa mawili tangu mwanzo mpaka mwisho, *tone* ya sauti ni ile ile na kutamka ni vilevile yaani mpaka mwisho, kiasi kwamba kila sehemu alikuwa anaendelea kusisitiza, kila *point* mpaka amemaliza nukta yake ya mwisho. Kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyomsaidia Mheshimiwa Rais kwa namna kubwa sana. Nguvu zake na akili zake zote anamsaidia Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kujenga nchi hii. Hii inajidhihirisha vile Mheshimiwa Waziri Mkuu anavyopita kwenye mikoa, kwenye wilaya, na kwenye halmashauri zetu. Waheshimiwa Wabunge hapa tangu asubuhi walipoanza kuchangia imedhihirisha kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu zote zile zinazoonekana kuna shida, kuna changamoto au kuna kadhia fulani, akishaenda Mheshimiwa Waziri Mkuu pale kama ulivyosikia, hajali mvua, hajali jua kali, atasimama hapo juani, atasimama hapo kwenye mvua lakini yupo na wananchi. Hakika hatujapata kushuhudia mtu kama huyu. Tunaomba tuendelee kumwombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa, humu ndani Wabunge wenzangu tutaendelea kumwombea Mheshimiwa Waziri Mkuu aendelee kuimarika na pia tunamwombea Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aendelee kumwamini kijana wake huyu, kwani ni msaada mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wizara ambayo ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, kuna kijana wake ambaye ni Waziri ambaye ni Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete akisaidiwa na Mheshimiwa Patrobass Katambi. Vijana hawa ni wanasheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo kwenye Kamati ile ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambayo tunasimamia Wizara hiyo. Vijana hawa pamoja na Katibu Mkuu, Maganga na Watendaji

wao wote ni watu mahiri, na ni watu wapo imara wanaosimamia kazi yao ambayo wamekabidhiwa. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hiyo hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, kuna taasisi hizi za hifadhi ya jamii; *NSSF, PSSSF, WCF, OSHA* na *CMA*. Taasisi hizi wamekuja hawa watendaji na ubunifu mkubwa kweli. Sasa hivi huduma zao wanaendesha kidijiti. Pia, kwenye uwekezaji, wanafanya uwekezaji mwingi kwenye mambo ya ujenzi. Tunawapongeza kwa sababu ni uwekezaji wenye tija, unaoenda kuhakikisha kwamba mwisho wa siku mafao ya wastaafu wetu yatatolewa katika uhalali wake na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye changamoto tulizonazo, kuna changamoto ya barabara hii ya Kibiti - Lindi. Barabara hii ni ya muda mrefu sana, tunakubaliana humu ndani na kama kuna wasiofahamu, basi wanaweza wakaendelea kurejea *Hansard* ya Bunge zilizopita kwa miaka iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, b,arabara hii pia ipo pembezoni mwa Bahari. Tangu inaanza Dar es Salaam mpaka inapofika Mtwara ni pembezoni mwa Bahari wa Hindi. Ni kilomita chache tu kutoka bahari ya Hindi, ndiyo barabara hii ilikopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini sasa kinachoendelea? Kwa kuwa barabara hii ipo pembezoni mwa bahari ya Hindi, kwa hiyo ardhi yake ipo na unyevunyevu. Mito yote inayotoka huko milimani kwenye hifadhi ya Selous, kwenye milima ya Matumbi, kwenye Wilaya hizo za Ruangwa, Nachingwea, kote huko inazoa inapeleka baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, barabara hiyo ni laini sana kiasi kwamba mvua kidogo tu ikinyesha basi barabara ile inaweza ikabomoka, na ndicho kilichotokea mwaka jana 2024 kwenye ile mvua kubwa na kile kimbunga cha Hidaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishuhudia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyafanya mambo makubwa, akatoa fedha za dharura na kazi ile ikafanyika mwaka jana, 2024. Hata hivyo,

ilifanyika kwa muda tu ili isaidie wale watu kwa muda. Mwaka huu pia imejirudia tena, mvua kubwa imenyesha na barabara imebomoka tena na madaraja yamezolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sisi Wanalindi hatuna mashaka, hatuna wasiwasi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na hatuna mashaka na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ambaye anasimamia shughuli za Serikali ndani ya Bunge hili. Kwa kuwa anamsaidia sana Mheshimiwa Rais, kazi hii Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kuimaliza. Sisi Wanalindi tuna imani sana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anaenda kuijenga hii barabara upya tena kuanzia Kibiti mpaka Lindi, mpaka Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna imani sana na ndiyo maana sisi Lindi tunasema, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mitano tena. Tunaamini kabisa hata kama ikiwa namna gani, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hatashindwa. Hatashindwa ile barabara ya kutoka Kibiti - Lindi - Mtwara, kuijenga upya kwa sababu ameyafanya mambo makubwa ndani ya nchi hii na anaendelea kuyafanya mambo makubwa ya maendeleo ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Naomba kwa asilimia zote bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu ipite kwa asilimia zote, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ungele. Nimwite sasa Mheshimiwa Aida Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, na Mheshimiwa Neema Mwandabila ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema aliyenijalia uzima kusimama tena kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Nkasi Kaskazini kwa ushirikiano mkubwa

ambao wamekuwa wananipatia, na imani kubwa waliyoijenga kwangu kuwa mwanamke wa kwanza katika historia ya nchi yetu na Mkoa wetu wa Rukwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini. Imani hiyo nimeilinda na nitaendelea kuilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara aliyoifanya kwenye Mkoa wetu na Jimbo langu. Ziara zote ambazo amekuwa anazifanya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni ziara zenye tija, zenye maagizo na unaona faida ya ziara anazokuwa anazifanya. Kwa hiyo, upande wa kumsaidia Mheshimiwa Rais, naye kama Mtendaji Mkuu wa Serikali, kiukweli viatu hivyo vimemtosha, amevitendea haki, na ameitendea haki nafasi hiyo. Pamoja na mema mengi ambayo yalifanyika kwenye ziara yake, nina mambo machache ya kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kwenye kushauri, jana Mheshimiwa Mwenyekiti wa CHADEMA, Mheshimiwa Tundu Antipas Mugwai Lissu, amekamatwa Ruvuma. Tungependa Serikali, kwa kuwa yule ni Kiongozi Mkuu wa Chama Kikuu cha Upinzani, taarifa za kukamatwa kwake na sababu ziwekwe hadharani Watanzania wazijue, na haki itendeke kama Mtanzania mwingine.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa mdogo wangu Mheshimiwa Khenani, Mbunge wa Nkasi. Kwa kweli ingekuwa mimi katika nafasi yake, nisingesimama kumsemea kiongozi asiye na heshima kama yule. Nisingethubutu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi huyo anayemwita yeye ni kiongozi, mimi nimemshangaa. Yaani badala ya kuongea na

wananchi mambo ya msingi, ameenda kupeleka matusi na kuwadharau wananchi wa Nyasa kwa kuwasemea matusi ya viongozi wao. Akome, akome, akome kabisa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani umepokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Manyanya?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tu mama yangu, nimelelewa, nimefundishwa, yule ni mama yangu na amekuwa Mkuu wangu wa Mkoa wa Rukwa. Ni wajibu wangu kama Mbunge, na nimesimama kuiambia Serikali, haki itatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini historia ya nchi yetu itaendelea kujengwa kwa amani na utulivu. Kama kuna kosa limefanyika, liwekwe hadharani na sababu za kukamatwa. Naomba niendelee.

**MWENYEKITI:** Endelea na mchango wako.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengi yaliyofanyika na Serikali, nina ushauri kwenye mambo kadhaa. Jambo la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 2024 na mwaka 2023 tumezungumza juu ya usafiri wa Ziwa Tanganyika. Tumelisema kwa kina, kwenye vitabu tunasoma kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika uwekezaji ambao Serikali imeweka kwenye bandari hakukuwa na sababu leo tuzungumzie ukosefu wa usafiri wa uhakika wa Ziwa Tanganyika. Tunawezaje kuwekeza Bandari ya Kabwe, Bandari ya Kasanga, Bandari ya Kipili, Bandari ya Kalema halafu usafiri haupo kwenye Ziwa Tanganyika? Tulitaka ku-*achieve* nini kwenye hizo fedha tulizowekeza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. MV Liemba ni meli ambayo imeharibika muda mrefu sana, MV Mwongozo, sababu zake ukiziona, hakukuwa na sababu ya kukaa zaidi ya miaka nane. Leo tulitegemea wananchi

wa Mkoa wa Rukwa kwenye hotuba yake ambayo inatoa mwelekeo wa nchi tujue, sisi Wanarukwa ambao tunaamini uchumi wetu unatokana na mazao tunayolima ikiwemo mpunga na mahindi, na watu wa Kongo wanategemea mazao kutoka Tanzania, tunasafirisha kwa njia gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye hili eneo kumekuwa na changamoto kubwa. Kila siku tunapoteza ndugu zetu kwa usafiri usiokuwa rasmi. Tunawezaje kupeleka meli mpya, iwe ni mbili au tatu kwenye ziwa moja, wakati Ziwa Tanganyika ambalo tungewekeza kwa kina ingesaidia uchumi wa mkoa na uchumi wa Taifa? Leo kutueleza habari tu ya ukarabati, na kuchukua muda wote huu Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaamini Wanarukwa hatujatendewa haki. Tumechoka kulia juu ya wananchi wetu kupoteza maisha kwa sababu ya biashara wanazozifanya kwa usafiri wanaotumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani kwenye hitimisho lake mtoa hoja, atueleze Wanarukwa, Kigoma na Katavi hatima ya usafiri wa uhakika wa Ziwa Tanganyika, Ni lini tutapata meli mpya? Meli hizo za ukarabati tu, ni lini zitakamilika ili tuweze kuinua uchumi wetu wa Mkoa wa Rukwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la uanzishwaji wa mamlaka za kiutawala. Hili jambo limekuwa kama *favor* hivi, lakini lipo kwa mujibu wa sheria, na nimelisema leo wakati nauliza swali. Nimesema hivi, Tume kutoka TAMISEMI 2013 ilifika Nkasi, wakaangalia vile vigezo vyao vyote 13, wakasema tumekidhi vigezo. Ni nini kinatokea leo mpaka nazungumza mara kadhaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namanyere upande wa *TANESCO,* badala ya kulipa shilingi 27,000/= wameingizwa kwenye kulipa shilingi 320,000/=. Kwa nini? *TANESCO* wanatumia Sheria ya Mipango Miji. Kwa hiyo, huku wanahukumiwa wakati mmeshindwa kutimiza wajibu wenu. Kwa nini tunawatia kwenye maisha magumu bila sababu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema, kama tunasema bado tunaendeleza yale maeneo tuliyoanzisha huko nyuma, tufute kwanza hizi mamlaka mpaka tutakapojiandaa, wasiendelee kuhukumiwa kwenye hili jambo. Ukiwaangalia maisha yao ni ya kawaida, lakini *TANESCO* wanatumia Sheria ya Mipango Miji; na hili eneo siyo kwa Namanyere tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, nilishapeleka mpaka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu *document* ikiwa imekamilika. Tume walizoziandaa, zimekwenda kule, kama hatujaamua leo kutoa halmashauri ya Mji wa Namanyere tukafute ile Mamlaka ya Mji Mdogo, waendelee kuishi kama zamani ili tuache kuimba huu wimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza haya, pamoja na kwamba lipo kisheria, nakubaliana kwamba kuna maeneo ambayo lazima waendeleze hayo majukumu mengine ya kimaendeleo. Sasa kama ndivyo, kipaumbele chetu kama Taifa ni nini? Hebu wewe fikiri, Mkoa wa Rukwa toka mwaka 1984, kaangalieni Halmashauri ziko ngapi? Mbona wengine wana Halmashauri nyingi, halafu Rukwa ni chache! Mikoa mingine mnaionaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kuanzisha hizi mamlaka ni kupeleka huduma kwa Watanzania. Sasa kama kuna shida imejitokeza hivi karibuni, kwanza ile sheria yenyewe tuibadilishe ili tujue kwamba sasa hivi kuongeza maeneo ya kiutawala ni *favor* au mtu aamue tu kwamba inakaaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, natambua jitihada za Serikali upande wa kilimo, na eneo hili limefanya vizuri sana kwa kuongeza bajeti, lakini hata utendaji wake. Leo wakulima wameongeza tija sasa ya kilimo chao baada ya kuweka ruzuku kwenye mbolea. Nataka kushauri jambo moja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024 wakati Mheshimiwa Rais amekuja kwenye Jimbo langu, akasimamia kama kiongozi wa nchi na kusikiliza kilio cha wananchi. Nikamweleza juu ya changamoto ya bei, aliongeza bei pale, sasa hatuwezi kuwa

tunasubiri mpaka aje kiongozi ndiyo tuzungumze changamoto ya bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua kila mwaka lazima twende kwake kumwambia kuna changamoto ya bei ya mahindi. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anafanya kazi nzuri, mbolea imekwenda, watu wamezalisha. Tunachotaka, ni uhakika wa masoko ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaenda kwenye msimu wa mavuno, mvua zinaendelea, kwa hiyo, mazao yataharibikia shambani. Ni wajibu wa Serikali kuona ni kwa namna gani inakwenda kumkomboa mkulima kama ilivyodhamiria kwa kuweka ruzuku kwenye mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo naweza kulishauri ni kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kwa sababu anamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwenye eneo hili, hiki ni kipindi ambacho wakulima wengi wanatamani kutoka kuwa wakulima wadogo kwenda kuwa wakulima wa kati au wakulima wakubwa. Serikali iangalie namna ya kuwakopesha hizi mbolea waje walipe kulingana na kilimo ambacho wanakipata, wasikose haki ya kupata mbolea kwa sababu hawana fedha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha.

**MHE. AIDA J. KHENAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa muda ulionipatia. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida. Namwita sasa Mheshimiwa Hamida Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mtemvu.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nami naendelea kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwanza kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kwa kuwasilisha hotuba yake nzuri yenye kurasa zaidi ya 100 hapa Bungeni. Ni hotuba ambayo imesheheni mambo mbalimbali ya maendeleo katika nchi yetu. Nampongeza na kumtakia kila la heri katika majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kila Mheshimiwa Mbunge aliyesimama hapa Bungeni, ameendelea kumpongeza kwa uwajibikaji wake katika Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi ndugu zake, wananchi wa Lindi tunapata faraja sana kwa kutuheshimisha katika uwajibikaji wake katika shughuli zake za Serikali. Tunaendelea kumwombea kila la heri, Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda na ampe baraka. Pia, wananchi wa Ruangwa na wananchi wa Lindi wote tuna imani kubwa naye na tumesema hatuna mbadala mwingine zaidi yake. Kila la heri na Mwenyezi Mungu aendelee kumwongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, yale yote ambayo yameelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mambo ambayo Mheshimiwa Rais wetu ameendelea kupambana, kuhakikisha kwamba ni lazima alete maendeleo na mapinduzi ya kweli katika nchi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, ni mwanamke pekee Tanzania ambaye hatuna mfano wake. Tuendelee kumtakia heri na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ili aendelee kumwongoza kuhakikisha kwamba anaendelea kutimiza majukumu yake yake ambayo amedhamiria kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba katika maendeleo makubwa ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyaelezea katika hotuba yake, nasi tumefaidika nayo, kwa sababu tulikuwa kwenye giza kubwa, lakini leo Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametutoa kwenye giza na ametuweka kwenye mwanga na sasa tunasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, wiki moja iliyopita Mheshimiwa Tundu Lissu alikuja Lindi Mjini, lakini mapokezi yake yeye mwenyewe ameyaona kwa macho, na amewaambia wananchi wa Lindi kwamba, najua kwamba mna misimamo yenu, nasi tunasema tuna misimamo yetu. Lindi ni ya Samia na tunakwenda na Samia 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri ambayo yametekelezwa kwenye kipindi cha miaka minne cha Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia, yako mazuri ambayo yametekelezwa katika Jimbo letu la Lindi Mjini. Kabla ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia, hatukuwa na Hospitali ya Wilaya ya Lindi; na tangu uhuru upatikane, Lindi Mjini hapakuwa na Hospitali ya Wilaya, lakini leo tunavyozungumza, Lindi Mjini tuna Hospitali ya Wilaya na tumeanza kutoa tiba kwa sababu Mheshimiwa Rais ametupa mapenzi makubwa na kujali afya za Wanalindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, yako mambo mbalimbali yaliyotekelezwa. Hatukuwa na shule za sekondari za kutosha, lakini leo tunapoongea, Jimbo la Lindi Mjini tuna shule tano mpya za sekondari. Tunahakikisha kwamba watoto wetu wote hakuna anayekosa kwenda shuleni kwa kukosa darasa la kusomea. Kwa hiyo, tumepiga hatua kubwa katika kipindi cha miaka minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tunazo changamoto mbalimbali. Ukiangalia upande wa Sekta ya Maji, tunayo miradi ambayo haijakamilika. Tunataka wananchi wa Lindi waendelee kufaidika na rasilimali ya maji kwa kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa Maji, amepiga hatua kubwa sana kuhakikisha kwamba amesimamia utekelezaji wa miradi ya maji Lindi, ili wananchi waweze kupata maji safi na salama, lakini bado tuna huduma mbalimbali ambazo tunazihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa maji wa Mkundi ambao unagharimu shilingi milioni 326. Nikisema Mkundi, Mheshimiwa Jumaa Aweso anajua, ni upande wa pili wa bahari, wananchi wanahitaji mradi huu wa maji uweze kukamilika. Kwa hiyo, tunaomba tukamilishiwe hizi shilingi milioni 326 ili tukamalize mradi wa maji ili wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunao mradi wa Angaza ambao unahudumia pale katikati ya mji, tunahitaji shilingi milioni 172 ili tumalizie. Mkandarasi amesimama anashindwa kukamilisha mradi huu. Kwa hiyo, tunajua kwamba Serikali imewekeza nguvu kubwa ya kuleta fedha nyingi ili kutekeleza miradi ya maji, lakini bado nguvu hii kubwa haionekani kwa sababu wananchi wengi hawajaunganishiwa maji nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Jumaa Aweso akamilishe ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutupatia shilingi milioni 500 kwa sababu alizungumza mbele ya wananchi ili tusogeze miundombinu ya maji na wananchi waweze kuvuta maji majumbani mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu wa Lindi unategemea uboreshaji mkubwa wa Barabara. Tunajua kwamba Lindi tuliathirika sana na mvua za mwaka uliopita. Kimbunga Hidaya kilituathiri kwa kiasi kikubwa sana na tumechelewa kurekebisha miundombinu kwa kukosa fedha kwa wakati. Ninaiomba sana Serikali kuhakikisha kwamba wanatuletea fedha kwa haraka ili tuweze kuboresha barabara zetu na tuweze kuendelea kufanya kazi, na pia wafanyabiashara na wakulima waweze kuendelea kutumia barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba barabara ya Kibiti – Lindi imepata changamoto. Wiki hii kumetokea mafuriko makubwa, lakini ukiangalia uharibifu uliotokea ni mkubwa sana. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Ulega, ameendelea kuwepo katika eneo kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kupata huduma ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi aangalie Daraja la Mbwemkuru, daraja lile linaliwa kwa kasi kubwa kwenye kingo za barabara kunakoshikilia daraja. Mto ule umeendelea kupanuka na maji yanakula barabara kwa kasi kubwa sana. Sasa tusipokwenda kuchukua hatua kwa haraka, maana yake daraja lile linakwenda kuvunjika, litazama na juhudi zote zinazofanywa na Serikali hazitasaidia kwa sababu daraja lile ni kubwa na likikatika maana yake mawasiliano yanakatika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi ahakikishe kwamba anakwenda kusimamia kwa haraka kutafuta dawa ya haraka na kuweza kunusuru daraja lile lisiweze kuporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaishi kwenye ukanda wa bahari na tunajua kwamba katika bahari yetu kumetokea uharibifu mkubwa wa mazingira, ardhi yetu inaendelea kuliwa kwa kasi kubwa sana, lakini nimeizungumza hoja hii karibu mara tatu hapa Bungeni. Mheshimiwa Waziri Mkuu alishatoa maagizo kumwagiza Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuja kutazama ili kuona ni kwa namna gani wanaweza kutusaidia kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ihakikishe wanakuja Lindi kuangalia ili kuwanusuru Wanalindi na bahari ile isiendelee kula nchi kavu ili kuhakikisha kwamba mji wetu unanusurika. Tusipochukua hatua kwa haraka, maana yake changamoto kubwa itakuja kutokea mbele ya safari. Tuna kilomita 570 zinazohitaji kufanyiwa ukarabati kwa haraka ili kunusuru mazingira ya bahari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo yote mazuri yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, bado katika Mji wetu wa Lindi ukiangalia jiografia ya Mji wa Lindi ni miteremko na vilima, lakini udongo wake ni wa mfinyanzi. Kwa hiyo, katika upande wa *TARURA*, tunashukuru kwamba Serikali inatupatia fedha kila mwaka shilingi bilioni 3.6, lakini kutokana na mazingira na changamoto kubwa iliyopo, tunahitaji kuongezewa fedha hizi

tuweze kuboresha barabara zetu ili ziwe kwenye ubora unaostahili ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Lindi wanaendelea kutumia barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo tunaletewa, tunashindwa kutengeneza hata kilomita mbili za lami, ni fedha kidogo, lakini ukiangalia mtandao wa barabara ni kilomita 564. Barabara ambazo zina lami hazizidi hata kilomita 200. Kwa hiyo, bado tuna changamoto kubwa ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwekeza ili kuboresha barabara zetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza, nami nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Ardhi anayeendelea kutujaalia afya pamoja na uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kufanya majukumu yake ambayo wananchi wa Tanzania pasipo shaka wanaona gurudumu linakwenda vile ambavyo limekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi zinaenda sambamba kwa viongozi ambao wanamsaidia Mheshimiwa Rais akiwemo Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za mwisho ni kwa Wizara husika ambayo inamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na hotuba nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameiwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia maeneo mawili. Eneo la kwanza ni la maji na mafanikio yake; na eneo la pili ni miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema hapa, nami Mbunge wa Jimbo la Kibamba ni lazima niwe shuhuda. Huu ni mwaka wangu wa tano ninazungumza humu, lakini miaka mitatu hivi ya mbele ilikuwa ni kila siku ninazungumza juu ya hili hakuna, lile hakuna na hili hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sasa hivi kila jambo liko kwenye njia. Mambo mengi yamefanyika kwa zaidi ya 90%, mambo yaliyobaki ni madogo madogo. Mfano mzuri, mara nyingi nilikuwa nikisimama hapa nilikuwa nazungumza juu ya maji, lakini nataka niseme, Kamisaa wetu ndugu yangu Jumaa Aweso, Mbunge, amefanya kazi kubwa sana kwenye Wizara yake ya Maji. Katika hili amemsaidia Mheshimiwa Rais vile ambavyo alikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu Kibamba kuna matenki makubwa matatu. Baada ya kuyakamilisha kama vihifadhia maji, lile la Tegeta ‘A’ lina ujazo wa lita milioni tano, la Mshikamano lina ujazo wa lita milioni sita na lile ambalo mmekamilisha juzi la kule Bangulo ambalo linasaidia wananchi wengi wa Kusini mwa Dar es Salaam na kwangu Kibamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake King’azi ‘A’ na ‘B’ ambao hawakuwa na maji kabisa, maeneo ya Mtaa wa Saranga ambao ni maeneo ya Mashujaa, eneo la Mpakani na eneo la Mtaa wa Ukombozi, maeneo haya yote hayakuwa na maji, lakini nashukuru sana sasa hivi wanaendelea kupeleka usambazaji wa maji na watu wengi wanashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wWanasema Mheshimiwa Mbunge, ule mradi wa ujazo wa lita milioni tisa uliokuwa unausema Bungeni mara nyingi, ambao shilingi bilioni 37.8 za Benki ya Dunia zimetumika. Sasa wananchi wengi wa Kusini mwa Dar es Salaam ambao kwa Jimbo la Kibamba ndiyo walikuwa bado wana shida ya maji, sasa hivi wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mara nyingi huwa napenda kutoa elimu katika eneo hili. Mheshimiwa Waziri huwa anajitahidi sana kutupa elimu kwa upana juu ya changamoto ya maji katika historia na sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda wananchi wa Dar es Salaam na Pwani kwa ujumla wakiwepo wa Kibamba wajue, kazi ambayo tumeifanya katika kipindi cha miaka mitatu minne ni kutengeneza matenki makubwa ya kuhifadhia maji ili nyakati nyingi za kiangazi ambazo zinaweza zikaja, tujikute tunayo maji ambayo yanaweza kuwafikia waliopo mbali, lakini ukweli ni kwamba maji bado siyo toshelevu kwa walio wachache. Wengi wamepata, lakini wengine bado wanalia juu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie ukweli kwamba chanzo cha maji ni Ruvu. Ruvu Juu ndiyo inatulisha katika kipindi chote toka tumepata uhuru. Sensa ya kwanza ilifanyika mwaka 1910, ikaruka tukaenda kuanza upya 1968 na sensa ya mwisho ya sita tumefanya 2022. Dar es Salaam ilikuwa ina watu gani mwaka 1967? Sensa ya mwaka 2022 imekuwa na ongezeko la *population* kiasi gani? Lakini chanzo bado kilikuwa ni Ruvu Juu. Kwa hiyo, ni lazima tujue watu wanaendelea kuongezeka, lakini chanzo ni kile kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan peke yake kwa kufikiria jambo hili, ndiyo ameenda kuanzisha mradi wa Bwawa la Kidunda. Nataka niwaambie, Bwawa la Kidunda mpaka mwezi Machi, 2025 lilikuwa limefika 28%. Hili likikamilika, linaenda kujaza ujazo wa lita bilioni 190. Mheshimiwa Waziri anajua hili, lakini fedha zinazohitajika kutumika

pale ni shilingi bilioni 335. Fedha hizi siyo nyingi kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumeambiwa amekamilisha bwawa au mradi wa maji kule Rufiji wa zaidi ya shilingi trilioni sita nukta kadhaa, atashindwa shilingi bilioni 335 kukamilisha Bwawa la Kidunda ili maji yawe ni *sustainable* kwa Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dar es Salaam? Kwa hiyo, tunamtakia Mheshimiwa Rais kila la heri katika mradi huu. Mradi huu utatusaidia sasa maji yatapatikana Dar es Salaam kwa muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo juu ya eneo la miundombinu. Jimbo la Kibamba wakati tunaingia, hali ilikuwa ni mbaya sana, lakini sasa hivi barabara nyingi zimepata wakandarasi na wananchi wanajua hilo na barabara nyingi zimejengwa kwa zege na lami zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwepesi, tunao mradi wa *DMDP* chini ya *TARURA,* ambao mpaka sasa tayari wakandarasi wameshasaini mikataba na Mheshimiwa Waziri Mchengerwa. Kwa mfano, barabara ya Makabe – Msumi yenye kilomita 11.2 na daraja lake sasa hivi tayari Mchina yuko *site* anaendelea. Wananchi wana furaha kwenye jambo hili na wanaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni barabara ya Mkorea *Road* – Goba yenye kilomita 7.7. N,ataka niwaambie kuna Daraja la Mama Katunzi tulilijenga mwaka 2022 na sasa hivi barabara nzima inaenda kujengwa na mkandarasi amepatikana. Mwisho, ni kule ambako tunajenga *VETA* ya Wilaya ya Kibamba – Kibwegere, barabara ya Shija *Road,* kwa heshima ya Mzee wetu Shija William Shija, tuliipa hiyo barabara jina lake, na sasa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amekubali kujenga lami kilomita 4.2 na mkandarasi amepatikana. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie, hizo ni barabara za *TARURA* ambazo ziko chini ya mradi wa *DMDP,* lakini

*TANROAD* na yenyewe imeendelea kuwepo ndani ya Jimbo la Kibamba kwa barabara chache cha haraka. Barabara ya njia panda ya shule inayoenda Mpiji mpaka sasa ipo kilomita ya saba ya lami na mkandarasi yuko *site* anaendelea. Haya mambo huko nyuma hayakuwepo. Pia, kuna barabara ya Matosa kuelekea Temboni, kilomita sita. Kilomita tatu tayari mkandarasi yupo na anaendelea na ujenzi wa barabara hiyo. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara ya pale Kimara inayoenda Bonyokwa, mara nyingi nimeisema hapa. Tupo Waheshimiwa Wabunge wote watatu, sasa hivi mkandarasi ameshalipwa na yupo *site,* anaendelea kujenga lami ya kilomita zote saba. Mimi kama Mbunge wa Kibamba, lazima niziseme shukrani. Huu mwaka siyo wa kulalamika, ni mwaka wa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake ya Awamu ya Sita kwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mheshimiwa Mbunge anasema huku mambo ambayo wamefanyiwa au ambayo wamefanikiwa. Huyu ni nani? Ni zaidi ya Rais mwenye macho makubwa yenye kuona kila pembe ya nchi hii, tunaona na tunapata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme wazi Mheshimiwa Rais anatudai sisi Jimbo la Kibamba na Wilaya ya Ubungo, tuna haki ya kutoa kura za kutosha kwa Mheshimiwa Rais. Pia, kwa kuendelea na utetezi wa Wabunge wote, kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Jimbo la Ubungo na Kibamba, ni mimi Issa Jumanne Mtemvu, kwa kishindo sana asubuhi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Abdul-Hafar Juma, unaweza kuchangia kwa dakika tano?

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelekezo yako.

**MWENYEKITI:** Basi changia kwa dakika tano.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi. Katika muda wangu huu, naomba niipongeze sana Serikali kwa kuendelea kufanya mambo muhimu na hasa yale ambayo tumeahidi katika Ilani yetu ya mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yaliyosemwa katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na yale tuliyoyaandika katika Ilani yamedhihirisha kwamba CCM huwa inapanga maendeleo kwa ajili ya Taifa na yeyote atakayekuwa Serikalini atatenda yale yaliyoelekezwa na CCM kwa maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tukaona Daraja la Kigogo – Busisi limekwisha, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere umekwisha na mambo mengine yote yaliyoahidiwa katika Ilani pamoja na mtihani uliotokea kwa Taifa letu, lakini Mheshimiwa Rais, Mama Mheshimiwa Dkt. Samia ameweza kuyatekeleza. Hii ni kwa sababu anatoka katika Chama cha Mapinduzi ambacho kina utaratibu mzuri wa kutenda kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishauri Serikali jambo moja. Hivi karibuni kumetokea changamoto kidogo kwa vijana wetu wanaosoma elimu, wanaomaliza diploma, walivyoomba kwenda kwenye *degree* kwa *course* ya *Pharmacy*, hakuna muunganiko mzuri sana kwa *TCU* pamoja na *NACTE* katika kuwachukua wanafunzi wanaotoka katika ngazi ya diploma kwenda katika ngazi ya *degree* kwa upande wa *Pharmacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vya mwanafunzi kujiunga na elimu ya diploma ya Pharmacy kwa mujibu wa *NACTE* vinamtaka afaulu *Chemistry, Biology* na masomo mengine yoyote lakini wanafunzi hawa walipoenda kuomba kujiunga na *degree* wakashindwa kwa sababu *TCU,* imeongeza kigezo cha kuangalia matokea yao ya Kidato cha Nne, siyo kuangalia *GPA* pekee yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanafunzi ambao hawakuweza kufaulu mfano katika Somo la *Physics*, *Mathematics* pamoja na kufaulu *Chemistry* na *Biology* hawakupata nafasi ya kujiunga katika vyuo vikuu ili kuendelea na *degree* kwa sababu vigezo hivyo haviendani na *TCU* pamoja na *NACTE.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ushauri wangu kwa Serikali? Ikiwa *TCU* itaboresha vigezo vya kuwapa nafasi vijana kuendelea na elimu ya juu, basi waangalie kwanza vijana waliopo na waangalie vijana ambao hawatoki Kidato cha Sita kwenda kwenye *degree,* wanatoka katika elimu hii ya kati ambayo inasimamiwa na *NACTE.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii imetokea, hata mimi Jimboni kwangu Mtoni wapo vijana wengi nilikutana nao katika ofisi yangu ya Jimbo. Wao walisoma *Diploma* ya *Pharmacy,* walipomaliza Kidato cha Nne, lakini kwa sababu hawakufaulu Somo la *Physics* na *Mathematic* na halikuwa katika vigezo vinavyowapa fursa ya kujiunga na *Diploma* ya *Pharmacy* lakini kwenda katika *degree* wamezuiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu kazi yake ni *coordination* ndani ya Serikali waone navyoweza kui-*coordinate NACTE* pamoja na *TCU* watengeneze suluhisho kwa maslahi ya vijana wale wa Jimbo langu la Mtoni na maslahi ya vijana wengi ambao wamekosa fursa hii kwa sababu ya kigezo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, kwa sababu kule Zanzibar, moja ya mambo ya manufaiko ya Muungano ni *TASAF*. Naomba niipongeze Serikali yetu katika miaka mitano hii kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuendelea kuimarisha *TASAF,* lakini nina ombi la ziada pale *TASAF* itakaporudi na kuongezeka, waone wanavyoweza kuongeza wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimboni kwetu kule bado maskini, ni wengi waliangaliwa na hawakupata fursa ya kunufaika na *TASAF,* lakini pia *TASAF* ina muda maalum wa kupitia wanachama wake na kuwaongeza. Naomba muda huu uwe wazi kwa sababu watu

maskini wanajulikana wakiwekwa katika vile vigezo vya kuigizwa katika kunufaika na *TASAF* basi, isisubiri ile mara moja kwa mwaka waendelee ku-*update* kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, naishukuru Serikali kwa kuendelea kuwawezesha wanachama wa *TASAF* kwa kuwapa ruzuku pale kila muda unapostahiki, lakini nawaomba zaidi mradi utakapokuja, basi waongeze ruzuku ile kwa sababu gharama za maisha zimepanda na muda mrefu wanufaika wa *TASAF* wamekuwa wakipewa gharama ile ile ama ruzuku ile ile moja kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuongeze fedha ili wanufaika wa *TASAF* waendelee kunufaika na ule msaada wa Serikali iliyo chini ya CCM kwa wananchi wake uendelee kuleta matunda kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nimalizie kwa kuwapongeza sana wasimamizi wa *TASAF* kule Zanzibar, Unguja na Pemba. Naomba nimpongeze *TMO* wa Pemba kwa maendeleo makubwa na matunda ya *TASAF* ambayo yameonekana Pemba. Pia, naomba nimpongeze *TMO* wa Unguja ambaye anasimamia na Jimbo langu, wananchi wameendelea kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Serikali ikifikiria kuendelea kuwatumia vijana kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, basi ni vema ikaendelea kuwafikiria vijana hao na vijana mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeisha. Tutakaporejea jioni, tutaanza na wachangiaji wafuatao: -

Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mheshimiwa Ali Hassan King na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha Kikao cha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na michango. Nilishawataja wale ambao wataanza. Nilimtaja Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, simwoni...

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo hapa.

**MWENYEKITI:** Umehama *seat* yako?

Haya, atafuatia Mheshimiwa Ali Hassan King na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel, ajiandae,

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Binafsi napenda

kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na afya njema kuweza kuhudhuria katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya katika kipindi chake cha uongozi. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amepata uongozi katika kipindi ambacho Taifa letu tulikuwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, lakini Mwenyezi Mungu alimpenda, baada ya kumpenda akatupa tunu nyingine, tukampata Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, Taifa hili ni Taifa la Mungu kwa maana katika kipindi kigumu ambacho tumekipitia, kama Taifa, tumeweza kuvuka salama. Mwenyezi Mungu kwa hekima kubwa alizomjalia Rais wetu, ameweza kutekeleza yale yote ambayo yalikuwa ndani ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha miaka mitano 2020/2025. Kwa kweli, tunampongeza na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema, aweze kuhudumu tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano, 2025/2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kipindi chote ambacho ameweza kuhudumu, sasa anaenda kukamilisha miaka 10 katika nafasi ya Uwaziri Mkuu, nampongeza sana. Utendaji aliokuwa akiufanya alipokuwa Waziri Mkuu kipindi cha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ameendelea kuwa hivyo hivyo ama zaidi katika kipindi cha Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu hongera sana, kazi yako ni njema. Tumeona umekuwa msaada mkubwa kwa Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan sehemu zote katika Taifa hili, lakini pia, umekuwa mstari wa mbele katika kuisimamia Serikali na Mawaziri wote ndani ya Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akifanya ziara maeneo mbalimbali. Hata hivi karibuni alikuja Jimboni kwetu Manonga, ndani ya Wilaya yetu ya Igunga na ameingia kipindi ambacho ni muda mrefu kumekuwa hakuna mvua, zimesimama, lakini siku aliyoingia yeye, mvua kubwa sana ilinyesha ndani ya Wilaya yetu ya Igunga. Mwenyezi Mungu, na yeye pia ni shahidi kwamba ilikuwa ni neema. Wananchi walifurika kumsubiria Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mvua kubwa, wananchi wa Simbo walijaa, walivumilia, walinyeshewa na mvua. Ama kwa hakika Mwenyezi Mungu amekubariki na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu, Mheshimiwa Rais akipata tena awamu ya 2025/2030, ikimpendeza, tunakuombea akurudishe kwenye nafasi hiyo ya Waziri Mkuu kwani unatosha na unaweza kuifanya hii kazi vizuri. Umekuwa ni kiongozi unayeleta matumaini kwa Watanzania, Mungu aendelee kukubariki na kukupa afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho naweza nikasema katika huu mpango ambao ameuwasilisha Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli kuna mambo makubwa ambayo watu huwa wanadhani kwamba, Rais anapokuwa madarakani, kwa mfano tunapomaliza bajeti mwezi wa Sita, watu wanadhani fedha huwa zinabaki kwenye akaunti za benki, zipo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawajui kwamba, fedha tunazikusanya, tunazitafuta. Mfano katika kipindi hiki cha Bunge la Bajeti, tunapanga mipango ya maendeleo ya miaka mingine mitano au kwa kutegemeza kwa bajeti ya mwaka mmoja mmoja. Katika utafutaji wa fedha, huwa tunazitafuta kutokana na makusanyo, kwa mfano, tulikuwa na bajeti ya shilingi trilioni 50 ambayo tunaenda kuikamilisha mwezi huu wa Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa na hii bajeti, tunakuwa na fedha ambazo nyingine tunazikusanya kutokana na mapato yetu ya ndani. Tumejiwekea kukusanya shilingi trilioni 39 *point something,* lakini tunakuwa na *deficit* ya bajeti ambayo fedha hizi nyingine tunakopa kutoka katika Mataifa mengine

mbalimbali, kutoka kwenye mashirika makubwa ya kifedha na pia, nyingine zinatoka kwa wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba, hatuna fedha ambazo zinakuwepo tu, maana yake, kuna fedha tunazitafuta kupitia kukusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanasema tunadaiwa shilingi trilioni 97. Ni kweli, tunadaiwa shilingi trilioni 97, lakini tumedaiwa kuanzia lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fedha ambazo ni za mwendelezo kuanzia Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ni madeni ya Awamu ya Pili ya Mwalimu Ally Hassan Mwinyi, madeni ya mwendelezo ya Mheshimiwa Mkapa, madeni ya mwendelezo ya Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ni madeni ya mwendelezo ya Dkt. John Pombe Magufuli na hivyo hivyo ni madeni ya mwendelezo katika Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni madeni ambayo tumeanzia chini mpaka leo kufikia deni la shilingi trilioni 97.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili deni ukilinganisha na Mataifa mengine, mfano katika Taifa la Kenya jirani zetu, ambao wao uchumi wao ni mkubwa, tunakwenda, tunawakimbiza, tunawafuata, wao wana deni la zaidi ya shilingi trilioni 200. Sisi ni shilingi trilioni 97, kumbe bado sisi ni Taifa himilivu na tuna uwezo wa kukopa. Serikali kopeni tutekeleze miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi tunazokopa, hatukopi kwa ajili ya kuja kulipana mishahara. Fedha hizi tunazokopa zinaenda kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Tumeona wakati ujenzi wa reli ya *SGR* unaanza, Dkt. Magufuli alitafuta fedha, ni fedha hizo hizo za mikopo tumeanza kujenga kutoka Dar es Salaam tukaja mpaka Morogoro na nyingine zikajengwa kutoka Morogoro kuja Dodoma. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati anaingia hakukuwa na fedha za kujenga treni, kwanza kumalizia, lakini pia kuanzisha *route* nyingine, kwa maana

ya kutoka Mwanza – Isaka, Isaka – Tabora, Tabora – Makutopora na pia, Tabora – Kigoma. Fedha hazikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutafuta fedha kwa ajili ya kuwekeza, na leo tumeona treni ya umeme kutoka Mwanza – Isaka imeshafikia hatua ya 62%. Pongezi nyingi sana, kazi ni nzuri na tunaendelea kuiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema, kwa sababu tunaruhusiwa kuendelea kukopa, tukope tukamilishe hii miradi na fedha tunazokusanya tunaenda, tunalipa madeni kidogo kidogo mpaka hata miaka 20, miaka 30, Taifa letu ni himilivu na linaweza kulipa haya madeni. Mtu ambaye hawezi kulipa madeni hawezi kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kazi zote nzuri. Tumeona mradi mkubwa wa Bwawa la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere la *megawatt* 2,115 limekamika. Hongera sana Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri iliyofanyika. Hili taifa lilikuwa na uhaba wa umeme, tuna upungufu, tulikuwa tunazalisha umeme kwa *megawatt* 1,700, lakini bado tulikuwa na upotevu, tulikuwa tunaweza kupeleka kwenye mfumo wa *grid* ya umeme 1,400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza, tumezalisha umeme zaidi ya *megawatt* 4,000. Kwa kweli, ni hatua kubwa, tunaipongeza sana Serikali na tunajua kwamba, kazi zote hizi ni kuhakikisha tunamkwamua Mtanzania, kumwondoa katika kiza, kumpeleka katika maendeleo. Tumeona katika maeneo yetu leo nchi nzima hakuna kijiji ambacho hakina umeme. Hii kazi ni nzuri, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kwa nini mnapongeza nyie Wabunge wa CCM? Sasa kama kazi inafanyika, kwa nini tusipongeze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anapofanya kazi vizuri, ni lazima apongezwe. Tuna vitongoji 66,000 nchi nzima, leo vitongoji

vilivyopelekewa umeme ni 33,000, tumebakiza vitongoji 33,000. Hii ndiyo kazi ambayo sisi Wabunge wa CCM tunaishauri Serikali itafute fedha, iwekeze ili wananchi wetu waweze kupata umeme katika maeneo yote. Serikali kopeni fedha zije zipeleke umeme katika vitongoji vyote ili nchi nzima iweze kuenea umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko tunaona mabadiliko makubwa sana kwenye vijiji vyetu. Vijiji ambavyo vilikuwa havina umeme, vikipata umeme tunaanza kuona maendeleo. Pale kwenye eneo lile la Kijiji, watu walikuwa wanalala saa mbili, leo wanalala mpaka saa saba usiku.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa Taarifa mzungumzaji. Pamoja na mchango mzuri, pale kwenye Jimbo la Kibiti kuna vitongoji na kuna vijiji vipo visiwani kabisa. Tangu uhuru walikuwa hawategemei na hatukutegemea kupata umeme. Leo ninavyozungumza, shilingi bilioni 3.8 imekwenda, na umeme kule uko pukapuka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gulamali, unaipokea Taarifa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa. Imenikumbusha hata jimboni kwangu nilipewa na Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan shilingi bilioni 15 kupeleka umeme kwenye vijiji vyangu vyote jimbo zima na sasa umeme unawake. Kwa nini nisipongeze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, napongeza na kuwatia moyo kwamba, chapeni kazi, Watanzania wamewaelewa, watu wa Manonga wamewaelewa. Hata jimboni kwangu tunasema, Mama Samia mitano na hata mimi mwenyewe, Gulamali, mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukwambia, ndani ya jimbo letu tulikuwa na shida kubwa sana ya maji. Hii Serikali imetupa fedha za kupeleka maji kwenye vijiji vyetu, kati ya kata 19, kata 16 tunakwenda kutumia maji ya Ziwa Viktoria. Kwa nini nisipongeze hii kazi nzuri ya Chama cha Mapinduzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia Watanzania na Wana-Manonga wanajua kwamba, tunakwenda kwenye uchaguzi mwaka huu 2025, watapata kura za kujaa nyingi. Hata haya maneno wanasema kwamba, *No Reform No* sijui nini, hakuna kitu kama hicho ndani ya Jimbo letu la Manonga; hakuna kitu kama hicho ndani ya Wilaya yetu ya Igunga. Mwaka huu uchaguzi utafanyika na utakuwa wa amani na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu na watu wako wote kwenye ofisi yako na Mawaziri wanaokusaidia tunawatia moyo, chapeni kazi, tembeeni kifua mbele, mjiamini, Watanzania wanawaunga mkono, msisikilize hizi kelele. Tunasema, kelele za chura hazimzuii ng'ombe kunywa maji. Kwa hiyo, ninyi chapeni kazi, sisi tupo, jeshi lenu lipo, na wananchi wanawaamini kwamba kazi inaonekana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gulamali ahsante sana. Muda wako umeisha.

**MHE. SEIF K. A. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa na mengi, lakini kwa sababu muda siyo rafiki, naipongeza na kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, na Mheshimiwa Maimuna Mtanda ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, tumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupatia uhai na leo kufika hapa, kuja kuangalia maslahi ya

nchi yetu, kupanga maendeleo na pia, kuweka sawa ustawi wa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi waliozungumza walikuwa wanataja maendeleo ya vitu. Vingi vilivyotajwa hapa ni vitu, lakini kuna maendeleo mengine inawezekana ikawa, pengine huwezi kuyaona kwa kuyashika, siyo *tangible* kwa sababu, huwezi ukaya-*count* kama ambavyo una-*count* barabara, kama unavyo-*count* visima au unavyo-*count* vijiji. Tumeahidi kwa wananchi kwamba, tutaweka ustawi au tutatizama maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu nilichokusudia kuzungumza hapa ni maendeleo ya watu. Nakwenda moja kwa moja katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 8(a) inasema kwamba: -

*(a) Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii; na*

*(b) Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nipo katika Kamati ya Ustawi wa Jamii. Sisi pale tunashughulika na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo mifuko hiyo ndiyo inatoa ustawi kwa watu ambao wapo katika shughuli zao za kazi, pengine watapata majanga watakuwa wanapata *compensation*, lakini pia, uzeeni watakuwa wanategemea kupata matibabu na vitu vingine kama tunavyojua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu makubwa ya hii mifuko yetu ambayo tumeipa, moja, ni kufanya uandikishaji wa wanachama ambao ni wafanyakazi, na sasa hivi tume-*extend* madirisha, tunakwenda mpaka kwa watu binafsi waliojiajiri wenyewe. Pia, kupokea michango kwa wanachama, kufanya uwekezaji kwa ajili ya kutunza hizi fedha zisije zikaathirika na mambo ya mfumuko wa bei, na pia, kulipa mafao kwa wanachama. Ni maendeleo makubwa ambayo yamepatikana

katika hii mifuko ya hifadhi ya jamii, kwa kila kipengele. Tunaishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa kuisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, nianze na Mfuko wa *NSSSF*. Kwenye *NSSSF* pale ukiangalia idadi ya wanachama ambao ndio wanashughulikiwa hapa katika kuandikishwa imeongezeka na hata uchangiaji nao umeongezeka. Ukija katika *PSSSF* vilevile, ukija *WCF* unakuta vilevile. Kwa hiyo, unakuta huduma hizi zimeboreshwa, zimeongezeka. Ukitazama katika uandikishaji na uchangiaji wa wanachama katika huu mfuko umeboreka na kuwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatoa *indicator* gani? Ni *indicator* kwamba, watu wanapokwenda kustaafu, bado wataendelea kupata uhakika wa maisha yao ya kila siku ambayo yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna changamoto katika uandikishaji na kupeleka michango. Changamoto moja ni usahihi wa taarifa za wanachama, na nyingine ni ucheleweshwaji wa michango. Hizi taasisi zetu zimeanzisha mifumo ambayo inaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri kwamba, kwa kuwa *garbage in, garbage out,* utakachokitia katika mfumo ndicho kitakachokuja kutoka, kama jawabu katika huo mfumo, kwa maana hiyo, nilikuwa nasema kwamba, hii mifumo ambayo imeanzishwa, ni lazima iendane au isomane na ile mifumo katika ajira au katika utumishi, na hapa ndipo tutakapohakikisha hizi taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni usahihi huu wa taarifa utatokana na Serikali. Kwa hiyo, hapa naiomba Serikali katika kubadilisha wale wafanyakazi wanapobadilishwa madaraja yao ya mshahara na wanavyobadilishwa vyeo, kwa sababu, inakuja changamoto kama mtu hajabadilishiwa mshahara wake, amepanda cheo halafu ikafika siku ya kustaafu bado mshahara siyo sahihi, au mchango sahihi haukupelekwa. Hapa huyu

mfanyakazi ndiyo hizi lawama zinazokuja. Pamoja na pongezi hizo tulifanyie kazi hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni hawa watu wanatunza fedha. Mimi hapa nimejaribu kufanya *calculation* nyingi, kutokana na muda siwezi kuzisoma zote, lakini ukitazama kwamba, mifuko ina uwezo wa kulipa kwa mwaka *three times* kutokana na zile rasilimali ambazo wanazo, walizokusanya na mapato kutokana na uwekezaji, kwa sababu, makusanyo ya michango yameongezeka, nizungumze kwa ujumla ule uwekezaji. Mapato kutokana na uwekezaji, umeongezeka ambapo ukiweka mapato ukigawa kwa mafao ambayo yanatarajiwa kulipwa, utakuja kuona kwamba, mifuko ina uwezo wa kulipa *more than three times*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hili hongera sana kwa sababu, kilikuwa ni kilio cha watu. Sasa hivi mtu ana uwezo wa kulipwa hata kama ni ndani ya miezi miwili baada ya kustaafu. Sasa hivi sisi Wabunge tunachelewa kupokea mishahara kuliko wastaafu wanavyopata pensheni, wao kabla ya tarehe 25 ya kila mwezi wanakuwa tayari wameshapata na wanashughulikiwa kila kitu chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kitu kimoja, kwenye uwekezaji, hii mifuko wametupatia *comfort* kubwa sana kwa maana ukitazama wao wamesema wanajilinda na *rate inflation*. Sasa hizi fedha ziko juu, yaani *income own investment* iko juu mara mbili zaidi kuliko ile *inflation* ya katika nchi. Sasa hapa naomba tuipongeze Serikali na pia, tuendelee kushika uzi huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri hapa ni kila tutakapowekeza, basi tujaribu kutazama kuwekeza kwenye tija zaidi. Hatusemi kwamba hii haijawekezwa kwenye tija, tuwekeze kwenye tija zaidi. Tujaribu kutazama maeneo ambayo tutapata *multiply effect* ili tuweze kuboresha pia maisha ya wananchi wengine ambao labda sio wanachama wa hii mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika kitu kimoja ambacho kila mwaka hapa lazima nisimame nizungumze, ni kuhusu *SDL*. Kuna makubaliano kuhusu hii *Skills Development Levy* baina ya Serikali na sekta binafsi, kwamba *one third* itakwenda kutizama *gap of skills* ambazo hizi kampuni zinazochangia ndizo zinazotoa hizo fedha ili ile *skill* ije kwa wananchi, ili hawa watu wasiende kuwaajiri watu wengine wa kutoka nje. Leo tunafurahi kupokea fedha kwa sababu ya kutoa vibali vya ajira, kumbe ile kazi ingeweza kufanyiwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wa *ATE* wanasikitika, na masikitiko yao kwamba wao ndio wanaomlisha ng'ombe majani, ila maziwa yanakamwa na mtu mwingine, sasa wao hawafaidiki na michango hii. Ukitizama hapa; nitaikabidhi *trendy* ya michango ya *SDL* na ile *one third* inayotakiwa ambayo hata hivyo haifiki; hata moja ya kumi na tano ambayo ndiyo inayokwenda katika kutizama *gap of skills* ambayo Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo inayoshughulikia. Hili lingefanyika katika uratibu mzuri, lingekuja vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo hapa kwamba tunatoa vibali, tunapokea fedha, lakini tunanyima ajira za Watanzania wenzetu. Leo ukiingia mtaani utakuta hata kidampa kinaendeshwa na Mchina. Hivi hapa imeshindikana kupatikana mtu wa kuendesha hiki kidampa! Kwa hiyo, hii ni lazima tutazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, tumetoa kazi kwa watu ambao wamesema watarithisha ujuzi lakini ule ujuzi hawarithishi. Anafika mtu anamaliza mkataba wake, amesema baada ya miaka mitatu ataacha ujuzi lakini hakuna ujuzi ulioachwa. Kwa hiyo, tunawaacha Watanzania wenzetu hawana ajira ndani ya nchi yao na ajira zinachukuliwa na wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kutaja taasisi ambazo zimeingia mikataba, lakini zipo taasisi zina mikataba. Hii mikataba ya kuacha ujuzi kwa wananchi, ingekuwa zinaratiwa pia na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu ndiyo inayosimamia masuala ya ujuzi. Huku kwingine ni sawa, Wizara ya Fedha watakuwa na mkataba, na *vendor* atakuwa na mkataba, Wizara ya Kilimo na mtu

mwingine, lakini hakuna taasisi inayoweza kwenda kuratibu ndani ya Wizara ya mwenzake. Kama hawakufanya hivyo, na kama hawajafahamiana, tutakosa ajira nyingi za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze jambo moja ingawa wenzangu wengi wamezungumza. Unajua kuna watu wengine ni majuha. Juha sifa yake kama hukumtaja, juha anakuwa havumi; lakini juha kila ukimtaja, yule huja anapata kichwa. Kwa hiyo, na sisi lipo juha humu tunalitajataja, kwa nini tusiliachie? Yule mtu tayari ameshapata mahana, na watu wameshamtoa maana. Baada ya kumahanika, amekuwa hana maana; hamwoni kwamba hata wananchi wameshamjua kwenye mikutano yake hawaendi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama ningelikuwa nasikilizwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, juha hili tungeliacha kwa sababu hili juha ukilitaja linapata kichwa. Tunampa *milage* ya bure. Ya nini mtu kama yule? Mtu ana laana mpaka ya Baba wa Taifa, kwa sababu anasema hii nchi haijakombolewa, yeye ndio anatafuta ukombozi. Wale wazee wetu walifanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Msajili wa Vyama vya Siasa tunapitisha bajeti yake hapa, kuna juha huyo anasema nchi haijakombolewa. Hatuna ajenga katika nchi hii za kuzungumza! Hivi kweli kipo chama kinaweza kikaundwa hapa kikawa ni chama cha ukombozi! Kwa hiyo, tulikuwa tunataka tutazame mambo haya kwa sababu watu hawa tayari wameshaingiwa na mahana, lakini sasa na wananchi wameshawatoa maana kwa sababu wamehamanika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na kutufanya tukutane leo kuzungumza maendeleo ya nchi yetu na kupitisha bajeti kwa ajili ya ofisi muhimu kabisa ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nitumie fursa hii kwa ruhusa yako kabla sijasahau, maana nimeona mambo yapo vizuri, niunge mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndipo niendelee kushauri na kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo amewasilisha, lakini kwa mambo ambayo yamewasilishwa kwenye hotuba yake ya bajeti ya ofisi yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu hongera sana na umetutendea vyema Watanzania na umelitendea vyema Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Mweyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu anao wasaidizi ofisini kwake wakiongozwa na Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Ridhiwani; Waheshimiwa Manaibu; mdogo wangu Mheshimiwa Katambi na Mheshimiwa Ummy, wanamsaidia vizuri; nao hongera zao ziwafikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme maneno machache ambayo ninaamini hata Mwenyezi Mungu yanayo baraka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tumemshukuru kwa uhai lakini Mwenyezi Mungu mimi ninamshukuru sana kwa nchi hii inayoitwa Tanzania. Mwenyezi Mungu ametujalia Taifa imara, lenye utulivu, lenye amani na lenye mshikamano. Nchi yetu bado ipo imara na tumekuwa mfano mzuri kwa dunia na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Tanzania ipo hivi kwa sababu Watanzania wenyewe waliamua iwe hivi. Watanzania kwa utashi wao na kwa uelewa wao wamendelea kwa muda mrefu kukiamini na kukipa kura nyingi na ushindi Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mapinduzi kimekuwa ni msingi wa uimara wa nchi yetu. Nawe na Watanzania wote ni

mashahidi, Chama Cha Mapinduzi kimepita katika mapito mbalimbali kikiwa imara na mshikamano na kuweka mbele Utaifa. Chama cha Mapinduzi kimekuwa kikibadilisha viongozi wake. Leo tunaye Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi ambaye ni wa sita chama kikiwa imara bila mgawanyiko na bila vurugu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi, kuna baadhi ya vyama vikitaka tu kubadilisha viongozi, mwisho wa siku hawamalizi vizuri. Kwa hiyo, Watanzania sio wajinga kuendelea kukiamini Chama Cha Mapinduzi. Mimi nawashukuru sana, wamekuwa wakitumia upeo wao, uwezo wao na baraka za Kimungu kuendelea kukiamini Chama Cha Mapinduzi. Naamini bado wanaendelea kukiamini, na mwaka huu watakipa ushindi wa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama hiki Cha Mapinduzi tangu mwaka 2020, leo ni 2025 tumekuwa na Ilani yetu, tumeitekeleza kwa kiwango kikubwa, na hii ni bajeti ya mwisho kwenye Ilani ya 2025. Nasimama mbele ya Bunge lako kama shuhuda. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye bajeti yake tunaijadili leo ndiye aliyekuja Sumve mwaka 2020 akaniombea kura kwa wananchi wa Sumve.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe ni shahidi, wakati anakuja Sumve wananchi walisema wana shida ya maji, walisema wana shida ya umeme, walisema wana upungufu wa vyumba vya madarasa, upungufu wa zahanati na vituo vya afya. Tunavyozungumza leo, wakati mimi naomba kura kwa watu wa Sumve, Serikali hii ya Awamu ya Sita iliyorithi kwenye Serikali ya Awamu ya Tano, wakati inaingia watu wa Sumve walikuwa wana vituo vya afya viwili, lakini leo tunavyozungumza, vimejengwa vituo vya afya vipya vitatu. Ina maana sasa vipo vitano. Katika muda wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wa miaka minne amejenga vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo tunavyozungumza, vijiji vya Sumve vipo 60, vijiji vilivyokuwa na umeme vilikuwa ni 18, leo tunavyozungumza vijiji vyote vina umeme. Hili ni ongezeko la vijiji

42. Kazi ya heshima kubwa sana imefanywa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza leo, barabara za Jimbo la Sumve zinapitika vizuri. Sumve haikuwa na maji ya Ziwa Victoria, lakini tunavyozungumza leo, zaidi ya shilingi bilioni 67 zimepelekwa Sumve ili kuleta maji ya Ziwa Victoria na kazi inaendelea. Kwa hiyo, tunajivuna. Tunasimama hapa kusema kwamba tumefanya kazi kubwa ya heshima, tunampongeza Mheshimiwa Rais. Kwa niaba ya watu wa Sumve, tunamwahidi kwamba kura zitajaa, zitakuwa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kidogo. Kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna jambo ambalo nafikiri tunatakiwa tuongeze kasi. Suala la ajira limekuwa bado na changamoto kwa vijana wetu. Vijana wanamaliza vyuo vikuu wanatafuta kazi, na Serikali kwa kweli imejitahidi kutoa nafasi za ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto ya vijana wanaoomba kazi kuwa na imani ya mfumo wa ajira Serikalini. Kwa hiyo, naomba kuishauri kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwamba tunayo kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa mfumo wa kuajiri vijana Serikalini unaaminika na umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sote ni mashahidi, zinapotokea nafasi za ajira Serikalini simu zetu Waheshimiwa Wabunge zinajaa *message*, kila mtu anataka tumsaidie kupata kazi. Hii ina maana kwamba wale wanaoomba kazi wanaamini kwamba kazi hizi zinapatikana kwa kusaidiwa na siyo kwa kuwa na sifa. Hawa watu hawawezi kufanya mambo haya kwa bahati mbaya, nadhani lipo jambo la kuangalia kwenye mfumo wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zetu zinazosimamia ajira, tuangalie namna bora ya kuhakikisha Watanzania wanaamini ule mfumo, na ule mfumo uwe rafiki ili kila mmoja aweze kuuamini. Ninadhani wote mmeona, juzi *TRA* wametangaza nafasi, kila mmoja hana imani. Kwa hiyo, hii ni changamoto, lakini ninaamini Serikali ya CCM ni sikivu na sisi Waheshimiwa Wabunge wa CCM

tutaendelea kuishauri vizuri Serikali yetu ili kuhakikisha kwamba changamoto zinazowazunguka Watanzania zinatatuliwa na tunaendelea kuaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri kwamba CCM bado inaaminika, CCM bado ni kimbilio la Watanzania, CCM bado ndicho chama chenye nguvu na kinachoweza kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba niishie hapo. Kwa kuwa nilishaunga mkono hoja, sasa nitoe nafasi kwa watu wengine. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasalali, ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Maimuna Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, na Mheshimiwa Japhet Hasunga ajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili nami nichangie machache kuhusiana na bajeti iliyopo mbele yetu, bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya, pia nawashukuru na niendelee kumwombea sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania afya njema kwa sababu ni mkombozi wetu, analeta ustawi katika maendeleo yetu na sisi tunayaona. Kipekee, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake yote kwa hotuba nzuri ambayo ameiwasilisha mbele yetu hapo jana. Hongereni sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo mnaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia, nianze na Jimbo la Newala Vijijini kwa kifupi sana. Sisi Wananewala Vijijini tulihamia kule jimboni tukawa hatuna jengo la utawala, hatuna Hospitali ya Halmashauri, hatuna shule nzuri na bora na mambo mengi; lakini kupitia uongozi mzuri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na wasaidizi wake wote, hapa tunapoongea, tuna jengo

la halmashari, tuna Hospitali ya Wilaya na kwamba umeme vijiji vyote sasa tumeshapata. Tulikuwa hatuna hata barabara ya lami pale mjini, sasa tunazo barabara za lami. Tunaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niongee kidogo kuhusiana na barabara yetu ya Kibiti – Lindi ambayo tarehe sita ya mwezi huu wa Nne ilipata changamoto ya mawasiliano kukatika. Naishukuru sana Serikali, kwa msimamzi wa Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake, msaidizi wake Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ameshinda kule, amekesha kule na ilipofika tarehe nane mawasiliano yakaanza kufunguka. Hapa tunapoongea, watu sasa wanapita. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuona haja ya kunusuru wananchi wa kusini kwa sababu maisha yao yalikuwa hatarini sana kwa kukosa yale mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kushauri kuhusiana na ile barabara kwa sababu mwaka 2024 ilijitokeza na sasa imejitokeza tena. Naomba Kiti chako, ili nishauri machache. La kwanza, ambalo nataka kushauri ni kuongeza usimamizi kwa wakandarasi ambao wamepewa kazi katika madaraja yale ambayo yalibomoka mwaka 2024. Tusipoongeza usimamizi wa karibu, inaweza yakatukuta haya yaliyotukuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee katika hili, namshukuru *M-NEC* wa Mkoa wa Mtwara, ndugu yangu Makapo kupitia *Makapo Contraction.* Yeye hakusubiri asimamiwe, alikuwa anafanya kazi muda wote, na eneo lake kwa kweli linaonekana. Kwa hiyo, nampongeza sana *M-NEC*. Nawaomba na wengine ambao wamepata kazi katika madaraja yale, waongeze nguvu, wasisubiri kusimamiwa ndipo wafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ambao nilitaka niutoe ni kwamba, mwaka 2023 niliiomba Serikali itujengee meli katika Bahari ya Hindi. Niendelee kuuomba mpango ule kwa sababu niliambiwa kwamba meli itajengwa, itawekwa kwenye mpango. Niendelee kuiomba Serikali yangu sikivu iweke kwenye

mpango wake ujenzi wa meli katika Bahari ya Hindi, meli ambayo inapotokea changamoto yoyote itasaidia kusafirisha abiria, pia itasafirisha na bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Visiwa vya Komoro wanategemea sana nchi ya Tanzania kupata huduma zao. Kwa hiyo, meli ya uhakika ikiwepo itawasaidia wananchi wa Komoro kupata bidhaa kwa urahisi na vilevile wananchi ambao wapo kando kando ya Bahari ya Hindi nao watapata fursa ya kufanya biashara zao ili ziweze kwenda kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kushauri ni kwamba kwa barabara hii imechoka sana, ina viraka vingi. Naishauri Serikali iweke kwenye mpango ili na yenyewe iweze kujengwa barabara yote badala ya vipande vipande au kuziba viraka viraka kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kushauri kuhisiana na barabara ni kuhusu wale wakandarasi ambao wamepewa kazi kuimarisha michepuko ile ambapo wakati wanatengeneza Barabara, watu pamoja na magari ya abiria pamoja na mizigo yanapita kwenye *diversions* waziimarishe zile *diversions* ili wananchi waweze kupita kwa uhakika wakati kazi ya ujenzi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine ambayo inahusiana na barabara, naiomba Serikali, Barabara ya Mtama – Kitangali – Newala kilomita 74 upembuzi yakinifu umeshafanyika, Serikali iweke kwenye mpango sasa wa kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Barabara ya Mnivata – Tandahimba, Newala – Masasi. Naomba kipande cha Mnivata – Tandahimba, kile kipande mkandarasi aongeze kasi kidogo ili iendane na muda. Mvua zilivyonyesha magari mengi sana yalikwama, lakini kama ataongeza kasi, basi huu mkwamo ambao umejitokeza kipindi hiki unaweza kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linalohusiana na barabara ni barabara za *TARURA*. Tunatambua kwamba mwaka 2024 mvua

nyingi zilinyesha na barabara nyingi ziliharibika na kuvunjika. Hata katika jimbo langu barabara nyingi sana zimevunjika. Kwa mfano, Mkoma II kwenda Chimemena, haipitiki kabisa; Mulunga kwenda Nandwahi imeharibika haipitiki; na Mtopwa kwenda Chilondolo imeharibika vibaya. Naomba wenzetu wa TAMISEMI watafute namna ambavyo watakuja kukarabati barabara zile ambazo ziliharibiwa na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye kilimo; nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na timu yake. Kwa kweli kwenye zao la korosho wametuheshimisha sana na wameliheshimisha Taifa kwa sababu uzalishaji kwa msimu wa 2024/2025 umeongezeka sana, na kuongezeka huku siyo kwamba kumekuja kwa bahati mbaya, hapana. Serikali ilileta pembejeo za kutosha ambazo wananchi walizitumia katika mashamba yao, jambo ambalo limeongeza uzalishaji kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe tu mfano kidogo kwa msimu wa mwaka 2023/2024. Tunacho Chama Kikuu cha TANEKU kinachohudumia Newala na Tandahimba, na ongezeko la uzalishaji ni 67.6%, lakini ukienda Bodi ya Korosho yenyewe, kwa ujumla wa Tanzania yote, ongezeko la uzalishaji kwa mwaka 2024/2025 ni 70%. Hili ni ongezeko kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapoongea leo, tayari mbolea ya *Sulphur* imeshateremka Mtwara, kinachosubiriwa ni usambazaji ambao utaanza tarehe 15 ya mwezi huu. Kwa hiyo, zile changamoto katika usimamizi wa ugawaji ambazo zilijitokeza kwa msimu uliopita, nishauri wenzetu wanaosimamia usambazaji wa pembejeo zile, basi wasimamie vizuri kwa ukaribu ili zile changamoto zipate tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hapo kwenye korosho, niwapongeze *TANEKU Limited* kwa sababu wamejenga kiwanda cha kwanza cha ushirika nchini. Tunawapongeza sana, kwani ni kiwanda ambacho kimeshakamilika, kimeanza kuzalisha ajira kwa wananchi wanaotoka maeneo jirani, kwa maana ya kwamba kimeanza kufanya kazi. Tunaipongeza sana TANEKU, wameanza utaratibu wa kujenga kiwanda kingine pale Tandahimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri tu Serikali, tuendelee kuwaunga mkono, watatuvusha kwa kiasi kikubwa sana. Katika hili, pia naishukuru Serikali kwa kutenga eneo la kongani ya viwanda vitakavyohudumia korosho katika Mkoa wa Mtwara pale Nanyamba. Tunawashukuru sana kwa sababu kongani hii itakuwa mkombozi badala ya kuuza korosho ghafi, basi tutauza korosho, karanga na matunda ambayo yanatokana na korosho tutayapata kwa namna mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali, na kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kazi, na anaumiza kichwa kwa ajili yetu. Sisi sote tumuunge mkono, ndiyo zawadi pekee ambayo tunaweza kumlipa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanakusini tunaendelea kumshukuru kwa sababu hata mazao ya ufuta na mbaazi na yenyewe bei ilikuwa nzuri kiasi kwamba iliwakwamua wananchi kutoka kwenye ile hali ambayo ilikuwepo na kwenda kwenye hali ambayo unafuu wa maisha ulipatikana kutokana na ziara ambazo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akizifanya katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hizo ndizo zilipelekea kuwapata wanunuzi wa mazao haya kwa urahisi kiasi kwamba bei ikaongezeka tofauti na ilivyokuwa kule nyuma. Sisi Wanamtwara na Wanaruvuma ambao na wenyewe wanalima korosho pamoja na ufuta, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuongelea ni suala la maji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda, muda wako umekwisha, ninaomba uhitimishe.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, yalikuwa mengi kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametukwamua kwenye maji, shilingi bilioni 84.7 haijawahi kutolewa. Ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiye ambaye ameleta kwenye mradi mkubwa wa Makonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilimwita Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga, na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ambayo iko chini ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara nyingine ambazo ziko chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutulinda na kutujalia afya njema hatimaye tumefika mwaka wa tano wa uhai wa Bunge hili toka tulivyochaguliwa mwaka 2020 na tunaamini kwa msaada wa Mungu tutarejea kwa sababu ni mpango wake na mapenzi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Tunamwona jinsi anavyohangaika kwenda wilayani na mikoani kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Namshukuru sana Waziri kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na wasaidizi wake wote na watendaji wote. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wajumbe wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI, tumekuwa tukifanya ziara mbalimbali mikoani na kwenye wilaya kufuatilia, kusimamia na kuangalia ni kwa kiasi gani fedha ambazo Bunge hili lilizipitisha,

zinafanya kazi. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana, yeye pamoja na Wizara yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kipindi cha miaka mitano ambayo nimekuwa hapa Bungeni, namshukuru Mwenyezi Mungu nimeweza kuhudumu kwenye Kamati ya UKIMWI, na sasa hivi Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa fedha za ndani, kulikuwa na changamoto kubwa sana ya utoaji wa fedha hasa kwenye masuala mazima ya fedha za maendeleo, lakini kwa miaka hii minne nikiangalia mtiririko wa utoaji wa fedha, kumekuwa na mabadiliko makubwa sana. Hadi kufikia Februari 2025, Tume ya Kudhibiti UKIMWI imepokea zaidi ya 73% ya fedha ambazo Bunge lako Tukufu lilizipitisha. Hayo ni matumizi ya kawaida, lakini kwenye matumizi ya miradi ya maendeleo, imepokea zaidi ya asilimia saba. Haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu ya nini? Ni kwa sababu Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan ina dhamira safi ya kuhakikisha kwamba mapambano dhidi ya virusi vya UKIMWI yanapiganwa kisawasawa. Kwa mara ya kwanza, ukiangalia ulinganisho wa bajeti kwa mwaka 2024/2025 na 2025/2026 utaona kabisa kwenye fedha za ndani za maendeleo fedha zilikuwa kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipiga kelele tukisema kwamba tuna Mfuko wa Kudhamini Mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI *(ATF)* ulikuwa ukipata fedha kidogo, ni shilingi milioni 500, bajeti inayomalizika ikatengwa shilingi bilioni 1.8; lakini kwa mwaka huu wa fedha Serikali imetenga shilingi bilioni 5.28 zaidi ya 180%. Haijawahi kutokea. Hii yote ni dhamira safi ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI yanapiganwa kiukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tuliweza kuona nchi mbalimbali na hasa nchi ambazo zilikuwa zinatufadhili sisi kama Watanzania kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ya

kupambana na Virusi vya UKIMWI pamoja na miradi mingine. Wananchi walipata hofu, walipata simanzi, kila mtu alikuwa na mashaka; itakuwaje? Kwa sababu misaada mingi inatoka nje, lakini kwa bajeti hii ambayo Serikali imeileta, na kwa maelezo ambayo Serikali imekuwa ikiyatoa, na kwa kuonesha kabisa dhamira ya kusimama, sisi kama Watanzania kuweza kuboresha mfuko wetu wa udhamini kutoka shilingi bilioni 1.8 mpaka shilingi bilioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wajumbe wa Kamati tunaona kwamba ni jitihada kubwa ambayo imeshafanyika. Japo, tunaona kwamba bado kuna uhitaji wa kuendelea kutafuta vyanzo vingine vya fedha za ndani kwa kushirikisha wadau wa ndani ili sasa mfuko wetu uwe endelevu na uweze kustahimili kuweza kupambana na Virusi vya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamefanyika, pamoja na afua ambazo zimefanyika na pamoja na mipango mizuri ambayo Serikali inayo, tunaona katika utafiti uliyofanyika mwaka 2022/2023 bado kuna changamoto ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Watanzania tusibweteke, UKIMWI bado upo, na kila mwaka Watanzania 60,000 wanapata maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, na katika hao 60,000 wanaopata maambukizi ya Virusi vya UKIMWI 34.4% ni vijana wadogo, na ni ambao ni nguvu kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatuambia nini? Hii inatukumbusha kwamba bado tuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha kwamba vijana wetu wanaendelea kupata elimu, lakini suala zima la kuhamasisha upimaji wa VVU unafanywa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika huo utafiti kwenye suala zima la upimaji, bado tuna 82.7% tu, ina maana kuna wananchi wengine wengi ambao bado hawaelewi afya zao mpaka sasa. Pamoja na afua zote zinazofanyika, bado kuna wananchi hawajajua *status* zao, ni 82.7%; lakini katika wale 82.7% ambao wameshajua kwamba wana maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, tunaishukuru sana Serikali yetu kwa kuhakikisha kwamba

97% wamepatiwa dawa za kuweza kufubaza Virusi vya UKIMWI; na katika wale ambao wameshagundulika, 94% tayari wameshafubaza Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwetu sisi hiyo ni hatua kubwa sana ambayo kama sekta tumeweza kuipiga. Kwa hiyo, kinachotakiwa sasa ni kuendelea kuhamasisha wananchi kuendelea kupima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina baba wengi hawapimi. Usijidanganye kwamba mke wako akipima, akaonekana yuko salama na wewe upo salama kwa sababu, kila mtu ana *modality* yake ya kupata maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Inawezekana mke wako yuko salama kwa sababu kinga yake iko imara, lakini wewe baba ukawa na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa kinara wa kuhamasisha upimaji wa Virusi vya UKIMWI. Kwa hiyo, Watanzania tujitokeze, tuendelee kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza hapa mambo makubwa ambayo yamefanywa na Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. Mwenye macho haambiwi tazama. Ukienda sekta ya afya hakuna kijiji ambacho hakijafikiwa, ukienda sekta ya maji, elimu na miundombinu; mwaka uliopita kulikuwa na Mvua za *El-Nino*, kila Mbunge hapa alikuwa analalamika, kila mwananchi alikuwa analalamika kwamba jamani, miundombinu imekuwa mibovu, lakini kutokana na juhudi za Serikali ya Mama Samia, miundombinu mingi iliweza kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata jana tumeshuhudia kule kusini barabara imekatika, lakini ndani ya masaa machache, barabara ile iliweza kupitika. Kwa hiyo, hizi ni juhudi kubwa ambazo zinafanywa na Serikali ya Mama Samia. Kwa hiyo, sisi kama Watanzania, sisi kama wananchi, sisi kama wanawake wa Tanzania, tutakuwa bega kwa bega kuhakikisha kwamba Mama Samia Suluhu Hassan na Serikali yote, Oktoba, 2025 inashinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, wamekuwa wasikivu, wachapakazi, hawalali; leo tunawaona Mashariki, kesho Magharibi, keshokutwa Kusini na Kaskazini, wanafanya kazi, wanatekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto waliozaliwa Shinyanga mwaka 2000 walikuwa wameusahau Uwanja wa Ndege Ibadakuli, lakini sasa hivi tunavyoongea, uwanja ule umeshakamilika zaidi ya 100%. Ni masuala machache ambayo yamebaki kwa ajili ya kukamilisha ili wale watoto wa mwaka 2000 waone kwamba kumbe Shinyanga kulikuwa na uwanja wa ndege mzuri ambao ndege kubwa zinaweza zikatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamefanyika. Halmashauri ya Manispaa ya Kahama ni mji ambao unakua sana, miundombinu haikuwa mizuri kabisa, barabara zilikuwa hazipitiki, ukienda Kata ya Majengo, ukienda Mungula, ukienda Malunga kulikuwa na barabara ambazo siyo rafiki na zilikuwa kero kwa wananchi, lakini sasa hivi ninavyoongea wakandarasi wako *site* wanatengeneza barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Shinyanga Manispaa wakandarasi wameshasaini mikataba, wanatengeneza miradi yote ya *TACTIC* ambayo imeidhinishwa. Tufanye nini sasa? Tuseme nini sasa? Ni lazima sisi kama Watanzania tuunge mkono juhudi za Mama Samia Suluhu Hassan, tumtie moyo na tumwambie kwamba akanyage mafuta, tena akanyage mafuta kwenye mteremko kabisa, asiachie. Wale wanaozira, wanaokataa, lakini sisi tunajua mwezi wa Kumi tuna Uchaguzi utafanyika, na Chama cha Mapinduzi kinakwenda kushinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, Mungu ibariki Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava. Nilimwita Mheshimiwa Japhet Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili nichangie katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na kutuwezesha kufika siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie nafasi hii kumshukuru sana, sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hekima, kwa umakini, kwa ujasiri na uwezo mkubwa ambao ameuonesha katika kuiongoza nchi yetu. Nampongeza sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza kwa sababu amekuwa na uwezo mkubwa sana wa kutafuta rasilimali, kutafuta fedha; amekuwa na uwezo mkubwa sana wa kupeleka miradi karibu kila jimbo, kila kata na kila kijiji. Amepeleka miradi mingi sana yenye manufaa kwa nchi yetu. Kwa hiyo, tunampa hongera kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake zote zilizoko chini ya ofisi yake kwa kazi nzuri ambayo taasisi hizo na Mheshimiwa Waziri Mkuu umefanya, kwanza katika kusimamia Serikali yetu, lakini la pili katika kuratibu majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na Serikali, na tatu kwa hotuba nzuri iliyosheheni taarifa, takwimu, maarifa mengi na mambo mengi ambayo yapo katika hotuba yako. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Timu yako kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa sababu imetekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa zaidi ya 100%. Kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025 tulibainisha baadhi ya mambo ambayo yalionekana ni changanmoto katika maendeleo ya Taifa letu. Moja ya changamoto zilizobainishwa ni pamoja na umaskini wa baadhi ya Watanzania, ambapo tuliona karibu 26% ya Watanzania, ambao ni robo, bado walikuwa katika umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tulibainisha changamoto ya ajira katika nchi yetu, tukabainisha uwezo mdogo katika kuongeza thamani ya mazao yetu katika maeneo mbalimbali; na tukabainisha uzalishaji duni na zana duni za uzalishaji na mambo mengine ambayo yapo katika ujenzi wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninapenda nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita. Katika suala la ajira, kutokana na kuona hizi changamoto, tuliweka lengo kwenye ilani, tukasema kwamba tunataka tuhakikishe katika kipindi hiki tutengeneze ajira zisizopungua milioni nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, takwimu zilionesha kuwa ajira zilizotengenezwa ni zaidi ya milioni nane kwenye upande huo. Kwa hiyo, hii ni kazi nzuri imefanyika, ndiyo maana ilani imetekelezwa kwa zaidi ya 100%, zaidi ya ajira milioni nane zimetekelezwa. Kutekelezwa kwa ajira hizo na miradi mbalimbali, maana yake umaskini wa Watanzania unazidi kupungua, kwa sababu uwekezaji mkubwa ndiyo unaosaidia katika kutanzua tatizo hili la umaskini katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hilo, Serikali ya Awamu ya Sita iliweka mkazo katika kuimarisha maslahi ya watumishi wa umma, na tumeona jitihada mbalimbali ambazo zimechukuliwa na Serikali katika kuhakikisha inaboresha maslahi ya watumishi wa umma. Kwa kweli kazi nzuri imefanyika, tumeona madaraja ya baadhi ya watumishi yanapanda, nyongeza zinajitokeza na mambo mengine mazuri ambapo fedha hizi zikipatikana ndiyo zinaenda kuwekezwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeona pia Ofisi ya Waziri Mkuu ikishughulikia masuala ya maslahi ya wafanyakazi katika sekta binafsi. Sekta binafsi, sekta mbalimbali zilionekana kwamba zina maslahi duni. Hata hivyo, Serikali imeshughulikia na inaendelea kushughulikia, lakini bado kuna changamoto kwamba, wafanyakazi wengi wanaofanya katika sekta binafsi bado masilahi yao ni duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunaamini Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kwamba inaboresha hayo maeneo na sekta binafsi inaimarika ili iweze kuwa ndiyo muhimili wa ujenzi wa Taifa letu na itoe ajira mbalimbali kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kutekeleza majukumu yote haya na katika kutanzua tatizo la ajira, ni wazi kabisa hii changamoto bado ni kubwa. Pamoja na kazi nzuri ambayo imefanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, bado ukienda mitaani kuna vijana wengi bado wanahangaika kutafuta ajira. Pia, hii inatupatia nafasi kwamba, sasa kuna haja ya kukaa chini na kuitafakari na kuona namna ya kuongeza mikakati zaidi ili kusudi tuweze kutatua tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi utaona vijana wengi sana wanahangaika. Ikitangazwa ajira, wanaoomba ni wengi kupitiliza. Wanaohangaika huko mitaani ni wengi. Sasa, maana yake ni lazima tuongeze mkakati wa kuimarisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya umma peke yake haitaweza kutatua hili tatizo la ajira. Hata hivyo, tumeona Serikali ya Awamu ya Sita imetoa ajira nyingi sana kwenye Mashirika, Wakala, lakini tumeona pia imeajiri watu wengi sana. Walimu wameajiriwa, watu wa afya wameajiriwa, lakini bado kuna sekta nyingine zinatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Baada ya kuliona hili tatizo, wameanzisha utaratibu wa kuhakikisha vijana wanaohitimu katika vyuo vikuu na vyuo vingine, waende katika Vyuo vya *VETA* ili waweze kupata maarifa ya kuweza kujiajiri. Hii hatua ni nzuri sana katika kuleta maendeleo. Kwa hili, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tumuunge mkono kwa kuwahamasisha vijana wetu waende kwenye vyuo vya *VETA* wakapate maarifa ili waweze

kuchangia katika ujenzi wa Taifa letu. Hii ni hatua madhubuti ya kukabiliana na changamoto ya ajira hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumeona katika Jimbo letu la Vwawa na katika Wilaya yetu ya Mbozi, tulikuwa na changamoto nyingi. Ni mkoa wa mwisho kuanzishwa katika utaratibu wa uanzishwaji wa mikoa. Tumeanzisha Mkoa wa Songwe, lakini tulikuwa hatuna vyuo vyovyote vinavyoweza kuwasaidia kuwapa maarifa, elimu na ujuzi vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali ya Awamu ya Sita imeanza ujenzi wa vyuo katika Mkoa wa Songwe. Chuo cha *VETA* kinajengwa, Chuo cha Walemavu kinajengwa, kwa kweli tunawapongeza sana. Pale Wilaya ya Mbozi kwenye eneo la Sasanda, kulikuwa na kambi ya vijana ambayo ina ekari zaidi ya 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile kambi bado tunaweza tukaweka mkakati na ikatumika katika kuwaandaa vijana ili kuweza kushiriki katika uchumi wa nchi hii. Ekari 700 ni nyingi, zinaweza zikazalisha, zikaongeza na tunaweza tukajenga hata vyuo vingine pale, na vikaweza kuwaajiri hata vijana wengi ambao wanakosa maarifa na ujuzi wa kuyaendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa ujenzi wa hivi vyuo. Hata hivyo, Chuo cha Afya najua kiko mbioni na wametutangazia kwamba kinakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, tumeona miradi ya barabara mbalimbali zimejengwa. Tunaona barabara ya kutoka Njiapanda ya Iyula kwenda mpaka Idiwili kilometa 21 wanajenga wanawake wa Tanzania. Barabara imechaguliwa, na wanawake wa Tanzania ndiyo wanaokwenda kujenga ili kuwajengea uwezo kiuchumi. Ni hatua nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi zinapojengwa ndiyo zinafungua uchumi. Zinafanya kila mahali sasa paweze kufikika na mazao ya wananchi yaweze kwenda sokoni. Hapo ndipo uchumi

unakuwa na ajira mbalimbali zinatengenezwa kwa wale wote wanaokwenda kufanya kazi. Kwa hiyo, hili ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona vituo vya afya vimefunguliwa na vimejengwa katika maeneo mengi. Pia, naipongeza Serikali imejenga vituo vya afya vizuri kwetu. Zaidi ya vituo vinne vimejengwa katika kipindi hiki. Sasa hivi tunapambana katika kuhakikisha tunapata watumishi wa kutosha, vifaa vya maabara na vifaatiba ili vituo vile viweze kutoa huduma zile ambazo tulikuwa tunazikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kazi nzuri, na zote hizi ni ajira kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la ajira hapa nchini na kupunguza umasikini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeona miradi ya maji mingi ambayo imetekelezwa katika maeneo mbalimbali. Tumeona mradi wa maji wa kutoka Ilomba unakuja mpaka Vwawa, Mradi wa maji kutoka kule Momba unakwenda mpaka Tunduma, unakuja mpaka Vwawa hadi Mlowo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tumeona soko la mazao, stendi ya Mkoa na Maghala ya *NFRA* yanajengwa. Zote hizi ni jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kutanzua umasikini, kukabiliana na ajira, kujenga uchumi mpana na kutatua matatizo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kazi nzuri hii tunaunga mkono hoja na tutaendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita ili tuweze kupata ushindi mkubwa na ninahakikisha kabisa kwamba, mwaka 2025 ushindi ni mkubwa, Mungu atubariki na naunga mkono. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga. Nilishamwita Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, atafuatia na Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninakushukuru sana. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kibali hiki cha kipekee kusimama kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kabla sijaendelea, nami naomba niunge mkono hoja ya bajeti ya Waziri Mkuu. Bajeti ni nzuri, lakini pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyoelezea bajeti na mwelekeo thabiti wa Serikali yetu ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama yetu, kwa kazi nzuri anayosaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa Jimbo langu la Ushetu, jimbo ambalo lina miradi mingi ya kimkakati. Kwa miaka minne ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ushetu peke yake tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 196 ambazo zimekwenda kwenye miradi mikubwa ya kimkakati iliyoshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, Jumah Aweso, alifika Jimboni Ushetu na aliwaona akina mama walivyokuwa wanateseka na ndoo za maji, aliona akina mama walivyokuwa wanalia. Shida ya maji katika Jimbo la Ushetu ilikuwa ni kilio kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa maji wa Ziwa Victoria uliokuwa katika Mji wa Kahama kwa zaidi ya miaka 19, lakini umekuja kutibiwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Jumah Aweso, kwa kazi kubwa ambayo umeifanya, zaidi ya shilingi bilioni 44 ambazo zimekuja kwa wananchi wa Ushetu, Mkandarasi yuko *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kazi anazozifanya za kuwapa wazawa, yaani kampuni za kitanzania ambazo zinafanya kazi vizuri sana. *SIHOTECH Engineering Company Limited,* ambayo inafanya kazi

katika Mradi huu inafanya kazi usiku na mchana katika kuchimba mitaro, kufukia mabomba, mabomba yanatandazwa. Hivyo, ni kazi kubwa inayofanyika kwa wananchi wa Ushetu. Napongeza sana kwa kweli, kazi kubwa imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata 11, Vijiji 54 vinakwenda kupata mradi wa maji, ambapo chini ya ardhi ya vijiji hivi, vitongoji na kata zake hazikuwa na mradi. Ushetu ina kata 20, naomba tu awamu inayokuja sasa kata hizi na vijiji vyake vinavyobaki viweze kukumbukwa pia katika kufikishiwa maji katika Mradi huu wa Maji wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kilimo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwa kinara wa ushirika. Alizunguka katika nchi hii ya Tanzania kuhamasisha ushirika uweze kuanzishwa. Hata hivyo, baadaye akabadilishiwa jina akawa Baba wa Ushirika. Nami niendelee kumwambia, sasa ushirika umeimarika. Mwaka 2019 alipokuja pale Shinyanga, aliita vyama vya ushirika vyote na warajisi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitoe shukrani za dhati sana kwake, alikuja kuigawa *SHIRECU* na akaagiza igawiwe *SHIRECU* na leo ikaenda kuzaliwa *SIMCU* (Chama Kikuu cha Ushirika Simiyu) ambapo kimekwenda kuwa chama bora na kupewa fedha na Benki ya Kilimo *TADB* zaidi ya shilingi 6,800,000,000/= na imenunua pamba safi kwa wakulima na kwa ushindani mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *Kahama, Cooperative Union,* mwaka huu pia nayo iliweza kupewa shilingi bilioni sita (Chama Kikuu cha Ushirika ambacho pia kilitoka *SHIRECU*), nacho kimefanya kazi kubwa. Vilevile, kimeongezewa fedha nyingine na Benki ya Kilimo, shilingi bilioni mbili ambapo imekwenda kuanzisha *oil mill* ili kuongeza thamani ya mazao yetu kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *MBCU* nayo imepewa shilingi bilioni 11.8. Vilevile, *CCU* – Chato nayo imepewa shilingi bilioni 8.9. Zaidi ya shilingi bilioni 39.6 zimetoka Benki ya Kilimo (Benki yetu inayohudumia wakulima) na zimepelekwa kuwahudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukuomba, Benki yetu ya Kilimo imefanya kazi kubwa sana kwenye kuimarisha ushirika. Imevichukua hivi vyama vikiwa na hali mbaya, na leo vyama hivi vimekwenda kuimarika na vimefanya kazi vizuri sana. Niendelee kuomba benki hii iendelee kuongezewa fedha ili iendelee kuwahudumia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ndugu yangu Mheshimiwa Hussein Bashe, amefanya kazi kubwa sana kwenye sekta ya kilimo. Leo anakwenda kuanzisha Benki ya Taifa ya Kilimo ambayo inazinduliwa tarehe 28. Ni mkombozi mkubwa sana kwenye sekta ya kilimo na vyama vya ushirika. Niendelee kuomba Mheshimiwa Waziri, tuimarishe mifumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ushirika ambao umeanzishwa na unafanya kazi vizuri sana, mfumo wa MUVU, mfumo huu unakwenda kuleta mapinduzi makubwa sana kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa mfumo huu uingie mpaka kwenye vyama vyetu vya ushirika vya pamba ili mkulima anapopeleka pamba yake kwenye *AMCOS,* akipima tu ni moja kwa moja mpaka kwa mrajisi wa vyama vya ushirika Tanzania ili aweze kuona Mkulima wa Simiyu, Mkulima wa Kishapu, Mkulima wa Ushetu na mkulima wa maeneo mengine nchini ajue kwamba kwenye eneo la ushirika wameuza nini na wamepata kiasi gani? Hata ule wizi mdogo mdogo uliokuwa unasemwa hapo nyuma, tayari tutakuwa tumeshautibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kwenye eneo la pembejeo na mbolea za ruzuku, amefanya kazi kubwa mno. Leo wakulima wa tumbaku ambao walikuwa hawajawahi kupata ruzuku, tayari hundi ya shilingi bilioni 13 imetolewa kwa wakulima. Ni pongezi nyingi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, masoko ya tumbaku yalikuwa yameshakufa. Masoko ya tumbaku hali ilikuwa mbaya, wanunuzi wote waliondoka. Leo tuna wanunuzi zaidi ya 15 katika nchi yetu ya Tanzania. Madaraja yameongezeka, wastani wa wakulima wa tumbaku hali ilikuwa mbaya sana, lakini leo wastani wa Kitaifa ni dola 2.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wamemalizia masoko pale kwa wenzetu wa Musoma. Madaraja ya tumbaku wastani wao ilikuwa ni dola 2.5, hali ilikuwa ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana uongozi wa vyama vikuu vya ushirika hapa nchini pamoja na warajisi wasaidizi wa vyama vya ushirika hapa nchini kwa kazi ambayo wanasimamia wakulima na kusimamia ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niendelee kuomba wachape kazi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, yuko pamoja nao. Waendelee tu kuimarisha vyama vyetu vya ushirika kwa sababu karibu 60% ya nchi yetu ni wakulima. Ili waendelee kuwaunganisha wakulima wetu waendelee kujua kwamba, dira ya ushirika wakati mwingine ndiyo maeneo ambayo watakuja kupata faida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, kwa upande wa barabara nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametupatia Ushetu zaidi ya shilingi bilioni 18. Tulikuwa na madaraja yaliyoshindikana toka uhuru. Leo tuna daraja letu la Mwabomba, mwaka 2024 wananchi wetu zaidi ya sita walikwenda na maji. Leo daraja lina shilingi bilioni 4.7 na linajengwa kiwango kizuri kwa zaidi ya mita 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tuna Daraja la Ubagwe ambalo nalo pia lilishindikana na lenyewe lina zaidi ya shilingi bilioni tano, tuna Daraja la Kasenga – Ulowa lina zaidi ya shilingi bilioni tano, Daraja la Ng'wande na lenyewe limepewa zaidi ya shilingi bilioni tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi sana kwa Wizara ya Ujenzi. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri aliyekuwepo, Ndugu yangu Mheshimiwa Bashungwa, alifika Ushetu na alijionea mwenyewe alipokuwa Waziri. Alishuhudia wananchi walipofurahi mapokezi yake baada ya mateso makubwa ya miaka nenda rudi kwa madaraja yale yaliyokuwa yameshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Wizara ya Ujenzi, tuna barabara yetu iliyowatesa wananchi miaka nenda rudi. Barabara inayotoka pale Nyandekwa – Kahama inakuja Uyogo ambayo ina kilometa 54. Naomba mwaka huu 2025/2026 wa bajeti angalau itengewe hata kilometa kadhaa ianze kujengwa taratibu kwa kuwa wananchi hawa wa Ushetu, hii barabara ndiyo kiungo chao kikubwa cha biashara na magari yao yanapita katika barabara hiyo, yanaleta mizigo katika Manispaa ya Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kupongeza sana upande wa umeme. Tuna mradi mkubwa wa *solar system,* ambao una zaidi ya shilingi bilioni 11.7. Nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dotto Biteko, hali ni nzuri na mradi wa mabilioni ya fedha umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, vijiji vyangu 112 tayari vina umeme na vitongoji tayari vimeanza kupelekewa umeme. Vile 15 tayari vimekamilika. Mheshimiwa Naibu Waziri, upande wa mafuta kwa kweli hongereni sana. Mafuta yanazidi kushuka bei, hali ya maisha ya Watanzania wanazidi kufurahia. Pongezi kubwa sana kwa usimamizi huu, endeleeni kusimamia na kuwasaidia Watanzania, endeleeni kumsaidia Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kazi mnayoifanya Waheshimiwa Mawaziri ni kubwa sana. Sisi kama Wabunge tunaendelea kuwapongeza sana, kwani kazi ni kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano kama Jimbo langu la Ushetu, ni jimbo ambalo liko vijijini na ni la wakulima. Kwa hiyo, mafuta yanapopanda bei, wananchi wetu wanapata shida sana. Hata hivyo, kwa kipindi hiki mafuta yanazidi kushuka bei na wananchi wetu wanazidi kufurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza sana Serikali kwa upande wa shule. Leo hii najengewa shule ya shilingi bilioni 1.6 ambayo ni shule ya vipaji maalumu. Pia, ni Mheshimiwa Rais huyu huyu ambaye amenipelekea Hospitali kubwa ya kisasa ya shilingi bilioni 3.5. Jengo langu la utawala zuri kabisa la shilingi bilioni tano limepelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hii 10% ambayo mmekuja kuiruhusu, sisi tunaruhusu. Mmeongeza kutoka vijana hawa ambao walikuwa wanaishia 35, leo mmekubali miaka 18 mpaka 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kundi hili la wanaume limesahaulika. Kama akina mama hawa tunawapa mikopo wote bila kujali umri, hili kundi nalo Wabunge tunapopita kule majimboni tunalalamikiwa sana. Tuwape tu na hawa wote waweze nao kupata mikopo kwa sababu ni kundi kubwa, lakini ni kundi ambalo ni tegemeo katika familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi hili ndilo unakuta linahangaika na ada, linagangaika kutibu familia, kundi hili ndilo kila kitu na shida ikipatikana nyumbani kundi hili linateseka. Naomba kwenye bajeti, kundi hili nalo liwekwe na liingie kwenye mikopo hii ya 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Halmashauri ya Ushetu, kwa mwaka huu peke yake, kwa vijana imetoa vikundi 85 zaidi ya shilingi 1,036,000,000 wamepewa hawa vijana wetu na akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, lakini pia niendelee kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cherehani. Nilimwita Mheshimiwa Hassan Seleman Mntenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar na Mheshimiwa *Engineer* Leonard Chamriho.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitangulize shukrani kwako. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kupata fursa ya leo kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi ambayo anaifanya kwa ujumla kwenye nchi yetu pamoja na jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake wote kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kutuunganisha na kutusaidia kupitia kwenye majimbo yetu. Mungu ambariki sana na ampe maisha marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ambao tunatoka ukanda huu wa kusini, lazima tuishukuru Serikali. Tunaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia, kwa vigezo. Kwanza, kwenye jimbo langu wakati naingia 2020 kulikuwa kuna shida kubwa sana ya maji. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweza kutupatia zaidi ya shilingi bilioni 3.4 za kujenga chujio pale na tukaweza kusafisha maji katika Mji wa Mtwara yakiwa salama na safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mtwara Mjini, ni jimbo ambalo lilikuwa na uhaba wa shule za sekondari takribani zaidi ya kata tisa. Hapa ninapozungumza, katika kata tisa, tumepatiwa shule za sekondari za mfano tatu, na shule ya moja msingi. Kwa hiyo, tunatoa shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza uchumi wa nchi, lazima tuwe na viwanda ndani ya nchi. Tunapozungumza Kanda ya Kusini, Mtwara na Lindi tuna malighafi ya aina nyingi sana. Hata hivyo, kwa suala hili naiomba Serikali, sasa kwenye mipango watusaidie kutuletea viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunaomba sana viwanda? Tumezungumza kuhusu ajira za vijana wetu na vijana wetu wengi

wanamaliza vyuo mwaka hadi mwaka, nao wanategemea ajira. Tukiwa tuna viwanda vya kutosha, nadhani suala la ajira litakuwa ni ndoto kwetu kulizungumzia kila mara tunaposimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza tena Rais, mwaka 2024 tulipatwa na mafuriko; barabara yetu ya Mtwara – Kibiti - Lindi ilipata hitilafu kubwa sana ya kuvunjika kwa madaraja. Mheshimiwa Rais alitupatia fedha shilingi bilioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa madaraja yale. Pia, tuna imani kabisa, mpaka kufika kufika mwezi wa Tisa au wa Kumi madaraja yale yatakuwa yamekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, barabara hii imejengwa kwa muda mrefu sana, na kujenga kilometa moja barabara ya lami, *standard* inawezekana tukajenga kwa shilingi bilioni 1.4 na kuendelea. Ikiwezekana Serikali itutafutie fedha zaidi ya shilingi bilioni 800, tunaweza tukatengeneza barabara ya lami kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi na Mtwara, ikawa shida yetu ile ya barabara imekwisha, kwa sababu shida ya kwanza ya madaraja Mheshimiwa Rais ameshatoa fedha, itakuwa hatuingii tena kwenye madaraja. Kwa hiyo, tutajenga barabara ambayo itakidhi mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunazungumzia shida za maji na mara nyingi Serikali imekuwa inatueleza kwamba sasa twende kwenye maji ambayo yanastahili ambayo ni maji ya kutoka kwenye mito mikubwa. Tunao Mto Ruvuma ambao unaweza ukatuletea maji katika Mkoa wa Mtwara na Lindi bila shida na maji yakawa mengi zaidi. Tuiombe Serikali, muda umefika sasa wa chanzo hiki cha maji ya kutosha tuweze kupatiwa fedha ili tupate maji ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishukuru Serikali kuhusu masuala ya umeme. Mtwara ilikuwa ni sehemu ina shida ya umeme takribani kwa siku umeme ulikuwa unakatika zaidi ya mara 30, lakini sasa hivi shida ya umeme imeisha. Tunamshukuru sana Rais na Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwani tayari tuna bandari pale ambayo ina uwezo mkubwa. Tumetumia zaidi ya shilingi bilioni 156 kuitengeneza Bandari ile, lakini ilikuwa haifanyi kazi hasa kupitisha mazao ambayo tunalima kwenye Mkoa wa Mtwara kama vile korosho, mbaazi na ufuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekaa zaidi ya miaka mitatu bandari ile haipitiki na wala haifanyi shughuli za kimazao. Tunamshukuru tena Mheshimiwa Rais, tulipomlilia juu ya kuitumia bandari yetu, alisimama nasi na akasema Bandari ya Mtwara itafanya kazi; na kweli Bandari ya Mtwara sasa inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunasema bandari yetu tulikuwa tunaipigania ifanye kazi? Sasa hivi vijana wengi wa Mkoa wetu wa Mtwara au majimbo yaliyo karibu na bandari wanafanya shughuli zao za halali pale bandarini na wanapata fedha na wanajiendeleza. Pia, hata uchumi wa kibiashara katika jimbo langu sasa hivi umekuwa mzuri sana kutokana na bandari hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali. Tunao mpango na hii ninaishukuru sana Serikali kwamba tayari imeamua sasa kama kutujengea hili Daraja la Mto Ruvuma pale Kilambo. Daraja hili na wenzangu tulipiga kelele sana takribani miaka mitatu mfululizo tukiiomba Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwamba tayari imeshaingiza kwenye mpango. Kwa hiyo, ujenzi wa daraja lile utaleta manufaa makubwa na uchumi mkubwa kwa Mkoa wa Mtwara. Mara nyingi nimekuwa nawaeleza hapa Waheshimiwa Mawaziri na muda ule walikuwa hawanielewi kwa nini nazungumzia daraja lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mikoa nane ya Mozambique ambayo ni mikubwa na ina matajiri. Katika mikoa ile minane, kutoka kwenye mkoa wa mwisho Pemba kuelekea Beira - Nampula ambako wanatumia ile Bandari ya Nampula

wanatumia zaidi ya kilometa 1,800 au 1,900 lakini kutoka kwenye mkoa wa mwisho tunaouzungumzia kuja Mtwara watatumia kilometa 800. Kwa hiyo, watatumia Bandari ya Mtwara yenye kilometa 800 kutoka kwao wanapoishi na hivyo bandari yetu itafanya kazi na tutapata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kiuchumi ninalozungumzia la korosho. Niendelee kumpongeza Mheshimiwa Bashe, Waziri wa Kilimo. Kwa kweli sisi watu wa Mtwara tunampa sifa zake zote. Korosho Mtwara ilikuwa haina thamani kwa sababu kulikuwa kuna wahuni wanachezea zao la korosho. Mheshimiwa Bashe alisimama akaingilia zao la korosho na kuondoa kitu kinachoitwa *box* ambacho wahuni waliweka mle. Sisi tunawaita wahuni kwa sababu walikuwa wanawaibia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka kwenye shilingi 1,800/= mpaka shilingi 1,700/= kwa kilo; mwaka huu uliopita tumeuza korosho kwa shilingi 4,300/= na kuendelea. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza kuhusu suala la kilimo, tayari *Sulphur* iko kwenye ma-*godown*. Yaani hatuzungumzii shida ya *Sulphu*r kwenye zao la korosho, tunamshukuru sana Rais, tunamshukuru Mheshimiwa Bashe kwamba kazi hii tunaiomba iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo nataka niishauri Serikali. Hizi halmashauri ziko tofauti. Ziko halmashauri zina uwezo wa kukusanya mapato zaidi ya shilingi bilioni moja, bilioni mbili au bilioni tatu, lakini ziko halmashauri zinakusanya zaidi ya shilingi bilioni 60 kwa mwaka. Sasa nini ninachotaka kukizungumza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko migao ya Serikali ambayo inatoka kupitia kwenye fedha za Serikali. Hebu tuangalie kwamba ziko halmashauri ambazo kwa kweli ziko nyuma kimaendeleo na halmashauri hizi tufike mahali sasa Serikali izi-*boost* baada ya kuachana na wale wenzetu ambao sasa hivi wamekuwa ni matajiri na wana fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ningekuwa na uwezo kwenye halmashauri yangu kupata shilingi bilioni 60 za makusanyo kwa mwaka, ningekuwa niko mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaishauri Serikali kwamba iangalie kwenye huu mfumo na hasa nataka kuzungumzia fedha za tozo za barabara. Tukikubaliana na Serikali tukasema kwamba kuna halmashauri zaidi ya 10 kwenye uwezo wa fedha wanaweza kujitegemea, basi hizi tozo za fedha za barabara za *TARURA* inawezekana baadhi ya halmashauri zikapiga hatua sana kwenda kutengeneza barabara kwenye eneo husika ili tuondokane na ile adha inayotukuta kila mwaka kutengeneza barabara za moramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unatumia zaidi ya shilingi milioni 200 kukwangua barabara kilometa 70 au kilometa 80 na mvua zikishanyesha, barabara ile imeharibika. Kwa hiyo, kila mwaka mtatumia shilingi milioni 100 au 200 kwenda kuburuza zile barabara. Kwa nini tusifike mahali tukasema tuna kilometa hapa zaidi ya 15, kilometa hizi bajeti yake iende tukaweke lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani baada ya miaka 10 itakuwa hatuwezi kupita tena kwenye barabara hizo kwenye *maintenance*, tutakuwa fedha zile tunafanyia jambo lingine lakini….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umeisha sasa Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja.

**MWENYEKITI:** Hitimisha.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo la ajira. Hivi karibuni vijana wetu walikuwa wanahitajika kwenye usaili Jeshi la Zimamoto. Kitu ambacho kimetokea na ni

kitu ambacho ni hatari sana, wanakwenda wale vijana pamoja ni sheria, sikatai ni sheria, wanapimwa ufupi au urefu. Wakishapimwa pale wanaambiwa wewe bwana una mita tatu haustahili kabisa kuwa kwenye Jeshi la Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twendeni tutafute lugha nyingine nzuri kwa sababu hao wafupi wameumbwa na Mwenyezi Mungu na kama wameumbwa na Mwenyezi Mungu ni vijana wetu, tumewasomesha, na wana elimu. Watafanya kazi wapi? Kwa hiyo, nawaomba sana, hili nalo tuliangalie, ni bomu ambalo linatujia. Sisi wenyewe hatujui kama hili ni bomu tunalitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Amar na Mheshimiwa *Engineer* Chamuriho atafuatia baada ya hapo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hii hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, naunga mkono hoja kwa sababu hii ndiyo hoja inayohusu maslahi ya Wabunge na maslahi ya watumishi wa Bunge. Kwa hiyo, hii ni hoja yetu sisi kama Wabunge, na ninaiunga mkono moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa humu, tumeona sifa za watu wengi. Mimi niwapongeza Mawaziri wote walio chini ya Waziri Mkuu na Mawaziri wengine tunafanya nao kazi. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, tunafanya naye kazi, Mheshimiwa Dorothy tunafanya naye kazi, lakini nampongeze sana Mheshimiwa Lukuvi. Amekaa Bungeni humu kwa muda mrefu, amekuwa mzee wa Bunge, ametushawishi mambo mengi sana ametushauri, tunamwombea kwa Mungu aendelee kuwepo, aendelee kutushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Waziri Mkuu, watu wengi mnakaa humu ndani, lakini sijawahi kuona, unakaa na mwanadamu mstaarabu kama Waziri Mkuu wa sasa hivi tuliyenaye. Ni mstaarabu mno yaani. Ni mchapakazi na mstaarabu, anasikiliza kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nikawa nasikiliza maneno maneno; unajua bwana, Waziri Mkuu sasa amemaliza vipindi viwili. Akienda huku sasa, akiwa Mbunge, anafanyaje kama siyo Waziri Mkuu? Kwani kuna hoja gani? Mbona tumeona watu wengi tu! Tumeona Mzee Malecela, tumeona Marehemu Mzee Lowassa wanakuwa Mawaziri Wakuu na wanakaa humu ndani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu arudi Bungeni. Habari ya vyeo, Mungu atajua. Yeye arudi Bungeni, ni mstaarabu mno. Mtu wa namna hii ambaye anafanya kazi usiku na mchana, amekuja kwangu pale mara tatu. Ameshaenda kila mahali na kila jimbo la Mbunge ameshaenda. Tunamwomba arudi Bungeni, tunamwombea huko anakotokea wamrudishe Bungeni, tukae pamoja naye ili asaidie hii nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu amepita vipindi vigumu sana. Alikuwa anafanya kazi na Marehemu Dkt. Magufuli, amekuja kwa Mama, amefanya naye kazi amemwonyesha kila mahali. Amemsaidia Mama kufanya kazi, nchi iko salama. Leo nchi iko salama kwa ajili ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia mimi sijui namfananisha na nani? Kwa sababu watu wengi mnajua mambo ya mpira humu ndani. Hakuna kitu kigumu duniani kama kupewa pasi halafu ukashindwa kufunga. Ma-*forward* wengi wanalaumiwa, wanapewa pasi hawafungi, lakini mama kapewa pasi ya Bwawa la Nyerere, kapiga goli; kapewa pasi Ikulu haijajengwa, kaijenga yote imeisha; kapewa Mji wa Magufuli, kapiga goli; kapewa madaraja, kapiga yote; kapewa ndege, zinaendelea. Hivi pasi gani ambayo hakufanya? Pasi zote alizopewa Mama, kafunga; sasa tunamtaka nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nyingine alikuwa anajitangulizia mwenyewe na anaenda kufunga mwenyewe. Kwa mfano, sekondari za wasichana zilizojengwa kila mkoa kapiga pasi mwenyewe, kakimbia mwenyewe, kufunga. Anajijua Mama ametokana na jinsia ya kike, anatengeneza mazingira watoto wa kike waendelee kusoma. Kwa hiyo, kapiga pasi yeye mwenyewe. Katupa hela kwenye majimbo shilingi milioni 500; bilioni ngapi kwenye mambo ya *TARURA;* amefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaweza kuwa Wabunge, unaweza kuwa Rais, unaweza kuwa kila mtu, lakini Mungu ndio anapanga mpango wake. Katika nchi yetu Mungu alimtoa Julius Kambarage Nyerere huko Musoma akampa Urais wa nchi hii akatuongoza miaka 24. Tukaungana na Zanzibar, Rais Nyerere alitoka upande wa pili wa nchi wa Tanzania Bara. Katikati hapa Mungu huyu huyu ametuleta Samia, huku tunamwita Mwalimu Nyerere Baba wa Taifa, Samia katokea upande wa pili wa Zanzibar amekuwa Rais na ni Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nchi hii Mungu ndio anaipenda, kaleta baba akawa Rais, akaleta mama akawa Rais upande wa nchi. Sasa sisi ni nani kupingana na Mungu? Kwa hiyo, tukubali kwamba Mama miaka hiyo inayokuja ni ya kwake. Kwanza nashangaa, kwani ana upinzani? Maana yake ndiyo ameshapita. Sisi ndiyo atuhurumie huko aliko, lakini yeye tayari kura zilishajaa. Kwa hiyo, tunamwombea Mama, Mungu amlinde aendelee kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingi imeletwa Bunda lakini mradi wa Hospitali ya Wilaya ya Bunda juzi tumepewa shilingi milioni 680. Tunaomba Waziri Mkuu aje akafungue hospitali yetu ya Bukama angalau watu wetu waone kwamba hii hospitali sasa inafanya kazi vizuri. Kuna Bwawa la Skimu la Mariwanda, namshukuru sana Mheshimiwa Bashe, ametoa fedha za kwenda kukarabati lile Bwawa ambalo lilikuwa limebomoka, sasa ametoa fedha kwenda kulikarabati, wanaenda kulitangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Bwawa lingine ambalo ni jirani yetu, tunafanya kazi ya Bwawa Bunda Mjini na Bwawa linaitwa Kisangwa. Wametoa mkandarasi akaenda kulikarabati, tunashukuru wote walioshiriki katika kusaidia hilo jambo kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwenye upande wa umeme. Huwa najiuliza sana, hivi kwa mfano mimi nina vitongoji 310 ambavyo vimebaki havijapata umeme, hatuna hela za kutosha za kupeleka vitongoji vyote. Hivi kwa nini tusiende Benki ya *CRDB* au Benki ya *NMB* au Benki ya Azania tukachukua ile tozo ya umeme inayotoka kwenye mafuta tukawapelekea *CRDB* au *NMB* tukawaambia tupeni fedha tujenge vitongoji vyote hivi, nyie mtakuwa mnalipwa na umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hii nayo inahitaji akili gani? Hatuna fedha, lakini tuna mapato ya kila siku. Kwa nini tusifanye hivyo? Sasa kwangu naomba mfanye *pilot area,* mtuletee fedha kutoka *CRDB,* watu wapewe umeme, walipe kwa kupitia mafuta? Kwa hiyo, naomba hili nalo lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu za msingi nyingi zimeoza na siyo nzuri sasa hivi. Tumefanya kazi kubwa sana kwenye sekondari, lakini shule za msingi, kwangu kuna shule inaitwa Masaba, yaani ni mbaya kuliko kawaida. Kuna Masaba, kuna Salama A na B, kuna Shule ya Nyang'aranga, kuna shule ya Songambele, kuna shule ya Chamtigiti; karibu zote na shule nyingine kama 15 nimeshapeleka TAMISEMI wazifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga sekondari nyingi. Kuna sekondari ya Tingirima imejengwa, lakini bado kuna maabara ya *Physics,* maabara ya Kemia na maabara ya *Biology* hazijatengamaa. Jengo limejengwa, limepigwa paa, lakini ndani hamna kitu kinachoendelea, na Serikali imetoa shilingi milioni 870.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, watu wa TAMISEMI wanaohusika waende pale, walishafanya *evaluation* wakamalizie yale majengo ya sekondari ambayo tulitoa shilingi

milioni 480 na majengo hayakukamilika. Pia, waongeze walimu kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Sekondari ya Sanzati wananchi wamechanga shilingi milioni 120, Serikali ika-*double* milioni 140, lakini sekondari ipo, majengo yapo, madarasa hayajaongezeka, jengo la utawala halipo, na vyumba vya maabara havipo. Tunaomba Serikali iende kwenye maeneo hayo isaidie kuleta maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunda ina barabara nyingi, lakini namshukuru Mheshimiwa Rais, Barabara ya kutoka Nyamuswa inaenda Bunda - Buramba imekamilika, ni ya lami. Pia, kuna Barabara ya Makutano - Butiama – Sanzati imekamilika, na ni ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya kutoka Sanzati kwenda Nata imekuwa tatizo. Naiomba Serikali, haiwezekani mkandarasi akaenda akaweka lami kwenye mchanga tu halafu akapotea na imegharimu shilingi bilioni 46. Tunaomba wanaohusika tafadhali, tafadhali sana, nendeni mkamalizie ile barabara ambayo iko 50% na imebaki 50% kuimalizia. Naomba kwenye Serikali waende watusaidie kujenga hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wote; nampongeza Waziri wa Fedha, kwa kweli tunamwona mara yuko Ufaransa, Ujerumani anahangaika. Jamani watu wanaofanya kazi tuwapongeze. Mawaziri wa sasa hivi, wengi wanafanya kazi wengi sana. Kwa mfano, ukimchukua Mheshimiwa Bashe anavyojitolea. Bahati nzuri Mama amewapa uhuru wa kutosha wa kufanya kazi zao, wakishindwa ni wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso sasa ndio usiseme. Yaani Mheshimiwa Aweso huyu basi tu, yeye anachoniudhi ni kwenda kuisimamia Simba inashinda. Hiyo ndiyo shida yake tu basi, lakini mengine anafanya mambo mazuri sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso amenipa mradi wa maji wa Ziwa Victoria kutoka Butiama kuja Nyamuswa na wananchi wanashukuru. Siku akifika Bunda ajiandae tu na gari ya zawadi, atabeba mbuzi, ng'ombe, na kila kitu. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Mawaziri wote wanaohusika, wanaofanya kazi nzuri ya Serikali. Pia, namshukuru Mama, namshukuru Waziri Mkuu na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere. Nimwite sasa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Leonard Chamuriho.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha mimi kunipa afya njema na kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imesheheni matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kwenye nchi hii ikiwemo kutoa fedha nyingi sana kwenye miradi ya maendeleo ikiwemo Wilaya ya Nyang'hwale ama Jimbo la Nyang'hwale, ambapo tumeweza kupokea fedha nyingi sana kwenye miradi ya maendeleo. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja na sasa nianze kusema yafuatayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweza kutoa fedha nyingi sana kwenye miradi mingi, lakini nitaisema miradi michache ikiwemo Sekta ya Elimu. Wilaya ya Nyang'hwale tumeweza kupokea fedha nyingi sana kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari na shule za msingi pamoja na ujenzi wa

nyumba za walimu, matundu ya vyoo na miundombinu mbalimbali. Mama Samia ameweza kutoa fedha nyingi sana kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya kisasa yenye *tiles,* yenye madirisha mazuri ya ku-*slide*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ameweza kutoa fedha nyingi sana kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo. Leo hii watoto na vijana wetu wanaenda kwenye vyoo vya kisasa. Kwa kweli tunampongeza sana kwa kutoa fedha nyingi sana kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kwenye upande wa sekta ya elimu, iweze kutoa fedha za kuendeleza majengo ama maboma ambayo yalijengwa na wananchi, yamekaa kwa muda mrefu, vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na vyoo. Naiomba na kuishauri Serikali iweze kutoa fedha kwenye bajeti ya mwaka huu ili iweze kukamilisha hayo ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliweza kutupa fedha nyingi sana. Jimbo la Nyang'hwale tulikuwa na shida ya maji, Mama Samia ametupunguzia adha hiyo. Hivi nilivyosimama na kuongea hapa, ni zaidi ya 70% ya vijiji vya Jimbo la Nyang'hwale tunapata maji kutoka Ziwa Victoria na kwenye vyanzo vya visima virefu ambavyo tumechimbiwa kwa zaidi ya 70%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Serikali itenge fedha kwenye bajeti hii iweze kutupatia. Tuliomba zaidi ya shilingi bilioni 4.5 ili tuweze kusambaza mabomba na kukamilisha zoezi la usambazaji wa mabomba kwenye kata 15 na vijiji 62 ndiyo tutakuwa tumekamilisha. Itupatie hizo shilingi bilioni 4.5 tuweze kukamilisha changamoto hiyo ya maji kwenye Jimbo la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweza kutoa fedha nyingi kwenye miradi mbalimbali ikiwemo umeme. Hivi ninavyoongea Jimbo la Nyang'hwale lina vijiji 62. Vijiji vyote 62 vimeshafikiwa na umeme. Tuna vitongoji 273, mpaka sasa hivi

ninavyoongea vitongoji 88 vina umeme na vitongoji 15 mkandarasi yuko *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, hawa wakandarasi wasimamiwe vyema na naishauri Serikali iweze kuongeza fedha ili sasa tuweze kupunguza vitongoji vingine ambavyo vimebaki ili tuweze kumaliza vitongoji vitakavyokuwa vimebaki angalau hata ndani ya miaka mitatu au minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweza kutoa fedha nyingi kwenye miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa *VETA*. Tunao ujenzi wa *VETA* kwenye Wilaya ya Nyang'hwale, lakini ujenzi huu unakwenda kwa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali na kuishauri iendelee ku-*pump* fedha ili tuweze kukamilisha kwa wakati majengo hayo ili vijana wetu waingie kwenda kujifunza ufundi stadi, kwa sababu vijana wengi sasa hivi wako mtaani hawana kazi na hawana ujuzi. Napenda sana kuishauri Serikali na kuiomba iweze kutoa fedha kwenye bajeti hii tuweze kukamilisha hayo majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Kamishna wa Kupambana na Kadawa Kulevya. Kamishna huyu kwenye bajeti hii nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba anaendelea kupambana na wameweza kukamata madawa mengi. Tani za dawa za kulevya zimeshikwa na ameweza kukamata na kuchoma mashamba mengi ya bangi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hiyo anayoifanya ya kuokoa vizazi vyetu na vijana wetu na nguvu kazi, ni kazi kubwa, naomba aongezewe fedha ili aweze kupambana na kuzuia. Leo hii vijana walio wengi wanavuta bangi na kutumia dawa. Kwa kweli kazi kubwa anaifanya. Analalamika; mimi niko kwenye Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, alikuja Kamishana akaelezea kwamba ana upungufu wa fedha na vitendea kazi na nguvu kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kupitia bajeti hii Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuidhinishiwa ili aweze kumpa Kamishna wa kupambana na dawa za kulevya aweze kupambana nazo vizuri dawa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi tena kuipongeza na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri. Mimi nasema kama mwakilishi wa wananchi wa Nyang'hwale, Mama Nyang'hwale anatudai. Tunasema, Kazi na Utu, Tunasonga Mbele 2025 Nyang'hwale kura nyingi kwa Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amar. Nilimwita Mheshimiwa *Engineer* Leonard Chamuriho, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu na Mheshimiwa Joseph George Kakunda na mchangiaji wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja muhimu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuongoza vizuri hasa kwa kutumia falsafa zake za *4R's.* Vilevile, kwa kuratibu na kuhakikisha kwamba kuna maendeleo endelevu ya mipango ambayo tumejiwekea wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uratibu mzuri wa shughuli za Serikali na kwa usimamizi mzuri wa mipango ya maendeleo ambayo ndiyo itakuwa msingi wa mchango wangu wa leo. Tatu, kwa kuandaa bajeti nzuri ambayo itahakikisha kwamba kuna uendelevu wa hiyo mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kuwapongeza wasaidizi wa Waziri Mkuu kwa kutengeneza bajeti hii nzuri. Kwanza, Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko na Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa William Lukuvi pamoja na Naibu wake na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete pamoja na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika uendelezaji wa mipango ya maendeleo katika hiyo hotuba yake ambapo rejea ya kwanza nakwenda kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2025/2026. Nikiangalia pale kwenye ukurasa wa 42 kuna vigezo vya kuchagua vipaumbele vya bajeti yetu ya mwaka huu ambavyo vimewekwa ambapo nikiangalia bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imevifuata kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nikiangalia katika mpango huo huo ukurasa wa 59, kuna kigezo cha kuendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele katika sekta mbalimbali. Kuna Sekta ya Ujenzi ukurasa wa 59, kuna ya miradi yenye lengo la kuchochea maendeleo ya uchumi, pale kuna sekta ya uchukuzi, pia ukurasa wa 60 hivyo hivyo kuna sekta nyingi ambazo zimewekwa pale ambazo zimepangiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana bajeti hiyo ya Waziri Mkuu kwa sababu imehakikisha kwamba kuna uendelevu wa mipango ya maendeleo. Mipango mingi imepangwa pale lakini nitatoa mifano michache ambayo itadhihirisha hilo na kuonesha ni wapi pa kutilia nguvu ili tuweze kuendelea zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aya ya 39, kuna orodha ndefu ya hiyo mipango ambayo itatekelezwa kulingana na bajeti hii, nami ninampongeza kwani orodha hiyo kama itatekelezwa kama ilivyopangwa, kweli tutakuwa tumesonga mbele sana katika mwaka huu ambao bajeti hii inakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kutoa mifano michache ambayo nitaisisitiza, nikiangalia aya ya 42 hadi ya 43 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapo, amejadili reli yetu ya *SGR*.

Ukiangalia katika vipande vyote ambavyo vimetajwa pale Dar es Salaam – Morogoro, Morogoro – Makutupora, Makutupora – Tabora, Tabora – Isaka, Isaka – Mwanza na Tabora - Kigoma utagundua kwamba maendeleo ni mazuri na hiyo yote inatokana na usimamizi mzuri ambao unaratibiwa na ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hilo tumpongeze na tunasema kwamba aendelee katika usimamizi huu mzuri ili katika mwaka husika malengo ambayo yamepangwa yaweze kufikiwa. Katika aya ya 44 mpaka 47 ameongelea uimarishaji wa huduma za bandari hasa ya Dar es Salaam. Ukiangalia pale kitu ambacho kimetajwa kwanza kuna uboreshaji ambao unaonesha dhahiri kwamba umezaa matunda na hiyo yote ni kwa sababu ya usimamizi mzuri wa hayo yaliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye ubebaji wa makasha, ameorodhesha pale kwamba tumefika makasha 687,000 kutoka makasha 670,000 katika miezi nane ya mwaka huu ambalo ni ongezeko kubwa. Hii yote ni kwa sababu ya usimamizi mzuri unaofanywa na ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ukienda kwenye meli zinazosubiri nangani, zimepungua kutoka 30 hadi tatu. Ukienda kwenye muda wa kuhudumia meli, umetoka kwenye siku 10 hadi siku tatu. Ukienda kwenye mapato ya *TPA,* yamepanda kutoka shilingi bilioni 850 hadi shilingi trilioni moja katika muda wa miezi nane. Hii yote imetokana na usimamizi mzuri na bajeti hii ambayo imepangwa ilenge katika kusimamia maendeleo haya ili yaweze kuboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye aya ya 48 mpaka aya ya 50, hapa ameongelea miundombinu ya ndege hasa *ATCL*. Hapa ameonesha kwamba ndege zimeongezeka hadi kufikia ndege 16 na nchi ambazo ndege zinakwenda mpaka sasa hivi ni 16. Huo ni uratibu mzuri kabisa, na tunakokwenda zinapangwa kuongezwa na ameonesha kabisa kwamba mwaka huu tunaweza tena tukaongeza *destination* nyingine tukaenda Kinshasa. Abiria wameongezeka na mizigo imeongezeka. Hivyo,

bajeti inayopangwa hapa ilenge katika kusimamia maendeleo haya ili yasirudi nyuma, tuendelee kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, aya ya 51 ameongelea madaraja makubwa. Huko nyuma tulianza na madaraja makubwa Tanzanite, Wami na Kigongo Busisi. Unakuta haya yamekamilika na tunakoelekea hayajaisha mengine mapya. Tunaomba basi katika kitengo chake hiki cha usimamizi na ufuatiliaji miradi, bajeti hii iweze kusimamia maendeleo haya ili tuweze kuyaendeleza na tusirudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imejaa miradi mingi ambayo inaonesha wazi kwamba ufuatiliaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu ni mzuri. Tukienda kwenye ujenzi na ukarabati wa meli tukianzia Ziwa Victoria, tulianza na MV Victoria na MV Umoja ambazo sasa hivi zinafanya kazi vizuri kule na hiyo yote ilitokana na usimamizi wake mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka hata wakati wanajenga kule chelezo walikuwa wanatembelea pale mara kwa mara. Kwa hiyo, sasa tuna MV Mwanza, Hapa Kazi Tu iko 98%. Nayo tunaomba basi isimamiwe vizuri ili katika hiyo mipango iliyopangwa iweze kwisha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika Ziwa Tanganyika kuna mipango mizuri ya meli za kukarabati MV Sangara, MV Liemba pamoja na ujenzi wa meli mpya. Hivyo, tunaomba kitengo chake hiki cha usimamizi kiweze kujikita hapo twende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi ambao unaonesha wazi kwamba usimamizi huo unakwenda vizuri ni mradi wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere. Mwendelezo wa usimamizi umelipa, na sasa hivi bwawa hilo limekamilika, na huo ni mfano mzuri wa usimamizi ambao unaendeshwa na ofisi yake. Kwa hiyo, bajeti hiyo iende vizuri katika usimamizi huo. Sasa ukienda kwenye randama ya Ofisi ya Waziri Mkuu ukurasa wa 12.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Injinia muda wako umeisha, ninaomba uhitimishe.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja nihitimishe. Katika Fungu 37, inaonekana kabisa kuna Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji Serikalini. Kitengo hicho ndicho ambacho ni jicho la kuangalia maendeleo haya. Hivyo, tunaomba kitengo hiki kiimarishwe na tuhakikishe kwamba bajeti inapatikana ya kutosha ili maendeleo haya yaweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda. Simwoni Mheshimiwa Kungu, nikuombe Mheshimiwa Joseph George Kakunda uendelee.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, nami niweze kuchangia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa kweli nianze kwa pongezi za dhati, Waziri Mkuu ametoa hotuba ambayo imetathmini angalau kwa miaka ya karibuni kuhusu utekelezaji wa Serikali na ametathmini utekelezaji wa mwaka huu wa fedha 2024/2025, lakini ametoa maono kwa utekelezaji wa mwaka ujao wa fedha 2025/2026. Nampa hongera sana, hotuba yake Watanzania wameipokea na kuielewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Julai mwaka 2002 huko Durban Afrika Kusini, Wakuu wa Nchi za Afrika *(AU)* walipokaa walikubaliana kuwa na azimio moja kubwa la nchi zote za Afrika kuwa na utaratibu wa kujifuatilia na kujitathmini kuhusu utekelezaji wa demokrasia na utawala bora na pale Wizara ya Mambo ya Nje kiliundwa kitengo maalum chini ya Idara ya Afrika ambacho kilikuwa kinasimamia utekelezaji wa azimio hilo ndani ya nchi. Sekretarieti ya *APRM* ilianzishwa pale Mambo ya Nje ili kumsaidia Mheshimiwa Rais ambaye alikuwa *signatory* kwenye ule Mkutano wa Durban kufuatilia utekelezaji wa lile azimio - Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kweli kila mwaka tulikuwa tunaandaa taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa hilo azimio. Sasa nirejee tu kwamba *AU* iliandaa mwongozo kwa kila nchi kujitathmini, lakini huo mwongozo ulikuwa ni kitabu kikubwa sana chenye kurasa zaidi ya 300, kila nchi ilikuwa inatumia huo mwongozo ili kujitathmini kwamba imefikia hatua gani katika utekelezaji wa demokrasia na utawala bora wa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia waraka wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, azimio hilo ameliboresha sana kwenye zile *4R's*. Kuridhiana, Kustahamiliana, Kufanya Mageuzi Muhimu katika Nchi na Kutoa Wito wa Kuijenga Nchi Upya kwa Kushirikiana, hizo ni *4R's*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kwamba Wabunge wote hapa pamoja na wananchi na viongozi wa chama tumekuwa tukimpongeza Mheshimiwa Rais kwa waraka ule ambao ni mwongozo na maono ya namna ya kuboresha lile azimio la mwaka 2002, utakubaliana nami kwamba maono hayo ya Mheshimiwa Rais yalihitaji sekretarieti ambayo ingeweza kumsaidia kufanya uratibu wa jambo hilo ambalo ni kubwa sana na linasifiwa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti hiyo haipo, ninatoa wito kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu aongoze kuundwa kwa sekretarieti ya *4R's* ambayo itasaidia sana kuweka vizuri utekelezaji kwenye kila sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Mheshimiwa Rais kunyoosha mkono wa upendo kwa vyama vyote vya siasa kupitia hizo *4R's* lakini na upendo wake kwa wananchi wa Tanzania wamejitokeza wananchi wenzetu ambao wamekuwa wanabeza kazi za Mheshimiwa Rais, na wanatumia maneno ya kejeli na ambayo hayana heshima. Wakati mwingine wamekasirika utafikiri wameudhiwa huko nyumbani kwao na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani jambo hili ambalo linaenda kutaka kumomonyoa mshikamano wetu kama Taifa ni

mambo ambayo inatakiwa tuwe *serious* katika kuyashughulikia. Siyo mambo ya kuangalia kwa kuyadharau. Katika nchi nyingine mambo yalianza kumomonyoka hivi hivi mpaka wakapata matatizo. Tusije tukakubaliana na msemo wa Kiswahili wa fadhila ya punda ni mateke, halafu tukaacha hapo hapo, lazima tuwe *serious.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natoa wito, Wabunge na viongozi wote wa CCM tusimame imara katika kumtetea na kumlinda Mheshimiwa Rais dhidi ya njama za hovyo kama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, siyo kwa hilo tu, ila kwa mambo ambayo ameyafanya kwenye jimbo langu na majimbo ya Wabunge karibu wote hapa. Mambo makubwa sana ya maendeleo yamefanyika kwenye sekta zote za miundombinu; barabara, usafirishaji, umeme, yote kwa ujumla kafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya huduma za jamii, afya, maji, elimu, kafanya mambo makubwa sana. Watanzania wanayajua na dunia inajua. Tusimame imara kumtetea Mheshimiwa Rais. Vilevile, kwenye eneo la uchumi napo kafanya makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yangu ya kijimbo ambayo ningependa Mheshimiwa Waziri Mkuu ayachukue na kuyafanyia kazi ni mambo kama manne tu. Kwanza ni barabara namba nane. Wakati zinapitishwa hizi barabara kuu mwaka 1964 zilikuwa 26 tu; 1964 zilikuwa barabara kuu 26, hatimaye sasa hivi tuna barabara zaidi ya 138, lakini barabara namba nane ambayo ilikuwa namba nane tangu 1964 haijakamilika. Hili jambo naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alichukue ofisini kwake kwa ajili ya kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inatoka Mwanza, inapita Nzega, inapita Tabora, inapita Sikonge kwangu, inakwenda Rungwa, inakwenda Makongolosi, inakwenda mpaka Mbeya. Hii barabara ni kubwa sana, naomba Mheshimiwa Waziri

Mkuu aichukue aifanyie kazi, ili ikamilike. Vipande vitatu havijakamilika. Kipande cha kutoka Rungwa, cha pili ni cha kutoka Rungwa mpaka Makongolosi na cha tatu ambacho hakijakamilika ni cha Rungwa kupitia Itigi kwenda Mkiwa. Hivyo, vipande vitatu vikikamilika, barabara hii itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kukamilisha miradi ya maji ambayo ni mikubwa. Mradi wa maji wa kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye miji 28, huu ni mradi mkubwa sana ambao naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu azidi kuuwekea nguvu ya kiutekelezaji. Pia kuna miradi ya umwagiliaji ambayo nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote, hasa Waziri wa Kilimo, waendelee kuiangalia kwa karibu na Wizara ya Fedha iendelee kutoa fedha kwa sababu, umwagiliaji ndiyo ukombozi wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila umwagiliaji tukategemea mvua tu za Mungu inawezekana kama Taifa, tukakwama. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ni muhimu sana. Mradi wangu wa Uluwa ambao ulikwama tangu 2009, naomba nao upewe kipaumbele cha juu ili uweze kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mimi huenda ndio naongoza, jimbo langu ni kubwa kuliko yote. Kuna tarafa ambayo tumeiombea iwe jimbo jipya. Hakuna kata yoyote ambayo inaweza ikafikika kule kwenye Tarafa ile ya Kiwele bila kutembea zaidi ya kilomita 200. Kwa hiyo, kokote utakakokwenda kwenye Tarafa ya Kiwele ni lazima utumie kilomita 200. Ni kweli kuna watu 100,000 lakini hao watu 100,000 nao vilevile wanahitaji uwakilishi mzuri, uwakilishi wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa ili nitembelee jimbo, ni lazima nitumie mafuta ya zaidi ya shilingi 2,000,000. Wapo wenzangu hapa wanaweza kutumia mafuta ya shilingi 200,000 wakatembelea jimbo likakamilika, hata wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo lilikuwa la mwisho, na ninaomba sana haya niliyoyazungumza yawekewe kipaumbele. Nashukuru sana, Mungu azidi kumbariki Mheshimiwa Waziri Mkuu,

azidi kumbariki Mheshimiwa Rais na Serikali nzima kwa ujumla wake. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENNYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kakunda. Namwita mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na kumshukuru kwa utumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na kiukweli nchi hii tangu tumepata uhuru, tumekuwa na Mawaziri Wakuu takribani 14, mpaka yeye wa sasa hivi. Ukiachana na Mheshimiwa Daktari Frederick Sumaye, Waziri Mkuu mstaafu, miongoni mwa wale 13 aliyefuata kwa kukaa miaka mingi mpaka sasa hivi ni Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na kwamba ni jambo ambalo ameweka rekodi yake, pamoja na kufuata rekodi ya Mheshimiwa Frederick Sumaye, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi binafsi kabla hata sijaingia huku Bungeni nimekuwa nikimfuatilia kama kiigizo chema. Kwa sababu, Mheshimiwa Waziri Mkuu watu wote wanaomfahamu hata ukiwa unazungumzanaye ni mtu mstaarabu sana, *very humble*. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana baba yetu kwa utumishi wako, *humbleness* yako na namna ambavyo upo tayari kuwasikiliza watu, wote ni wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka hata mara ya kwanza kabisa nimekuja, miongoni mwa watu ambao niliendakusalimiana nao, alikuwa ni yeye. Tunasema hivyo kwa sababu, pia amemsaidia sana Mheshimiwa Rais katika majukumu yake kwa nafasi yake kama kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu bado ana nguvu, inawezekana bado akaendelea kutumika katika maeneo mengine, lakini sidhani kama kuna mtu ana

wasiwasi na utendaji wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na *humbleness* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia sehemu chache sana kwa sababu, nawakilisha kundi la vijana katika Bunge hili, itakuwa siyo busara na hawatanielewa kama sitazungumza kuhusu tatizo la ajira kwa vijana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Wajumbe wa Kamati wametoa maoni yao, nami nakubaliana na mapendekezo na maoni ya Kamati kuhusiana na suala la ajira, hususan katika ile mifuko ya kukopesha vijana. Pia, tunaipongeza Serikali kwamba wameamua warudishe utaratibu mpya wa kukopesha vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja *specific,* wakati sisi vijana wa nchi hii bado hatujatosha kwenye ajira za Serikali zinazotangazwa katika soko la ajira, bado kuna *gap* kubwa sana. Watanzania wengi vijana bado wana changamoto ya kujikimu kwa sababu, hawawezi kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sisi tuko katikati ya lindi hilo, kumeibuka wimbi kubwa la raia wa kigeni ambao wanafanya kazi za wazawa, kinyume na Sheria ya Mwaka 2015 ambayo inaitwa Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Nchini. Sasa, watu wanafahamu kuna maeneo ambayo raia wa kigeni, ambao wengine ni wachina na waturuki, wanafanya mpaka Uber na Bolt; wanafanya kazi ambazo tungeweza kufanya sisi Vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hawa raia wa kigeni wamejaa pale Kariakoo kiasi kwamba, wanauza mpaka hereni za shilingi 3,000. Sasa sisi kama vijana wa Tanzania, mawinga wa pale Kariakoo, watafanya shughuli gani? Kwa hiyo, niliona ni busara sana tuliangalie hili jambo. Ni jambo ambalo kwa kweli, linaathiri shughuli za wazawa kama sisi, Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia pia, utafahamu kwamba, raia hawa ambao ni wa kigeni wanafanya shughuli mpaka za kwenda kugonga nyumba za watu, nyumba moja baada ya

nyingine, wanakuwa wana kigari chao wamejaza vyombo mle, wanapita nyumba moja baada ya nyingine, wanakuwa na Mtanzania mmoja wamemtanguliza pale. Sasa tunakwenda wapi? Tunajua kuna utaratibu wa kuratibu ajira za wageni, lakini wamefika hatua ambayo mpaka sisi tunashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna mnyororo wa thamani kuichumi hapo katikati. Watanzania walikuwa wanaweza kwenda China wanafunga mzigo, wanakuja hapo Dar es Salaam, Kariakoo, wanawauzia wengine wa hapa ambao na wao watachukua, watapeleka pale Singida Mjini. Wengine wanaotoka Ikungi watakwenda Singida Mjini, watachukua mzigo watapeleka Ikungi, wakifika pale Ikungi kuna mwingine atachukua, atapeleka ndani ndani huko, Isuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa katikati kote wanakopita kuna hela ambayo inaachwa, ambayo hawa ni Watanzania walikuwa wanapata chochote katika huo mnyororo. Sasa hivi kama raia wa kigeni anaweza kutoka China moja kwa moja akachukua hela za katikati hapa, zote akachukua yeye, maana yake hapa sisi Watanzania twende wapi? Sisi kama raia wa Tanzania, vijana wa Tanzania, waende wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado siamini kabisa kwamba, imefika hatua tumeshindwa kufuatilia hili jambo na kulidhibiti. Naomba wakati Waziri anakuja kufanya hitimisho, Serikali itueleze wanachukua hatua gani kudhibiti wimbi kubwa la raia wa kigeni ambao wanakuja Tanzania? Wanakuja kwenye nchi yetu wanakwenda mpaka vijijini kufanya shughuli ambazo zingeweza kufanywa na vijana wa Tanzania na akina mama wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini tuna intelijensia ya kutosha kubaini ninavyovisema. Naomba msipige hoja rungu, nendeni mkafuatilie ili mjue kama hiki kitu kipo na kinafanyika kwa sababu, kinazungumzwa kila siku. Leo kulikuwa kuna uwezo, mama yule akaweza kwenda dukani, akanunua mchele kwenye duka la Mangi, halafu akarudi kwenye kibanda chake cha kupikia mama lishe akapika wali, akapika na vitumbua, asubuhi akauza vitambua kwa yule yule Mangi anayeuza duka…

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hanje, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**TAARIFA**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa. Nataka nimpe Taarifa mchangiaji anayechangia sasa. Ni kweli kabisa anachokisema. Ukiangalia ndugu zetu wa nchi za jirani wamekuwa wakienda mpaka kwenye mashamba yetu huko vijijini wakati huu wa mavuno. Wanakwenda kule kuwarubuni wananchi kununua mazao kwa bei ya chini, wanapeleka mpaka mifuko kule mashambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani ipo haja ya kuhakikisha kwamba, halmashauri zetu kule usimamizi uwe mzuri kwa sababu, mimi ninachofahamu huwezi kutoka hapa ukaenda nchi za jirani, za wenzetu, ukaingia mpaka mashambani kwao. Kwa hiyo, wanaona kuna *loophole* katika nchi yetu ya Tanzania ya kwenda huko na kufanya vitendo kama hivyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hanje unapokea taarifa hiyo?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, raia wa kigeni wanakopesha, mpaka ile ya kukopesha buku buku, kila siku wanaenda wanagonga, kama Waha. Waha wamerudi wote Kigoma kwa hiyo, napokea taarifa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwenye hoja yangu ya pili. Nitazungumza kuhusiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Nchini, Jenerali Erasto Lyimo, nafikiri jina sijalikosea. Wanafanya kazi nzuri sana kwa sababu, najua waathirika wakubwa wa dawa

za kulevya nchini ni pamoja na vijana. Kuna sababu nyingi, sidhani kama kuna muda wa kuzizungumza sababu ambazo zinasababisha watu waingie kwenye dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana kwa jambo moja. Mpaka sasa hivi wameweza kutumia teknolojia kwa ajili ya kubaini, kufuatilia na kudhibiti dawa za kulevya nchini. Tunapoteza vijana wengi sana kwa sababu ya matumizi ya dawa za kulevya. Ukienda kwenye zile sehemu za uraibu, unaweza ukaumia roho sana. Kwa hiyo, nawapongeza na ninawaomba wasiache kwa sababu, sasa hivi huko Dar es Salaam hakufai, yaani kuna hizo *bar;* wana shisha humo, hapafai kabisa. Tunaomba mwendelee kukazia hapo hapo na Serikali itawaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa, siyo kwa umuhimu, niwaambie tu, hakuna mtu anayeweza kuzuia uchaguzi jamani. Kuna vitu vingine unaweza ukampa mtu jina bure. Kulikuwa hata hakuna haja ya kufanya naye jambo lolote, lilikuwa ni jambo la kuliacha lipite tu. Hakuna mtu mwenye uwezo wa kudhibiti uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA. Pale hakuna hata wapigakura 5,000,000. Huwezi ukawaambia watu wazunguke mikoani wakatafute *signature* milioni 15, ya nini? *Automatically* ni *natural death.* Kwa hiyo, hakukuwa na haja ya kutumia nguvu. Achaneninao, hawana hata fedha za kuzunguka kwenye mikoa kufanya mikutano ya hadhara huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri shughuli nyingine, Mheshimiwa Waziri Mkuu kama alivyoongeza bajeti, nimeona bajeti ya uchaguzi imeongezeka, hebu twende kwenye mambo ya msingi. Watu wengine wanafanya shughuli nyingine, wanaweza kuanzisha wakawa kikundi cha harakati kwenye nchi, viko vingi. Kuna *NGO's* za harakati zimesajiliwa, lakini masuala ya uchaguzi nafikiri msiondoke kwenye *focus,* tuendelee kwenye masuala ya uchaguzi, watu watafanya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkitaka kujua kama hakuna anayeweza kuzuia uchaguzi, kama kungekuwa kuna watu wa kuzuia uchaguzi, hata jana pale wakati wanamchukua, wasingemchukua. Achaneni na hizo habari, twendeni kwenye *focus,* uchaguzi upo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hanje.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kikao chetu cha leo. Kwa hiyo, naahirisha Bunge mpaka kesho, Siku ya Ijumaa, Tarehe 11 Aprili, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.10 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 11 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*